# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Sita – Tarehe 04 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwashilishwa Mezani na: -

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka.

Na. 90

### Uratibu wa Ahadi za Viongozi Wakuu

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je, Serikali inatumia utaratibu gani wa kuratibu na kutekeleza ahadi za Viongozi Wakuu nchini ili zisionekane ni za uongo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa ahadi zinazotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa, wanaposhiriki katika matukio mbalimbali ya Kitaifa ikiwemo mikutano na wananchi pamoja na Kampeni za Uchaguzi Mkuu. Mara baada ya viongozi hao kutoa ahadi au maagizo, Ofisi Binafsi za viongozi hao kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu huziwasilisha kwenye Wizara za kisekta kwa ajili ya utekelezaji na kutoa mrejesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha taarifa za utekelezaji wa ahadi hizo zinazowasilishwa zinakuwa na uhalisia, Ofisi ya Waziri Mkuu ilibuni na kuanza kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa

Uratibu na Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali *(Dashboard)*. Mfumo huo, umeimarisha uratibu na ufuatiliaji wa ahadi hizo, kuweka kumbukumbu za ahadi hizo na kuwawezesha wataalamu kutumia muda mfupi kutuma maelekezo na kupokea taarifa za utekelezaji kutoka kwenye Wizara na Sekta husika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, majibu ambayo yanatia moyo na kuonyesha kwamba ni kweli kuna uratibu. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa sababu ahadi hizi huwa zinatekelezwa kwenye Wizara za Kisekta. Je, Serikali haioni umuhimu, huko kwenye Wizara za Kisekta kukawekwa mafungu maalumu, yaani kwenye bajeti ikaonekana kwamba fedha hizi zinakwenda kutekeleza ahadi fulani ili Wabunge waweze kufuatilia pale ambapo bajeti hiyo inaweza kutekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kule kwangu barabara ya Nangurukuru – Liwale na Nachingwea – Liwale, ni miongoni mwa ahadi za Uchanguzi wa 2015/2020. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya utekelezaji wa ahadi hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Kuchauka kwa kazi, lakini nimwambie kwenye hili la Wizara za Kisekta, ahadi za viongozi ni kipaumbele cha kila sekta wanapowasilisha bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wamekuwa wakiendelea kuziweka kila wanavyowasilisha bajeti zao. Sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, tunafanya kazi ya kuratibu kuhakikisha kwamba ahadi hizi zimewekwa na kama nilivyosema kwenye *dashboard* tunaona kila ahadi imefikia hatua gani na asilimia ngapi kwenye utekelezaji, kwenye kila sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Halmashauri ya Liwale kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwaka jana tu tumetoa fedha kwenye yale maafa yaliyotokea ya *El Nino* na Kimbunga Hidaya, shilingi bilioni 1.3 ili kuweza kuendelea kutengeneza barabara zile. Lakini pia, bajeti yako Mheshimiwa Mbunge Kuchauka imeongezeka kutoka shilingi milioni 839 hadi tunavyoongea leo ni shilingi bilioni 2.4. Nataka nikuhakikishie, ahadi zote za Viongozi wetu Wakuu tunaendelea kuzifanyia kazi. Sisi tunawaomba Watanzania waendelee kutuamini, waendelee kuiamini Serikali ya Awamu ya Sita, kwa sababu ahadi zote ni vipaumbele vya Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini ahadi ya Waziri Mkuu ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Butimba itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hilo swali linakuwa tofauti na swali la msingi, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri hebu mjibu tu, Serikali mna majibu mengi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niagize Wizara ya Kisekta iendelee kulifanyia kazi jambo la Mheshimiwa Mbunge ambalo ameulizia kuhusu ujengaji wa kituo hicho cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na. 91

**Mstaafu Kudai Fedha ya Usumbufu**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza: -

Je, Mstaafu aliyecheleweshewa kupata mafao, anaweza kudai fedha kutokana na usumbufu alioupata wakati anasubiri mafao yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PSSSF* katika vifungu 49(3) na 43(3) mtawalia, vinaeleza kuwa endapo mfuko utachelewesha kulipa mafao kwa mwanachama na ucheleweshо huo haukusababishwa na mwanachama mwenyewe au mwajiri, Mfuko utamlipa mwanachama huyo mafao yake pamoja na riba ya 15% kwa mwaka, ya kiasi atakachokuwa amelipwa kama mafao kwa Mfuko wa *NSSF* na asilimia tano kwa Mfuko wa *PSSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, sheria imetoa haki ya mwanachama kulipwa fidia endapo atacheleweshewa kulipwa mafao yake ikiwa ucheleweshaji huo umesababishwa na mfuko, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Maelezo yake yanaeleweka kwa sababu yeye amepita kwenye sheria, lakini nataka kujua ni sababu zipi za msingi ambazo mara nyingi huchelewesha watu kupata mafao yao kwa haraka? Ingawa sheria ipo, lakini kuna kitu hapo nimekwambia cha msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kawaida, Serikali inafahamu tarehe ya wastaafu wake. Je, hawa wanaohusika kufanya shughuli hizo za wastaafu tunawadhibiti vipi ili nao wasiwajibike, kwa sababu na wao ni sehemu ya kuwafanya wale wastaafu wachelewe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana kwa swali hilo zuri. Tayari Serikali imeshachukua hatua. Utakumbuka Bunge lako lililopita tulifanya mabadiliko kwenye hizi sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa baada ya kutambua kwamba kulikuwa kuna changamoto zilizokuwa zinasababisha wastaafu kutokulipwa kwa wakati, moja ya changamoto ilikuwa kwamba, wanapoombwa nyaraka labda za tarehe ya kuajiriwa, lakini mwisho wanaombwa taarifa nyingine ambazo kimsingi mwajiri alipaswa kuwanazo; na upande wa mfuko pia, kulikuwa kuna changamoto za taarifa, na ukinzani wa taarifa. Hizi zilisababisha sana wastaafu hawa wakawa hawapati fedha zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubaini changamoto hizo pamoja na nyinginezo za kifedha na hali ya mifuko, tulileta mabadiliko ya sheria hapa. Tulitunga sheria na baadaye Bunge lako Tukufu lilipitisha mafao kwamba lazima yalipwe ndani ya siku 60 na ikiwa hayajalipwa ndani ya siku 60 ndiyo inatokea hiyo *interest* ya kulipwa 15% kwa asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika eneo la uwajibikaji. Tumekuwa na uwajibikaji mkubwa kwa sababu sheria hizi sasa tumekuwa tukizitekeleza kuhakikisha kwamba mfanyakazi ambaye kabla ya kustaafu kwake ndani ya miezi mitatu, taarifa zake zinatafutwa, zinahakikiwa na wakati unapokuja kufika analipwa. Hizo siku 60 tulizoziweka kwa mujibu wa sheria, mara nyingi hazitimii, wengine wanalipwa ndani ya siku tatu, ndani ya

siku saba. Yaani siku 60 ni *threshold* ya mwisho kabisa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesha-*advance* kwenye Mfuko wa *NSSF* na *PSSSF*. Sasa tunatumia Mifumo ya TEHAMA na taarifa zinatolewa kiganjani kwa kutumia simu ya kiganjani *(smartphone)* kwa wafanyakazi ambao hata wale wanaolekea kustaafu. Kwa hiyo, taarifa zao za mifuko na michango zinatolewa kule. Kwa hiyo, hilo tatizo halipo tena, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwenye mifuko wameweka hiyo *penalty*. Sasa kwa Serikali mmeacha wazi, ni nini kinachosababisha kukae wazi? Napenda Serikali ituambie upande wa Serikali kwa nini nao hawajaweka *penalty* wanapochelewesha mafao ya mstaafu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, Mfuko wa *NSSF* unalipa 15% na hiyo ilikuwa ni riba kwa maana ya ucheleweshaji. Hata upande wa Serikali Mfuko wa *PSSSF* ukichelewesha mafao unalipa asilimia tano ya ucheleweshaji. Kwa hiyo, ni sahihi kwamba upande wa Serikali na *Private Sectors* kote kuna adhabu ikitokea kuna ucheleweshwaji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Antipas Zeno.

Na. 92

**Kukamilika kwa Miradi ya Afya Wilaya ya Malinyi**

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA K.n.y. MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za kukamilisha miradi ya Hospitali ya Wilaya ya Malinyi na Kituo cha Afya cha Ngoheranga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Malinyi ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 3.6 zimetolewa na kuwezesha ujenzi wa majengo 15, ambayo yamekamilika na yanatoa huduma mbalimbali ngazi ya hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali ilitoa shilingi milioni 570 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ngoheranga ambapo jumla ya majengo matano, ujenzi umekamilika na kituo kimeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyosalia katika Hospitali ya Wilaya pamoja na Kituo cha Afya cha Ngoheranga, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamguna.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Malinyi ni hospitali kubwa kweli, imejengwa vizuri na majengo mazuri sana, lakini Hospitali ile ina upungufu wa wahudumu, hasa wataalamu wa magonjwa ya wanawake *(Gynaecologists)*. Je, ni lini Serikali itapeleka wataalamu hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Kituo cha Afya cha Ngoheranga ni kituo ambacho kilijengwa kwa nguvu za wananchi walijitolea, lakini mpaka leo hakina wodi za watoto na watu wazima. Je, ni lini Serikali itaenda kusaidia kumalizia ujenzi huo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia ustawi wa wananchi wa Mkoa wa Morogoro na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimhakikishie kwamba, tunatambua kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha kujenga Hospitali nzuri ya Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi. Tunafahamu kwamba, kila mwaka watumishi wameendelea kupelekwa ili kupunguza pengo la watumishi katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kibali cha mwaka huu, Mheshimiwa Rais ametoa watumishi zaidi ya 10,183 na Halmashauri ya Malinyi pia imepata watumishi hao. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba, Serikali itaendelea kuajiri kila vibali vinavyojitokeza na kuwapeleka watumishi kwenye Hospitali ya Wilaya ya Malinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuhusiana na Kituo cha Afya cha Ngoheranga, tunafahamu wananchi walitoa nguvu zao. Nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Ngoheranga kwa kutoa nguvu zao kuchangia ujenzi wa kituo cha afya. Pia, Serikali ilipeleka shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho ambacho kimekamilika na kinaendelea kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu ujenzi wa hivi vituo vya afya unakwenda kwa awamu; tumeanza na majengo haya matano, lakini tutaendelea na wodi nyingine ikiwemo wodi ya watoto mpaka kituo kiweze kutoa huduma zote ambazo zinahitajika ngazi ya kituo cha afya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha Kituo cha Afya cha Nyakagwe, Kata ya Butobela?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya ambacho kipo katika Jimbo la Mheshimiwa Magessa ni kweli Serikali ilishapeleka fedha na ujenzi umefanyika, lakini tunafahamu bado baadhi ya majengo hayajakamilika. Naomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea na ujenzi wa hicho kituo cha afya kwa awamu na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka na kukamilisha majengo ambayo yamesalia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kituo cha Afya Ilunda kimebakiza takribani shilingi milioni 100 tu kianze kazi na mpaka sasa hakijaanza. Ni lini Serikali itatupatia fedha hizo ili kumalizia Kituo cha Afya Ilunda na wananchi waendelee kupata huduma ya upasuaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Ilunda kilipelekewa fedha na Serikali Kuu na ujenzi wake uko zaidi ya 95%. Tunafahamu kwamba, kuna kiasi cha fedha ambacho kinahitajika kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Isack kwamba, fedha hizo zitapelekwa kupitia mapato ya Serikali. Inawezekana ikawa ni mapato ya ndani ya halmashauri au mapato kutoka Serikali Kuu, ilimradi Kituo kikamilike na kianze kutoa huduma kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Serikali itapeleka shilingi milioni 125 kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Afya Bugalama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Bugalama katika Jimbo la Geita Vijijini kilipelekewa fedha na Serikali na ujenzi wa majengo yake umefikia zaidi ya 90%. Tunafahamu kwamba, kuna baadhi ya majengo ambayo yanahitaji fedha hiyo shilingi milioni 123 na zaidi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Musukuma kwamba, Serikali itaendelea kutafuta fedha na kupeleka kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

Na. 93

**Hitaji la Watumishi na Vifaa tiba Hospitali ya Wilaya Mbulu**

**MHE. REGINA N. QWARAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka vifaa tiba na watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilipokea shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu, ambapo imepelekewa shilingi milioni 800. Vituo vya afya vimepelekewa shilingi milioni 600 na zahanati zimepelekewa jumla ya shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada za afya na kuwapeleka katika vituo vya huduma kote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ambapo katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025, jumla ya watumishi 177 wa afya wameajiriwa na kati yao watumishi 70 wamepangwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu na wengine katika vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri, vituo vya afya na zahanati kote nchini, pamoja na kuajiri wataalamu wa kada mbalimbali za afya na kuwapanga katika maeneo yenye upungufu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa huduma ya upasuaji ni muhimu sana, hasa kwa akina mama wanapokwenda kujifungua. Wilaya ya Mbulu kwenye hii hospitali bado huduma hiyo haijaanza kwa sababu ya ukosefu wa taa za upasuaji na vitanda vya upasuaji. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka vifaa hivyo ili huduma hii ya upasuaji iweze kuanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali itapeleka shilingi milioni 220 ili jengo la *maternity ward,* jengo la watoto, jengo la wanaume na jengo la wanawake yakamilike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ni moja ya hospitali ambazo zimeanza kujengwa katika kipindi cha mwaka 2018/2019. Nilifanya ziara katika hospitali ile na niliona kwa kiasi kikubwa majengo yalikuwa hayajakamilika. Hata hivyo, kuna hatua ambazo zilichukuliwa na tukakamilisha majengo yaliyo mengi, ila bado ukamilishaji wa jengo la upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri kwamba, kwa kupitia mapato ya ndani na fedha za vifaa tiba ambazo Mheshimiwa Rais amezipeleka kwenye halmashauri zote 184 katika mwaka 2024/2025 wa fedha, ambapo kila halmashauri imepata kati ya shilingi milioni 800 hadi shilingi bilioni tatu, waweke kipaumbele kwenye kununua taa kwa ajili ya jengo la upasuaji, ili jengo hilo lianze kufanya kazi kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa Wilaya ya Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na fedha shilingi milioni 200 ambazo zinahitajika kwa ajili ya ukamilishaji wodi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itapeleka fedha hizo ili kukamilisha majengo hayo kwa ajili ya kuboresha huduma za wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutujengea hospitali ya Wilaya katika Kata ya Mabogini, na hospitali hii karibu inakamilika. Je, ni lini Serikali itapeleka vifaatiba na wataalamu ili wananchi wa eneo hili waanze kupata huduma?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu

Spika, ni kweli kwamba Serikali ilipeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya mpya katika Halmashauri ya Moshi Vijijini katika Kata ya Mabogini, na niwapongeze wananchi kwa kushiriki katika ujenzi wa hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali dhamira yake ni kuhakikisha hospitali hiyo inakamilika kwa wakati, na inapelekewa vifaa tiba ili ianze kutoa huduma mapema iwezekanavyo. Kwa bahati njema, Mheshimiwa Rais ameshatoa fedha kwenye kila halmashauri katika mwaka huu wa fedha ikiwemo Halmashauri ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Niabu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi kuweka kipaumbele kwenye vifaatiba vya muhimu ili hospitali ianze kutoa huduma na kuhudumia wananchi ipasavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imejenga hospitali nzuri na ya kisasa Wilaya ya Tanganyika na wakati huo huo hakuna watumishi kwenye hospitali ya wilaya na vituo vya afya, ni lini Serikali itapeleka watumishi kwenye hospitali ya wilaya sambamba na vituo vya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mpango mkakati wa kuajiri watumishi wa Sekta ya Afya, na pia huwapeleka katika vituo vyenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi. Katika *Portal* yetu ya ajira, watumishi wanaelekezwa zaidi maeneo ya pembezoni ikiwemo Halmashauri ya Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba Serikali katika miaka yote kuanzia mwaka 2021 mpaka sasa imeendelea kupeleka watumishi

kwenye hospitali ya Wilaya ya Tanganyika pamoja na vituo vya afya na zahanati na tutaendelea kuelekeza watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kibali cha mwaka huu ambacho watumishi 10,183 wameajiriwa hivi karibuni, wapo ambao wameelekezwa Tanganyika, na zoezi hili ni endelevu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Karatu, na pia tuna vituo viwili vya afya ambavyo vina upungufu. Kituo cha Afya Kambi ya Simba na Kituo cha Afya Mbuga Nyekundu, vina upungufu wa watumishi, vifaatiba na ukosefu wa *standby generator* ili huduma ziweze kutolewa saa 24. Nini mkakati wa Serikali kuondoa upungufu huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imejenga Hospitali Halmashauri ya Karatu, Kituo cha Afya Mbuga Nyekundu na bahati njema nilifanya ziara pale, niliona ujenzi mzuri. Nimhakikishie tu kwamba safari ni hatua, tumepeleka vifaatiba kwa kiasi na mwaka huu wa fedha Mheshimiwa Rais amepeleka zaidi ya shilingi bilioni moja katika Halmashauri ya Karatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, watumishi walioajiriwa ni zaidi ya 10,183. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Paresso kwamba ni kipaumbele cha Serikali kupeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika Hospitali ya Karatu na vituo na zahanati. Pia, tutahakikisha tunaipa kipaumbele halmashauri hiyo katika watumishi kwa kila kibali kinapotoka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya kuboresha Zahanati ya Narumbegu kwa sababu wananchi, hasa wanawake na watoto hutoka pale na kwenda wilaya nyingine kwa ajili ya kupata huduma ya afya? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza mama yangu Mheshimiwa Salma Kikwete, kwanza kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na nafahamu Serikali ya Awamu ya Sita hivi karibuni imepeleka zaidi ya shilingi milioni 600 katika Kituo chake cha Rutamba ambacho amekuwa anakisemea muda mrefu.

Mheshimiwa naibu Spika, pia nimhakikishie tu kwamba katika Zahanati hiyo ya Narumbegu na maeneo mengine yote ya kimkakati ambayo ni vijiji vyenye idadi kubwa ya wananchi na umbali mkubwa kwenda kwenye vituo vingine vya huduma, tutahakikisha tunaweka kipaumbele kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya. Kwa hiyo, eneo hilo tumelichukua na tutalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Twaha Ally.

Na. 94

**Mkakati wa Kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti Kuuza *Carbon Credit***

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza: -

Je, ni nini mkakati wa Serikali kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kupata Mapato kwa kuuza *Carbon Credit?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Biashara ya Kaboni kwa ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini, Kifungu cha 15 - 18. Serikali inaendelea kubainisha fursa mbalimbali zinazopatikana katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo fursa ya kaboni katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti ambapo ikianza kuuzwa itaongeza mapato kwa halmashauri na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa wadau watatu wameonyesha nia ya kuwekeza katika Biashara ya Kaboni kupitia rasilimali za misitu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti. Wadau hao ni pamoja na *Amaly Asset Management LTD, TAZA Nature Company LTD na WWF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri kwa kushirikiana na wadau walioonyesha nia ya kuwekeza kwenye kaboni wanaendelea kutambua maeneo yatakayoweza kutumika ili waweze kusajili miradi na kuanza uzalishaji kwa kuzingatia makubaliano ya Mkataba wa Paris Ibara ya Sita. Aidha, Serikali inazisisitiza halmashauri zote kote nchini zenye fursa ya misitu kuchukua hatua za kuanza biashara ya kaboni ili kuongeza mapato ya ndani na kuhifadhi misitu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yustina.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni kwa kiasi gani wananchi wa Tanzania wana ufahamu kuhusu hiyo biashara ya *Carbon Credit?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hilo swali linataka takwimu, Waziri hawezi kulijibu sasa hivi. Tunaendelea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua.

Na. 95

**Uhitaji wa Umeme kwenye Machimbo ya Madini – Kilindi**

**MHE. OMAR M. KIGUA** aliuliza:-

Je, upi mpango mkakati wa kufikisha nishati ya umeme kwenye maeneo yote ya uchimbaji wa Madini – Kilindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi ina maeneo yapatayo 12 ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ambapo kati ya hayo, maeneo manne tayari yameshapatiwa huduma ya umeme. Maeneo hayo ni Mafulila, Mfyalime/Najim, Masagulu Muheza na Chanungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, eneo la Matanda, mkandarasi aitwaye *DIEYNEM Company Ltd* anaendelea na kazi ya kuweka miundombinu ya umeme na anatarajia kukamilisha kazi hiyo hivi karibuni. Maeneo mengine yaliyosalia yatapata umeme kupitia miradi mbalimbali itakayofuata, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMAR M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kuweza kupeleka umeme kwenye maeneo manne ambayo yalikuwa yana uhitaji mkubwa sana kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Je, ni lini sasa maeneo nane yaliyobaki yataweza kupelekewa umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kwamba, tuna Mradi wa Gridi Imara ambao unaanzia Mkata hadi Kilindi kwa ajili ya kuimarisha umeme maeneo mbalimbali, lakini mradi huo umesimama. Je, nini mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba mradi ule unaendelea? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na maeneo nane ambayo yamebakia, Serikali inayo miradi ambayo tutaianza mwaka huu wa fedha. Kwa maeneo haya nane ya Mheshimiwa Mbunge, nitakaa na *REA* na kuwaambia katika maeneo ambayo tunayatenga kupeleka umeme kwenye vitongoji, basi na maeneo ambayo vitongoji hivi vinapita waweze kupata umeme kwa ajili ya kuimarisha shughuli hizo za uchimbaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Mradi wa Gridi Imara wa Mkata na Kilindi tutahakikisha tunaendelea na mazungumzo na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili fedha ziweze kutoka kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** *Advocate* Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kiteto umeme ulikuwa unakatika sana, mara kwa mara, na ni kwa muda mrefu sasa, na imeleta madhara ya kuunguza vifaa vya wananchi. Nini kauli ya Serikali? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunao utaratibu wa kuwalinda walaji kupitia *EWURA,* ambapo mwananchi ambaye amepata athari kutokana na matumizi ya umeme, kuna utaratibu wa kufuata kuleta malalamiko, na kisha

kuna utaratibu wa kuyafanyia kazi na kuona kama anastahili kupewa fidia au vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi kutoka kwenye jimbo lake tufuate utaratibu ambao tunao, mwananchi yeyote ambaye amepata athari hii, upo utaratibu wa kupata haki yake, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

Na. 96

**Kumaliza Kusambaza Umeme kwenye Vitongoji**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza kusambaza umeme kwenye vitongoji nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Januari, 2025, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* imekamilisha kupeleka umeme kwenye vijiji vyote 12,318 nchini. Aidha, Serikali imepeleka umeme kwenye vitongoji 33,657 kati ya vitongoji 64,359 sawa na 52.3%. Vitongoji 30,702 vilivyobaki vipo kwenye mpango wa kupatiwa umeme kupitia miradi ya kusambaza umeme katika vitongoji ambapo Serikali imeandaa Mpango wa kupeleka umeme katika vitongoji 20,000 kwa kipindi cha kati ya miaka mitano mitano hadi kumi 10 kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024. Mpaka sasa vitongoji 4,020 vipo katika Mpango wa utekelezaji kupitia miradi mbalimbali. Serikali inajipanga katika miradi mingine ya kupeleka umeme vitongojini kulingana na miradi itakayofuata, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuongeza kasi katika kupeleka umeme kwenye vitongoji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Nini mkakati na mpango madhubuti wa vitongoji vilivyobaki katika Mkoa wangu wa Tabora?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge. Kuhusiana na Serikali kuongeza kasi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji, tayari kwa mwaka huu wa fedha katika mradi wetu wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 20,000 kwa awamu tulikuwa tumepanga vitongoji 4,000, lakini Serikali imetafuta fedha takribani shilingi trilioni 1.5 na sasa tutapeleka umeme kwenye vitongoji 8,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imejidhatiti kuongeza kasi katika kupeleka kwenye vitongoji. Kuhusiana na umeme Tabora, Tabora kuna vitongoji takribani 3,700. Tumeshapeleka umeme kwenye vitongoji takribani 1,300 na mwaka huu wa fedha tutapeleka umeme kwenye vitongoji takribani 663. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Mkoa wa Tabora Serikali imejipanga kuendeleza miradi ya vitongoji katika mkoa huo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itaanza ule utaratibu wa kusambaza umeme kwenye mitaa 15 kwenye kila jimbo ikiwepo Iringa Mjini, Mtaa wa Mtalagala na Msisina?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mkandarasi yuko *site* na ameshamaliza uhakiki katika mitaa yote 15. Kwa hiyo, sasa hivi yupo katika hatua ya manunuzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mkandarasi yupo *site* na atamaliza manunuzi hivi karibuni na kazi itaanza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Serikali kwa kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Wilaya ya Lushoto, lakini pamoja na jitihada hizo, kupata umeme ni jambo moja, lakini upatikanaji wa umeme ni jambo lingine. Kwa takribani wiki ya tatu sasa Wilaya ya Lushoto iko gizani, hakuna umeme kwa sababu maeneo mengi miti imedondoka na imedondosha nguzo. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba Wilaya ya Lushoto inapata umeme wa uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Mbunge yuko sahihi kwa takribani mwezi sasa Wilaya ya Lushoto imekuwa ina mvua nyingi pamoja na upepo mkali. Kwa hiyo, inasababisha nguzo kuweza kudondoka. Tayari nimeshafanya kikao na Meneja wa Lushoto na viongozi wa Makao Makuu na tumekubaliana yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tutawapatia Mkoa wa Tanga *concrete poles* (nguzo za zege) 1,000 na 400 zitaenda eneo la Lushoto, hususan eneo la Mlalo ambapo *line* hii imeathirika kwa kiasi kikubwa. Nimeshamwelekeza Meneja kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri kuhakikisha hizo *concrete poles* zinakaa kwenye maeneo ya kawaida. Hata hivyo, kwa kuwa Lushoto kuna milima mikali, nimewaelekeza *TANESCO* waje na mkakati wa nguzo za chuma ili tuweze kuzipandisha kwenye maeneo ya milima mikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya nimewaagiza waende ili waweze kuwaomba wale wenye mashamba makubwa waturuhusu kupanua njia ya umeme ili tuweze kusafisha na kupunguza athari katika miundombinu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Lushoto, tumelichukua jambo hili kwa uzito mkubwa, na nimewaambia waje na *timeline* mahususi ya kufanyia kazi mikakati hii kwa ajili ya kupunguza changamoto hii katika Wilaya ya Lushoto, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maji, Mheshimiwa Anatropia.

Na. 97

**Kukamilisha Miradi ya Maji Kyerwa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, lini miradi ya maji Wilayani Kyerwa itakamilika ili Wananchi wapate huduma ya maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, swali Na. 97.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi sita ya maji katika Wilaya ya Kyerwa ambayo ni Runyinya - Chanya, Kikukuru, Kimuli – Rwanyango - Chakalisa, Kaisho - Isingiro, Nyamyaga - Nayakatera na Mabira. Hadi kufikia mwezi Januari, 2025, Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi miwili ya Nyamyaga – Nayakatera na Mibira ambayo inahudumia wananchi 26,218 waishio kwenye Kata za Bugomora na Mabira.

Ujenzi wa miradi iliyobaki upo katika hatua za mwisho za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, lakini kwa upekee sana nakuomba uniruhusu niseme haya. Hapa Bungeni Serikali imekuwa ikieleza mwaka 2024 wote kwamba inaenda kukamilisha mradi wa maji wa Kimuli – Rwanyango, mwaka mzima 2024 yamekuwa yakiongelewa haya lakini huo mradi haujakamilika na haujafanya chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, siyo hilo tu, kuna miradi Serikali hapa inataja kwamba imekamilika, lakini hiyo miradi haitoi maji. Nayaongea haya kwa sababu Kyerwa ni moja ya Wilaya ambayo ina changamoto kubwa ya maji. Licha ya kukaa kwenye mabonde na kuwa na mito ya kutosha, lakini Kyerwa haina maji. Kwa hiyo, nayaongea haya kwa masikitiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni lini hiyo miradi ya maji ambayo mmekuwa mkiitaja miaka yote itakamilika ili iweze kupunguza adha ya wananchi iliyopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kukamilika kwa hiyo miradi itasababisha kuanza miradi mingine ili Kata kama za Rwabwere, Songambele, Bugara na Businde ambazo nimekuwa nikikutumia picha wakinywa maji machafu na waki-*share* maji na ng'ombe. Ni lini hizo kata zitaenda kupatiwa maji? Naongea kwa uchungu sana kwa sababu wananchi wa Kyerwa wanalalamika sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kaa. Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, eneo la Kyerwa nimepata wasaa nami kuweza kufika, lakini kazi kubwa imefanyika na tuna miradi mingi ambayo inaendelea. Mheshimiwa Mbunge nakuomba, ukiangalia taarifa miradi mingi ipo kwenye 80%. Ukipata wasaa naomba leo tukutane, lakini kuna

kazi ambayo ni kubwa inafanyika nami nilipata wasaa wa kwenda kuzindua baadhi ya miradi. Nataka niwahakikishie wana Kyerwa, moja ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha wananchi wa Tanzania waishio mijini na vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Wanakyerwa jukumu hilo tunaliweza katika kuhakikisha miradi iliyobaki tunaikamilisha na wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kijiji cha Masimba ni miongoni mwa vijiji ambavyo bado vina changamoto kubwa sana ya maji Mvomero. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini mtatupa shilingi milioni 950 ambazo tuliomba kwa ajili ya kumaliza tatizo hili la maji katika Kijiji cha Masimba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Tumeshaanza kupokea fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali. Nataka nimhakikishie kwamba maeneo ambayo ameyataja tutabana kuhakikisha tunapeleka fedha na wananchi hao wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Mji wa Tukuyu, Wilayani Rungwe, una kata sita ambazo zinategemea tenki la maji, na Mheshimiwa Waziri, Aweso, alikuwepo wakati Mheshimiwa Rais anatoa maagizo kwamba lile tenki likamilike mara moja. Hata hivyo, mpaka sasa hivi tunaingia mwaka wa tatu lile tenki bado halijakamilika. Kata hizo sita za Bulyaga, Bagamoyo, Makandana,

na Msasani mpaka sasa hivi, hakuna maji kwenye Kata zote za Ibigi kwa sababu tenki halijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa busara na hekima za Mheshimiwa Waziri, naomba hawa watu wa Wilaya ya Rungwe wapate majibu sahihi juu ya tenki lao lile ambalo liko muda mrefu sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, tulipata *concern* ya madai ya mkandarasi juu ya utekelezaji. Katika ule mradi pamoja na ujenzi wa tenki pia tulifanya *pass way* ili kuhakikisha watu wanapata huduma ya maji safi na salama. Hata hivyo, alikuwa anadai kiasi cha shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuhakikishia kwamba tumeshamlipa na hawana kisingizio chochote. Kwa hiyo, jukumu lao ni kuhakikisha kazi ile inakamilika na wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji ya Mwika Kaskazini na Mwika Kusini ambayo ilikuwa imetengewa shilingi bilioni 2.7 ndani ya bajeti ya miaka mitatu iliyopita, lakini haijapewa fedha hata kidogo na kazi ndogo iliyofanyika pale imetokana na fedha za ndani kutoka kwenye mamlaka husika. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa tamko kwamba sasa fedha hiyo itaachiliwa ili miradi hiyo ikamilike na mwanamke wa Mwika Kaskazini na Kusini atuliwe ndoo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mzee wangu, Mheshimiwa Dkt. Kimei kwa kuwa kipindi hiki tupo katika kipindi cha Bunge apate wasaa wa kufika ofisini tuone

namna ya haraka tunaweza kuwasaidia wananchi wa Mwika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya kilimo. Mheshimiwa Nashon William.

Na. 98

**Miradi ya Umwagiliaji Uvinza kwa Mwaka 2023/2024**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza: -

Je, miradi mingapi ya umwagiliaji imepangwa kujengwa Wilayani Uvinza kwa mwaka wa fedha 2023/2024?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wilaya ya Uvinza ilikuwa na miradi minne ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Skimu za Kashagulu, Mgambazi, Nkonkwa na Ilagala. Aidha, hatua za manunuzi kwa ajili ya kumpata mshauri elekezi wa kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu zimekamilika na kazi za upembuzi yakinifu zitaanza mara baada ya hatua za kimkataba kukamilika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nashon.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi anayoitaja ya Kashagulu yote ilikuwepo. Sasa, nataka atoe ufafanuzi ili wananchi wangu wasikie na waelewe kwa nini inatajwa kama ndiyo miradi ambayo nimeiuliza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna miradi ambayo ilianzishwa katika Kijiji cha Nyanganga, Itebula pamoja na Nguruka mpaka sasa bado haijakamilika na ni muda mrefu sana. Je, ni lini miradi hii nayo itakwenda kukamilishwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza namthibitishia Mheshimiwa Mbunge wa Uvinza kwamba mradi kama wa Kashagulu ambao ulijengwa zamani haukuwa umefuata zile taratibu za ujenzi na hauja-*cover* eneo kubwa kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alituelekeza sisi kuhakikisha tunapitia miradi yote ya zamani na kujenga miradi mipya, ndiyo maana katika jimbo lake, moja ya miradi ambayo tunapitia ni pamoja na Mradi wa Kashagulu. Tunataka kuujenga kisasa na tunaupanua ili uweze kuhudumia wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maeneo ya Nguruka na Itebula na yenyewe tutaiingiza katika mpango unaofuatia kwa sababu tunafanya kwa awamu kulingana na bajeti ambayo Serikali inakuwa imetupangia. Kwa hiyo, na lenyewe uwathibitishie wananchi wa Uvinza kwamba hili litafanyika chini ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, mwaka 2024 Serikali ilifanilkiwa kutangaza tenda mbili za ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji wa Mbwasa na Udimaa. Taarifa niliyonayo ni kuwa wakandarasi walishapatikana. Je, ni lini wakandarasi wataenda *site* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hizo *schemes*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Manyoni ambako anatokea Mheshimiwa Dkt. Chaya, tayari miradi hiyo wakandarasi wamepatikana na nimwambie tu kwamba mwezi uliopita Januari, mwishoni Serikali ilishatoa fedha *(advance payment)* kwa ajili ya kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mradi wa Mbwasa anajenga mkandarasi anaitwa *Tonde Construction* ambaye tayari ameshapatiwa karibu shilingi bilioni moja za awali na anafanya *organisation* kwa ajili ya kuingia *site*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maganga, jiandae Mheshimiwa Njau.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Kata ya Isebya, Kijiji cha Mgelele tuna mradi wa kilimo toka mwaka 2023 tunauingiza kwenye bajeti. Serikali itatoa lini fedha ili utekelezaji wa mradi huo wa kilimo uanze? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mbogwe ambako anatokea Mheshimiwa Maganga, tunatambua kuhusu huo mradi, na ni kweli kwamba tunachotafuta sasa hivi ni fedha. Wizara ya Fedha imeshatuahidi kwamba itatupatia fedha katika mgao unaofuatia, maana yake tutatoa kwa ajili ya huo mradi kukamilika. Kwa hiyo, waondoe shaka wananchi wako jambo hilo litafanyika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na agizo la Serikali la kufufua zao la kahawa Mkoani Kilimanjaro, ipo mikakati mbalimbali inayowezesha kufufua zao hili ikiwemo kuboresha mifereji ambayo inapeleka maji katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya *Old* Moshi Mashariki, tangu mwaka 2009 walilaza mabomba na Serikali ilitoa shilingi milioni 240, mabomba yale yanaharibika. Nataka kujua ni nini kauli ya Serikali ya kuendeleza mifereji hii ili wananchi waweze kumwagilia zao hili na Serikali iweze kupata kipato? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nimwondoe shaka Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Felista Njau, vilevile, namtambua Mbunge wa Jimbo. Ni kwamba eneo hilo la Moshi Vijijini kuna kazi nzuri ambayo Serikali imeifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali ni kwamba tumeshaielekeza Tume ya Umwagiliaji kupitia mkoa kwamba wafanye *feasibility study* ili kujua gharama halisi za mradi ili tuje kuleta yale mabomba kwa ajili ya kusaidia wakulima wa kahawa katika Mkoa wa Kilimanjaro hasa katika Kata za *Old Moshi*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Shekilindi.

Na. 99

**Ujenzi wa Barabara ya Mkuzi hadi Mlola Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Barabara ya Mkuzi hadi Mlola Lushoto kwa mkupuo mmoja kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Magamba – Mkuzi hadi Mlola (kilometa 35.37) unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 5.33 kuanzia Magamba hadi Mkuzi zimejengwa kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu iliyobaki ya kutoka Mkuzi hadi Mlola (kilometa 30.04), Serikali itaendelea kuijenga kwa kadiri ya fedha zinavyopatikana, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, na pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Wakati Serikali inatafuta fedha, kwa nini isitenge fedha za dharura kutengeneza maeneo korofi ili wananchi waweze kupita hasa kipindi hiki cha mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara hiyo hiyo sehemu ya Kwai ina *sharp corner* (kona kali) na husababisha magari ya mizigo kushindwa kuzunguka pale. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kujenga daraja maeneo yale ili kukwepa kupita eneo hilo la kona kali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Tanga, aweze kufika kwenye barabara ya Mheshimiwa Mbunge na kuainisha maeneo yote ambayo yamekuwa korofi hasa katika kipindi hiki cha mvua ili aweze kuyakarabati, na ikiwezekana aweze kuleta taarifa Wizarani ili

wananchi waweze kuhakikisha kwamba wanapita katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la Kwai ambalo Mheshimiwa Mbunge anasema kuna kona kali, kwa kuwa Meneja atakwenda maeneo hayo aweze kufanya tathmini kama kuna uhitaji wa kujenga hilo daraja, basi aweze kuleta taarifa Wizarani ili mipango iwekwe kwa ajili ya kujenga hilo daraja eneo hilo lenye kona kali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni mara ya tisa nauliza swali hili kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni lini mshauri ambaye alitangaza hapa Bungeni kwamba ataniambia anaenda kuanza kazi ya upembuzi yakinifu wa barabara ya kutoka Kahama – Nyang'hwale – Busisi ili ijengwe kwa kiwango cha lami? Lini atatutangazia kuwa mpembuzi anaanza kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba baada ya hapa niweze kupata taarifa, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari hatua za manunuzi zilishaanza. Kuhusu ni lini ataanza, labda baada ya hapa niweze kutoka nijiridhishe ili nimpe tarehe na mwezi ambao hakika atakuwa yuko uwandani kwa ajili ya kufanya kazi ya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke, jiandae Mheshimiwa Grace.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kuwalipa fidia wananchi wa Mnanila ambao vibanda vyao vilibomolewa. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia

wananchi hao wa Mnanila Wilaya ya Buhigwe ambao ahadi yao ilitolewa mbele ya Makamu wa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa swali lako haliendani na swali la msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri, mjibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi hao wamefika mara kadhaa katika Wizara kufuatilia hiyo fidia na mpaka sasa hivi tunaendelea na majadiliano nao hasa wale ambao walikutwa nje ya eneo lenyewe. Kwa hiyo, Serikali tumeendelea kufanya mazungumzo pamoja na wenzetu wa mkoa ili kuona kama hawa wananchi walikuwa na haki au wao ndio walikuwa wameingia kwenye Barabara, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Iringa – Dodoma imechoka sana, ina mashimo mengi, haina hadhi ya barabara ya kuunganisha mkoa na mkoa. Ni lini Serikali itajenga upya barabara hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, siyo barabara hiyo tu, ziko barabara nyingi ambazo kwa kweli zinahitaji matengenezo makubwa ikiwepo hiyo Barabara ya Iringa – Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari sasa hivi tuko kwenye mipango ya kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo muda wake umepita ama zimechoka, tuweze kuziingiza kwenye mpango hasa hizi barabara kubwa za kiuchumi ili tuweze kuzitengeneza zirudi katika ubora wake unaostahili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini barabara ya kutoka Kolandoto – Kishapu – Lalago mpaka Meatu itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ipo kwenye bajeti yetu na tunaendelea kufanya taratibu za kuandaa makabrasha kwa sababu katika bajeti hiyo ambayo tunaitekeleza, hiyo barabara tumeipangia bajeti ili ianze kujengwa kwenye kipindi hiki cha bajeti. Kwa hiyo, taratibu zinaendelea, zikikamilika tutaanza kuijenga, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Sichalwe.

Na. 100

**Usafiri Kwenda Lubumbashi kwa Njia ya Ziwa Tanganyika**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kwa kushirikiana na Serikali ya *DRC* kuanzisha usafiri wa kufika Lubumbashi kupita Ziwa Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania *(TASHICO)* inakamilisha miradi ya ukarabati wa meli zake tatu ambazo ni *MV* Liemba na MV. Mwongozo zitakazofanya kazi kati ya Bandari za Kigoma na Karema kwa upande wa Tanzania na Bandari ya Kalemie kwa upande wa *DRC* na siyo Lubumbashi. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za ujenzi wa meli mpya

ya abiria na mizigo itakayofanya kazi kati ya nchi hizo mbili, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Lubumbashi ambayo jimbo lake kuu ni Haut-Katanga ni kati ya majimbo tajiri sana kwenye Nchi ya *DRC* na ni miongoni mwa jimbo ambalo Watanzania wengi wanalitumia kwa sababu hakuna vita…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikiwa wamekamilisha meli hizo kupitia Ziwa Tanganyika, mpango wa barabara baada ya kumaliza Ziwa Tanganyika kuelekea Lubumbashi umefikia wapi? Ndiyo hoja kubwa iko hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ikiwa Bandari ya Karema imejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 49 na imekamilika na mpango wa kujenga Bandari ya Karema ulikuwa ni kuepusha mlolongo wa kutoka Bandari ya Kalemie upande wa *DRC* ili kupatikane Bandari ya Moba; mpaka sasa hivi *DRC* hawana Bandari ya Moba, sisi tija ya kujenga bandari hii upande wa kwetu yenye zaidi ya shilingi trilioni 49 ni nini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge twende kwenye swali, acha stori kwenye Bunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna mahusiano mazuri na

wenzetu wa *DRC* na tunafanya shughuli nyingi kwa pamoja. Tunapoongea sasa hivi ni kwamba bahati nzuri wenzetu wa *DRC* na sisi hasa Wizara ya Ujenzi tuna timu ya pamoja ambayo inapitia uwezekano wa kujenga barabara kutoka kwenye bandari za upande wa *DRC* kwenda Lubumbashi. Tayari tuna timu ambayo inafanya hizo kazi, kwa hiyo, iko kwenye taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, itaangaliwa kama kutakuwa na tija na hiyo Barabara, basi tutasaidiana nao au tutatafuta utaratibu wa namna ya kuijenga hiyo barabara na wenzetu wa *DRC*…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Kuhusu Bandari ya …

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari ya Karema, haijafanya kazi vizuri sana, lakini tunavyoongea sasa hivi kwa upande wetu, Serikali tuna wakandarasi wawili ambao tumewa-*engage* kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mpanda – Karema na tayari wako *site*. Kwa hiyo, meli hizo zitakapokuwa zimekamilika, zinaweza kwenda kwenye bandari yoyote upande wa pili pale ambapo tutakuwa tumekamilisha barabara upande wetu na kwao kule. Kwa hiyo, taratibu zipo zinaendelea vizuri kati yetu na wenzetu wa *DRC*, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina utaratibu gani wa kurejesha usafiri wa meli baada ya Bandari ya Mtwara na Dar es Salaam kuimarika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri kwamba tulikuwa na usafiri huo, lakini baada ya kuwa na usafiri mzuri wa Barabara, tutaangalia uwezekano kama tukiwa na usafiri wa abiria wa meli itakuwa na tija ili tuweze kurejesha usafiri huo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

Na. 101

**Malipo ya Fidia kwa Wananchi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza: -

Je, lini Wananchi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza watalipwa fidia zao kwa kuwa tathmini imefanyika mara mbili sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Nyamagana zinaendelelea kukamilisha taratibu za uteuzi wa eneo ambalo litapangwa na kupimwa ili wananchi watakaoondolewa wamilikishwe kwa gharama nafuu. Katika zoezi hilo jumla Kaya zipatazo 1,404 zinatakiwa kupisha eneo la Uwanja wa Ndege wa Mwanza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Suala hili limechukua muda mrefu sana, wananchi wamekuwa wakipewa matumaini na

wamefanyiwa uthamini mara mbili, lakini leo wakati wanasubiri kulipwa, bado wanaambiwa Serikali inajipanga tena kwa ajili ya kuwapa viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu. Kwa kuwa, Serikali inaonekana sasa imebadilisha mtazamo wa kuwalipa na badala yake inataka kuwapa viwanja vya bei nafuu, naomba kufahamu, ni lini mchakato huo utakwisha ili basi, wananchi waweze kuishi kwa amani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, wananchi wamezuiwa kuendeleza majengo yao na sasa mengi yameanza kubomoka kulingana na mvua inayoendelea, wakati huo huo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege haiwezi kufanya maendelezo yoyote kwa sababu, bado kuna *interest* ya *third party* ambayo Serikali haijailipa, je, Serikali haioni kwamba kuchelewa kuwalipa wananchi hawa ni kuchelewa pia kupandishwa kwa hadhi ya uwanja ule kuwa wa Kimataifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwenye hili zoezi ambalo sasa tunakwenda kupima viwanja na kuwamilikisha hawa wananchi, haya yamekuwa ni maelekezo ambayo yanatakiwa yafanywe kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, watakaopewa viwanja hivi pamoja na wananchi wa Mwanza ni wale tu ambao wanatakiwa fidia, yaani wana haki ya kupata fidia kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, ni suala ambalo tunategemea kwamba, tutalifanyia haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ucheleweshwaji, sheria zipo. Naamini kwamba, kama kuna wananchi watakuwa wana madai zaidi kwa maana ya kucheleweshewa, ndiyo maana sheria ipo. Nadhani Serikali tumekuwa tunalipa, pale

tunapochelewa, tunawalipa riba yao. Kwa hiyo, nadhani utaratibu huo huo utatumika pia kwa Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa wananchi ambao watapata kadhia hii, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 102

**Ujenzi wa Nyumba za Polisi – Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Nyumba za Polisi kwenye Kituo cha Polisi Micheweni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatarajia kutenga fedha kiasi cha shilingi 368,770,600/= toka kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026, kwa ajili ya kujenga nyumba mbili za makazi ya kuishi familia sita za Askari Polisi katika Kituo cha Polisi Micheweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi 802,926,788/= kwa ajili ya kujenga kituo kipya cha Polisi daraja "B" cha Micheweni, kwani kituo kilichopo sasa ni kichakavu na hakiwezi kufanyiwa ukarabati. Ujenzi huo unatarajia kuanza katika mwaka wa fedha 2024/2025, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omar.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini kwa kuwa ni muda mrefu nimeuliza maswali kuhusu ujenzi wa Kituo cha Polisi pamoja na nyumba za Askari, na Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba,

ametenga shilingi 800,000,000/=, sasa je, ni *quarter* gani ya mwaka wa fedha ujenzi huu wa Kituo cha Polisi Micheweni utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kupanga ratiba yako baada ya Mkutano huu wa Bunge, kuambatana nami kwenda kutembelea Kituo hiki cha Polisi Micheweni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, fedha imetengwa kwenye mwaka wa fedha 2024. Kwa hiyo, kwenye *quarter* hii ya tatu na ya nne itatolewa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utayari wa Kwenda huko baada ya Bunge lako Tukufu; nitakaa na Mheshimiwa Mbunge, tutapanga ratiba ya kwenda kutembelea Kituo hicho cha Micheweni, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri. Tuliomba fedha za ukarabati wa Vituo vya Polisi Kwamtoro pamoja na Mrijo na tuliahidiwa mwaka huu wa fedha wangetoa hiyo fedha, lakini mpaka sasa fedha haijaenda. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa vituo viwili vya Polisi; Kwamtoro pamoja na Mrijo, Wilayani Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika mwaka wa fedha 2024/2025 tutapeleka fedha, kwa kuwa mwaka bado unaendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi

fedha itakuja kwa ajili ya ukarabati wa vituo viwili vya Polisi vya Chemba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kituo cha Polisi cha Mgeta, Serikali imetoa shilingi 53,000,000/= na sasa ghafla kimesimama, hakiendelei kujengwa. Ni lini sasa kituo hicho kitamalizika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeshatoa fedha kiasi cha shilingi 53,000,000/=, basi namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baada ya kipindi cha maswali, nitakutananaye. Tutafuatilia ni kwa nini kituo hicho kisikamilike wakati fedha imetolewa? Ahsante

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mwanyika.

Na. 103

**Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Misitu**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itachukua hatua za kuhakikisha uvunaji wa rasilimali misitu unazingatia uongezaji thamani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kuhakikisha uvunaji wa rasilimali misitu unazingatia uongezaji wa thamani ya mazao hayo, kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na soko la nje. Katika kutekeleza

mpango huo Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wadau wa mazao ya misitu kuhusu matumizi ya teknolojia ya kisasa katika uongezaji thamani katika mnyororo mzima wa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeanzisha Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu kilichopo Wilayani Mafinga, Mkoani Iringa, ambacho kinatoa mafunzo ya kuongeza thamani mazao ya misitu, hususan Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya vijana 27 wa kozi ndefu na vijana 103 wa kozi fupi wamehitimu, ambao hutumika kutoa mafunzo kwa wakulima wa miti katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Mazao ya Mbao yaliyohandisiwa Mwaka 2021 pamoja na Mpango Kazi wake kwa Mwaka (2021–2031). Mpango mkakati huu umesaidia katika kuimarisha uzalishaji na biashara ya mazao ya misitu yaliyohandisiwa, ambapo hadi sasa kuna jumla ya viwanda 48 vinavyozalisha bidhaa ya *venia* katika Mikoa ya Iringa na Njombe na kati ya viwanda hivyo, viwanda 27 vipo katika Jimbo la Njombe Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara imeandaa kanuni kupitia Tangazo la Serikali Na. 266 la Machi, 2023 linalolenga kusimamia usafirishaji wa bidhaa za mazao ya misitu yanayoingia na yanayoenda nje ya nchi. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2024 kiasi cha mita za ujazo 38,056 za bidhaa za misitu zilizongezwa thamani, zenye thamani ya Dola ya Marekani 9,079,813, zilisafirishwa kwenda nje ya nchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali na vile vile tunawashukuru kwa hizo juhudi zote ambazo wanazifanya, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, natambua sasa kwamba, vibali vinaendelea kutolewa kwa wale wazalishaji wa

*venia* katika kipindi hiki ambacho sisi tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba, thamani katika mazao ya misitu inaongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali. Serikali ipo tayari kutoa masharti kwamba, hata kama hawa wanafanya uvunaji, na nyingi ni kampuni za nje kutoka sehemu za Asia. Je, wanaweza wakawapa masharti kwamba, wavune, lakini wawe na mpango kazi wa kuhakikisha kwamba, wanajenga viwanda vya kuongeza thamani katika mazao haya ya misitu na hasa venia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Hata kwa hicho kidogo ambacho kinachukuliwa kama mazao ya misitu na yanakuwa *processed*, bei ambayo wakulima wanapewa ni ndogo sana. Tunaiomba Serikali, ni kwa nini isiweke utaratibu wa kutoa angalau bei elekezi ambayo iko *fair* kwa wakulima wetu wa mazao ya misitu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge linakumbuka kwamba, tulikuwa na zuio la kuruhusu usafirishaji wa *venia*. Serikali ilipata muda wa kuandaa utaratibu mpya ambao sasa unatumika kuwaruhusu wenye viwanda kuweza kuzalisha *venia* na kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia utaratibu mpya uliowekwa wote ambao wamepewa leseni za kuzalisha na kusafirisha *venia* nje ya nchi, wamewekewa utaratibu wa kuhakikisha ndani ya kipindi cha miaka miwili wawe wamejenga uwezo wa kuboresha viwanda vyao ili kuweza kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha hapa ndani ya nchi. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili. Muda wote tunaongozwa na nguvu ya soko, lakini tumepokea ushauri wake, tunaenda kuufanyia kazi, tutaona jinsi ambavyo tunaweza kuu-*accommodate*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa *Eng*. Ezra.

Na. 104

**Kuondoa Adha ya Uvamizi wa Tembo, Kata ya Nyakahura, Biharamulo.**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali wa kuondoa adha ya uvamizi wa tembo katika Kijiji cha Nyabugombe, Kata ya Nyakahura, Biharamulo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Nyabugombe kilichopo katika Kata ya Nyakahura ni miongoni mwa vijiji 38 vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Burigi, Chato. Kwa kipindi cha miezi sita Julai – Desemba, 2024 jumla ya matukio 16 ya tembo yaliripotiwa na kudhibitiwa katika Kijiji cha Nyabugombe kilichopo Kata ya Nyakahura, Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na adha ya wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo katika maeneo yanayopakana na Hifadhi ya Taifa ya Burigi, Chato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kushirikiana na wananchi kudhibiti tembo kwa wakati, ambapo jumla ya Askari sita wa uhifadhi kwa kushirikiana na mgambo sita waliopewa mafunzo kuhusu tabia za wanyamapori wanatumika kufukuza tembo kupitia Kituo cha Nyungwe kilichopo Kijiji cha Nyabugombe, Kata ya Nyakahura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari hao wamewezeshwa vitendea kazi mbalimbali, likiwemo gari moja, *GPS* mbili, tochi muhimu za kufukuzia tembo na mabomu baridi 50. Aidha, wananchi 425 wamepatiwa elimu kuhusu mbinu mbadala za kukabiliana na tembo kupitia mikutano ya hadhara. Vilevile katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi 19,800,000/= kwa ajili ya kuweka uzio wa pilipili katika eneo la Hifadhi ya Burigi, Chato, linalopakana na Kata ya Nyakahura.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Eng.* Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, na ninashukuru kwa ajili ya hao maaskari ambao wameletwa katika eneo la Nyabugombe, *especially* Kituo kile cha Nyungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili. Sehemu ya kwanza ni kwamba, pamoja na wale maaskari kuwepo, lakini bado matukio ya tembo kutoka na kupita yamekuwa yanaendelea kiasi kwamba, baadhi ya wananchi wameathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu. Ni lini madai ya wananchi wote wa Nyakahura ambao wameathiriwa na tembo waliotoka ndani ya hifadhi wataweza kulipwa, kwa sababu, ni muda mrefu yapo madai, lakini hayajalipwa na wananchi waliharibiwa mazao ambayo ndiyo chakula wanachokitegemea kwa sababu, hawana shughuli nyingine ya kuwaingizia Uchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kipindi kilichopita tukiongea na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, alitujulisha habari ya kuhamisha tembo zaidi ya 200, kuwatoa kwenye Hifadhi ya Kyerwa na hatimaye wawalete katika eneo letu hili la Burigi. Sasa tunafurahi kwa sababu wanadumisha utalii, lakini wale tembo wanaokuja ni wengi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tembo waliopo sasa, bado wamekuwa wanaweza kutoka nje ya hifadhi. Je, mmejiandaaje kukabiliana na ongezeko la tembo zaidi ya 200 wanaohamishwa kutoka Rumanyika kuja Biharamulo kwenye Hifadhi ya Burigi ili iweze kuondoa matatizo ambayo yanawakabili wananchi, hususan uharibifu wa mazao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, yapo madai ya wananchi ambapo tathmini ya awali iliyofanyika inaonesha kwamba, kiasi cha shilingi 1,675,000/= zinahitajika, kwa ajili ya kuwalipa, lakini vilevile tuko kwenye hatua ya kuhakikisha kwamba, madai haya ndiyo sahihi. Kwa hiyo, tumewasiliana na wenzetu wa halmashauri husika ili kuhakikisha kwamba, taarifa walizotuletea ndiyo halisi na hakuna taarifa nyingine ambazo bado hazijafika. Mara baada ya wao kukamilisha utaratibu huo wananchi hao watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hili la kukabiliana na tembo ambao tunakusudia kuwahamishia kwenye eneo hili, kama ambavyo tumesema, katika mwaka huu wa fedha tuna mkakati wa kuweka uzio wa pilipili katika eneo linalopakana na hifadhi. Tunataka kutumia mkakati huo kuona jinsi ambavyo unaweza kutumika kufukuza tembo na kama kutahitajika jitihada kubwa zaidi za kuweka uzio wa umeme, basi Serikali haitasita kufanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wananchi wa Mkoa wa Mara wanaoishi kandokando ya Mbuga ya Serengeti wamekuwa wakiathirika na uvamizi huu wa tembo. Sasa, moja ya mkakati wa Serikali, wameainisha pia, ni matumizi ya mabomu baridi ambayo unakuta wamegawiwa baadhi tu ya watu. Serikali haioni kwamba, kuna haja ya kutoa elimu ya matumizi ya haya mabomu baridi ikiwa ni sanjari na ugawaji wa mabomu haya…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, twende kwenye swali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kaya ambazo zinaathirika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** …na uvamizi wa tembo hawa, ili waweze kujilinda pale ambapo unakuta wanavamiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya mabomu baridi ni moja tu ya njia ambazo tunazitumia katika kukabiliana na madhara ya tembo. Kwenye maeneo ambayo tunaweza kutumia teknolojia ya *drone* au tunaweza kutumia helikopta, tunatumia njia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo ambayo tunatumia mabomu, elimu inatolewa kwa wananchi, lakini nguvu kubwa zaidi inaelekezwa kwa wale wanaoyatumia mabomu haya kwa sababu, bila kutoa elimu hiyo tunaweza kupata madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo wananchi waliamua wenyewe kutumia mabomu bila ya kupata mafunzo, yakaleta madhara. Kwa hiyo, sasa hivi tumezuia kabisa wananchi ambao hawajapewa mafunzo kuweza kutumia mabomu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa halmashauri zetu ambazo zimekuwa na mpango wa kununua mabomu, kuongeza nguvu kwa yale yanayoletwa na Serikali, wazingatie utaratibu uliowekwa wa kuhakikisha wanaoyatumia wawe ni wale tu ambao wamepatiwa mafunzo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba kutumia fursa hii kulieleza Bunge letu Tukufu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la changamoto ya tembo katika baadhi ya maeneo ambayo yanapakana na hifadhi, linapaswa kuwa ni ajenda ya halmashauri husika. Katika vikao vya halmashauri, tuna Kamati ya Madiwani inayoshughulika na masuala ya mazingira. Mfano, baadhi ya maeneo kuna changamoto ya mamba kuumiza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri husika inapaswa kutenga eneo la kuweka bomba ili wananchi wasichote maji katika eneo ambako kuna mamba. Vilevile, kuna maeneo kuna changamoto ya tembo, halmashauri husika inapaswa kuchukua majukumu yote kulinda wananchi wakishirikiana na sisi Wizara na mashirika yetu ya *TAWA* na *TANAPA*. Katika bajeti za halmashauri, asilimia 10 za halmashauri, mapato ya ndani na kuna maeneo tunarudisha fedha za *Wildlife Management Area,* 25% inarudi katika halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinatakiwa zitumike kwa shughuli rafiki, uhifadhi, pamoja na kulinda wananchi wasiumizwe. Hivyo, ajenda ya kulinda wananchi dhidi ya changamoto mbalimbali, ikiwa ni pamoja ya wanyama, ni ajenda ya halmashauri husika na *full council*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshawasiliana na Mheshimiwa Waziri mwenzangu kwamba, wakati umefika tuelekeze Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wafanye kazi nzuri. Ma-*DC* na Waheshimiwa Madiwani lazima walijadili hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna halmashauri za kutosha, walijadili, tunalindaje wananchi katika *jurisdiction*, mamlaka, ya eneo husika? Halmashauri zinaweza kununua *drone*, halmashauri inaweza kupeleka vijana *VGS* kusomea namna ya kulinda, tunaita

*Village Game Scout*. Tuna vyuo vyetu vya Likuyu na Sekamaganga, ni lazima tuje na *reforms*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nitoe shukrani sana kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, sasa tutashirikiana na Kamati za Madiwani kuhakikisha tunalinda wananchi wetu kwa fedha za Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu sahihi. Tuendelee na Wizara ya Habari na Utamaduni, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Na. 105

**Kuinua Lugha ya Kiswahili**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua lugha ya Kiswahili kupitia vyombo vyake vya habari vya kitaifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuinua na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili kupitia vyombo vya habari vya kitaifa kama vile redio, televisheni, makala za magazeti na mitandao ya kijamii. Serikali imeweka msisitizo kwa vyombo vya

habari vya kitaifa, kuandaa na kurusha vipindi vinavyoelimisha, kuburudisha na kuhamasisha matumizi ya Kiswahili fasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipindi hivi vinahusisha mijadala ya kitaaluma, tamthilia, mashairi, na makala zinazochambua masuala ya lugha na utamaduni. Kwa sasa idadi ya vipindi imeongezeka hadi kufikia 35 kwa wiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, majibu sawia, majibu mwanana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti nyingi zinazohusu masuala ya kawaida ya Watanzania zinafanyika kwa lugha ya kigeni hasa Kiingereza. Je, Serikali mpaka sasa haioni umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili kwa kuelekeza kupata tafsiri katika lugha hii adhimu katika utafiti wa kisayansi na maendeleo ya kiteknolojia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Je, Serikali kupitia mamlaka husika za ustawishaji wa lugha ya Kiswahili imeweza kujifunza nini kutoka mataifa mengine ulimwenguni ambayo yamefanikiwa kutumia lugha zao rasmi za kitaifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Asha Abdullah Juma maarufu kama Bi. Mshua kwa uzalendo na mapenzi ya dhati. Maana haya siyo mapenzi tu, ni mahaba ya dhati kwa lugha ya Kiswahili. Sisi wapenzi wenzako wa Kiswahili akiwemo ndugu yangu Ahmed Ally na Mkandaji Kibu Dennis tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujibu maswali yake, hoja aliyoleta Bi Mshua ni ya msingi sana na kasi ya mabadiliko ya kidunia inapaswa kuwafikia Watanzania kwa lugha waliyoizoea

ambayo ni lugha ya Kiswahili. Kwa kufahamu hilo, Baraza la Kiswahili la Taifa na Baraza la Kiswahili la Zanzibar wameandaa na kusanifu msamiati wa utafiti kwenye sayansi na teknolojia kwa lugha ya Kiswahili na machapisho kadhaa yameshatengenezwa kwa lugha hiyo, yakiwemo machapisho ya Kamusi ya awali ya sayansi na teknolojia. Halikadhalika, kuna Kamusi ya Fizikia, Kemia, Biolojia, Kamusi ya Kompyuta na machapisho mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, fauka na hayo, machapisho mengine katika nyanja husika yametengenezwa kwa Kiswahili na sasa hivi jitihada ya Serikali inayoifanya ni kuhakikisha tunawashawishi watafiti kufanya tafiti zinazofuata kwa lugha ya Kiswahili na kutafsiri tafiti ambazo walishazifanya kwa lugha nyingine kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu tulichojifunza ni muhimu kuwa na vyombo imara na mahsusi kwa ajili ya kusimamia lugha. Hivyo, Serikali imeongeza uwekezaji kwenye Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar ili kuviimarisha vyombo hivi na kuhakikisha lugha ya Kiswahili inasimamiwa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji unaofanywa, yamefanya mambo mengi yakiwemo makongamano nje ya nchi kujaribu kukieneza Kiswahili na kukipa hadhi inayostahili. Pia, tumejifunza kuhusu umuhimu wa kusambaza lugha kwa kutumia mifumo ya kidigitali, kwa vile dunia sasa imebadilika na mifumo ya kidigitali ndiyo hasa inayotumika kueneza mambo mbalimbali ambayo yanatakiwa kwenda kwa kasi duniani, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Kembaki.

Na. 106

**Kubadili Majina ya Kampuni Mara kwa Mara**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Wawekezaji wa nje ambao kila baada ya miaka kadhaa hubadili majina ya Kampuni kwa lengo la kukwepa kodi?

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto ya ukwepaji wa kodi unaosababishwa na mabadiliko ya majina ya kampuni za kigeni, Serikali imechukua hatua madhubuti kudhibiti mianya hiyo ya ukwepaji wa kodi. Hatua hizi ni pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Kampuni, Sura 212, ambayo inawataka wawekezaji kutoa taarifa kwa Msajili wa Kampuni *(BRELA)* wanapobadilisha jina la kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya mabadiliko yote ya majina huhifadhiwa kwenye kumbukumbu rasmi ili kuhakikisha kuwa majina mapya hayawezi kutumika kuficha madeni ya kodi au kushiriki katika shughuli zisizo halali. Aidha, kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438, Serikali imeweka sharti kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* itahakikisha Namba ya Utambulisho wa Kodi *(TIN)* inabaki ile ile hata kama kampuni itabadilisha jina. *TIN* hutumika kufuatilia historia yote ya ulipaji kodi wa kampuni, hivyo mabadiliko ya jina hayaondoi wala kufuta wajibu wa kodi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu mazuri ninalo swali la nyongeza. Kwa kuwa, mchakato wa kubadilisha

majina ya kampuni kwa Watanzania, ni mchakato mkubwa sana, unaambiwa uwe na vyeti mbalimbali mfano *RITA* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kampuni za kigeni zikitoka kwenye eneo hili kwenda hili pasipo kujua Watanzania sababu gani inayowafanya watoke kwenye kampuni hii na kwenda hii, hali ambayo inawaletea Watanzania sintofahamu kubwa ya ukwepaji wa kodi. Je, Serikali inatoa tamko gani sasa la kuhakikisha hao wanaohama kwenye kampuni hii kwenda nyingine kutoa elimu ya kutosha kwa Watanzania ili wajiridhishe kwamba, wanahama kisheria na wala hawakwepi kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa kunakuwa na kampuni ambayo labda ina wadeni Watanzania, lakini kampuni ile imebadilisha jina ghafla. Je, Watanzania hawaathiriki na mabadiliko hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mariam kwa maswali mawili mazuri aliyoyatoa. Tuna mambo kama matatu kwenye hili jambo la kubadili majina. Moja, kubadili jina kama jina la kampuni haiathiri na wala haihusiani na masuala ya kikodi. Kinachozingatiwa sana, punde panapokuwepo na mabadiliko ambacho kinaweza kusababisha pawepo na kodi ama ukwepaji wa kodi, ni mabadiliko ya umiliki ambayo yanasababisha kama aliyekuwa anamiliki ameuza *share,* iwe *share* moja, mbili au tatu na akapata kipato cha ziada kutokana na zaidi ya uwekezaji aliokuwa amepata, hapo pana *attract capital gain tax,* inatakiwa alipie kodi ya faida ambayo ameipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mmiliki ni yule yule ameamua kubadilisha jina la kampuni, labda kwa ajili ya matangazo ya kibiashara na *TIN Number* ya mlipaji wa kodi bado ni ile ile, hili halileti badiliko lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukabadili majina mara nyingi kama Musa Sima anavyobadili majina ya Timu ya Singida, hii haileti ongezeko la kodi kwenye kampuni. Kama Festo Sanga anamiliki Dodoma Hotel leo akaiita *The Capital Hotel* na mmiliki ni yeye mwenyewe, hii haileti jambo lolote la kodi, lakini kama Mheshimiwa Sanga alikuwa anamiliki *hotel* labda *share* kadhaa akiziuza kwa mtu mwingine, ile faida ya kuuza ndiyo ambayo tunaitaja kama *capital gain tax* ambayo anatakiwa alipie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna makampuni ya nje ambayo yanamiliki sehemu ya kampuni huku Tanzania na yanafanya shughuli, ukiyafatilia kule nje unakuta hayana shughuli zaidi ya kampuni inayofanya kazi hapa Tanzania. Ikitokea kule wamebadilishana umiliki unaozidi 50% hapo ndiyo na penyewe tunasema pana kodi lazima ikusanywe.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo Serikali imeshayafanyia kazi sana yalikuwepo zamani kwenye masuala ya mawasiliano, kwenye masuala ya madini, lakini sasa hivi yameshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba yanapotokea mabadiliko ya aina hiyo, Serikali imeshaweka kwenye sheria na inafuatilia kwa ukaribu sana na mara zote yanapotokea mabadiliko ya aina hiyo Serikali imekuwa ikipata kodi inayostahili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo hewa nzito sana isije ikawa watu wameingia na ………*(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Hongera kwa majibu sahihi. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ally Mlaghila.

Na. 107

**Ujenzi wa Chuo cha Veta Wilaya ya Kyela**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo Cha *VETA* Wilaya ya Kyela?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi nchini ili kuwawezesha wananchi kupata ujuzi na mafunzo yatakayowawezesha wananchi kutekeleza kwa ufanisi shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kuzingatia fursa mbalimbali ambazo zipo kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ipo katika hatua za mwisho za makabidhiano ya Chuo cha Kyela *Polytechnical College* kilichokuwa kinamilikiwa na Kampuni ya *KPC Limited.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kufanya maandalizi ya awali ikiwa ni pamoja na kupeleka wanafunzi na vifaa kwa ajili ya mafunzo ili kuhakikisha kuwa chuo hiki kinaanza kutoa mafunzo mapema kikiwa chini ya Mamlaka ya *VETA* na kuwezesha Wilaya ya Kyela kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi kama Wilaya nyingine zote nchini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha *KPC,* tayari makabidhiano ya kisheria yalifanyika miaka minne iliyopita na sherehe za makabidhiano pia zilifanyika tarehe 03 Agosti, 2022 mbele ya Waziri Mkuu na iliamuliwa chuo kianze, mpaka sasa ni muda mrefu sana umepita.

Je, sababu za kusuasua ni malipo ya waliokuwa wafanyakazi wa *KPC* au kuna sababu nyingine?

Swali la pili, nini mpango wa Serikali katika kuendeleza vipaji vya ufundi kwa vijana Wilayani Kyela ili waweze kujitegemea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Mlaghila Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli makabidhiano yamefanyika chini ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania miaka mitatu iliyopita, lakini zilikuwa ni sherehe za makabidhiano. Baada ya sherehe zile, ilikuwa ni lazima tufuate taratibu za makabidhiano rasmi ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mali zilizopo pamoja na vifaa, vilevile tathmni ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali tayari imeshatekeleza wajibu wake kwa kufanya tathmini ya mali zile zilizopo na tayari hivi sasa ninapozungumza ardhi ile inasomeka kwa jina la *VETA*. Taratibu zinazofuata ni kwa ajili ya majengo pamoja na vifaa, hizo zinaendelea kufanyika chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mbeya pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lililosababisha kusuasua kwa makabidhiano haya ni kutokana na madai au mapendekezo ya mmiliki wa awali, alihitaji yale madeni ya watumishi waliokuwa wa *KPC Ltd* yaweze kulipwa na Serikali. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunafanya tathmini ya kina ili kuweza kugundua au kubaini uhalali wa madai hayo na mara mchakato huo utakapokamilika, makabidhiano rasmi sasa yatafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili la suala la vipaji na ujuzi kwa vijana wetu, Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu wote mnafahamu kwamba, tumefanya mapitio ya sera pamoja na mitaala yetu na siku ya tarehe 01 Februari, 2025 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua

zile sera pamoja na mitaala ile mipya kwa lengo la kukuza ujuzi pamoja na vipaji vya vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumekuwa tukijenga *VETA* katika kila Wilaya pamoja na shule za ufundi katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba vipaji na ujuzi kwa vijana wetu unaweza kukuzwa kupitia utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha, sasa ni kipindi cha wageni. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kutoka Mkoani Geita ambao ni Ndugu Martine Rueben Shigella, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Ndugu Nicolaus Kasendamila, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Geita, Ndugu Alexandrina Katabi, Katibu wa CCM Mkoa wa Geita, Ndugu Evarist Paschal Mjumbe wa *NEC* Mkoa wa Geita, Ndugu Chacha Mwita, Mjumbe wa *NEC* Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine 31 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, amba oni Wadau wa Maendeleo kutoka Mkoani Geita. Karibuni sana na hatutegemei kama mtamwacha Kiongozi wetu, maana Wajumbe ninyi hamtabiriki. Kwa hiyo, tunaomba sana mumchague tena. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum abao ni Viongozi wa Wizara hiyo. Dkt. John Jingu - Katibu Mkuu, Wakili Amon Mpanju - Naibu Katibu Mkuu, Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa taarifa ya kipekee, kwa mujibu wa mitandao ya Kimataifa, Simba ndiyo Klabu pekee iliyopo katika michuano, inayosimamiwa… *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walipaza Sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Tarimba mbona umekasirika? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Simba ndiyo Klabu pekee iliyopo katika michuano inayosimamiwa na *CAF* kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na ndiyo Klabu pekee ya Tanzania inayoshiriki robo fainali kwa misimu sita mfululizo, kwa michuano inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira Barani Afrika *(CAF)*.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Simba, tunayo Klabu ya Yanga ambayo nayo ni timu muhimu sana kwa Taifa letu kwa umoja wa Taifa letu. Namna Klabu ya Simba na Yanga zinavyoitangaza nchi yetu, inampa sifa kubwa sana Rais wetu. Tanzania inakuwa kwenye ramani ya Afrika na dunia kwa vilabu hivi viwili muhimu kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, tunawapongeza Klabu ya Simba na Yanga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ambao ni Wachezaji, Menejimenti na Viongozi wa benchi la ufundi wa timu ya mpira wa miguu ya Simba kutoka Jijini Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, nimeambiwa Mwenyekiti amechelewa ndege, sasa namtambulisha kwenu Ndugu Zubeda Sakuru, Mtendaji Mkuu, huyu alishakuwa Mbunge, *CPA*; Issa Masoud, Mjumbe wa Bodi; Ndugu Seleman Haroub, Mjumbe wa Bodi; Ndugu Fadluraghma Davids, Kocha Mkuu; Ndugu Ahmed Ally, Meneja Habari na Mawasiliano; Wachezaji wa Simba wakiongozwa na *Captain* Mohamed na Viongozi wengine walioambatana na Klabu hii ya Simba. Ahsanteni *(Makofi/Vigelegele)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais,

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambaye ni Diwani Kata ya Kitongoni Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi, huyu ni mtoto wake kutoka Mkoani Kusini Pemba. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ng’wasi Damas Kamani, ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Benaya Kapinga, ambaye ni Katibu wa Mbunge na Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum kutoka Mbinga. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Jesca, hawa ni Viongozi wa Kamati ya Kuhifadhi *Quran* Nyanda ya Juu Kusini kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Omari Kigua, amba oni Wanafunzi wa Chuo cha Elimu Biashara, kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni tisa wa Mheshimiwa George Mwenisongole, haw ani Wafanyakazi wa Mgahawa Laliga kutoka Kisasa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 128 wa Mheshimiwa Francis Mtinga, ambao ni Makatibu wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Mkalama Mkoani Singida. Karibuni sana, na Mbunge wenu hapa anawawakilisha vizuri sana ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni Wanafunzi 25 na Walimu wanne kutoka Shule ya Msingi *Dar es Salaam Independent School (DIS)* ya Jijini Dar es Salaam. Hongereni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye shule hii tunaye Mtoto wa Mheshimiwa Ndejembi, Waziri wa Ardhi. Mtoto wa Mheshimiwa

Ndejembi hebu simama peke yako tukuone, hongera sana. *(Makofi)*

Katibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo wa Spika…

**NAIBU SPIKA:** Nani anataka Mwongozo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa.

**NAIBU SPIKA:** Ehee!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata mwongozo wako kwa Kanuni ya 76. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili wakati akijibu swali lake Na.104, ameeleza kwamba ni wajibu wa halmashauri zinazopakana na misitu, lakini pia ni wajibu wa halmashauri zinazoishi karibu na ziwa na bahari kutenga bajeti kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya ulinzi wa tembo na mamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja wa watu tunaoishi kwenye ziwa. Amesema tunatakiwa kutenga uwekaji wa mabomba kutoa kwenye ziwa ili wananchi wasogee ziwani kukwepa mamba.

Mheshimiwa Naibuy Spika, nataka kutoa mfano mmoja wa Geita. Geita tulivamiwa na tumbili na nyani katikati ya mji, na kuna kikosi kikubwa tu cha Jeshi la Polisi na Majeshi mengine, lakini hatukuweza kuwakabili mpaka ikalazimika kuwaita *TAWA* na *TAWIRI* ndiyo wakawakamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa maelezo ya Waziri, sisi tunaokaa karibu na ziwa, wananchi wangu wananitumia *message* hapa, ni kana kwamba anatoa kibali kwamba

wananchi wetu wakabiliane na wale Wanyama; na sisi kwa uzoefu wetu ni kuua. Wao wanataka kukamata kuwarudisha pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kupata mwongozo, ametoa wapi majibu haya ikiwa humu ndani sisi tunampitishia bajeti ya ulinzi wa maliasili zetu Tanzania? Nilitaka kupata mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, mwongozo wangu kwako, changamoto za wanyama nchini mwetu ni kubwa sana, na haziko nchini mwetu peke yetu, ziko karibuni maeneo mengi katika Bara letu la Afrika. Changamoto hizi ni kubwa na zinahitaji *engagement* vizuri.

Sasa mwongozo wangu kwako, kaa na Waziri mpange shughuli hii vizuri akuelimishe vizuri na wewe umweleze yale unayoyaona yanafaa ili kwa pamoja *we walk together,* ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tusikilizane. Sasa namwita Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Naomba hii Taarifa ya Kamati yote iingie kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imaini ya Kamati kuwa hatua hii italiwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza jukumu la kusimamia Serikali kwa niaba ya wananchi na hivyo kuweza kuishauri vyema juu ya hatua stahiki za kuchukua kwa maslahi ya Taifa na kwa kuzingatia ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya shughuli. Eneo hili linaelezea kwa kina shughuli ambazo Kamati imefanikiwa kuzitekeleza kwa kipindi cha mwaka 2024 kwa mujibu wa Kanuni. Katika kipindi hicho shughuli kuu zilizotekelezwa na Kamati ni kama ifuatavyo: -

(a) Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maazimio;

(b) Ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(c) Uchambuzi wa Miswada mbalimbali ya sheria;

(d) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Waziri Mkuu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunaomba utulivu ndani ya ukumbi. Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika,

(e) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pia;

(f) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, JInsia, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Desemba, 2024);

(g) Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Taasisi zinazosimamia; na

(h) Gharama za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya nyongeza ya 7(1)(d) Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Taarifa ya kina ya namna ya Kamati inavyochambua taarifa hizo ipo katika taarifa yetu iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa upekee naomba kuwasilisha taarifa ya suala la wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya michango wanayodaiwa na waajiri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4 Juni, 2024 kwenye Kikao cha Arobaini cha Mkutano wa Kumi na Tano ulielekeza kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ishughulikie suala la Wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya michango wanayodaiwa waajiri wao ili waweze kulipwa mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo hayo yalitolewa kufuatia mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Esther Nicholus Matiko, Mbunge, kuhusu jambo lililotokea wakati wa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge. Swali hilo lilihusu wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya waajiri wao ya michango kwenye mifuko ya hifadhi za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu maelekezo yako, "Jambo hili Waheshimiwa Wabunge si rahisi kulitolea mwongozo kwa sababu siko na takwimu hapa, lakini nitalipeleka hili jambo kwa Kamati yetu ambayo ofisi hii inaripoti kwake ili waweze kulifuatilia kwa ukamilifu kwa maana ya Serikali kule ipate nafasi ya kupeleka taarifa. Pia kama iko sababu waitwe Wakurugenzi hawa na mifuko hii yote hapa nchini ili iwaelekeze kule kwenye Kamati ni mazingira gani? Hapo siyo wa Serikali pekee, pengine na wa binafsi kwa sababu mifuko yote iko chini ya Ofisi hii. Basi waende kule wakaeleze ni mazingira gani wanamdai mwajiriwa fedha." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maelekezo yako, Kamati ilialika wadau mbalimbali kuja mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu suala hili ikiwemo vyama vinavyounda *TUCTA* pamoja na Umoja wa Wastaafu *(REAT)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mahojiano ya wadau mbalimbali wakiwemo *TUCTA* na *REAT* walithibisha kwamba kwa nyakati tofauti wamepokea malalamiko ya wastaafu kutakiwa kulipa madeni ya michango ambayo ilipaswa kulipwa na mwajiri ili waweze kulipwa mafao yao. Ushahidi wa maelezo hayo na nyaraka za uthibitisho zilizowasilishwa kipo katika kielelezo namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali ulieleza kuwa sheria na miongozo ya mifuko hairuhusu mwanachama kulipa michango ya mwajiri ili alipwe mafao. Hata hivyo, iliongezwa kuwa mazingira yanaweza kutokea na kusababisha wastaafu kulipa michango hiyo endapo wastaafu watatumiwa namba za malipo zilizotolewa mfuko kwenda kwa mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mahojiano na nyaraka zilizowasilishwa, Kamati ilibaini kwamba baadhi ya wastaafu walilazimika kupewa nyaraka zenye namba ya malipo kwa ajili ya kulipa madeni ya mwajiri ili waweze kulipwa mafao yao. Kamati ilitaka kujua ni namna gani mazingira mstaafu anapata nyaraka zenye namba ya malipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilieleza kuwa mfuko hutoa namba hiyo kwa mwajiri na mwajiri ndiye humpatia mstaafu hiyo namba ili alipe. Hata hivyo, Serikali ilishindwa kuwasilisha ushahidi wa namba ya malipo waliyotoa kwa mwajiri na ikaja kulipwa na mstaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu hawa wanaolazimika kulipa huwa hawana kingine wanachokitegemea zaidi ya mafao yao. Suala hili siyo sawa hata kidogo, hasa ikizingatiwa kuwa sheria haizuii mstafu kulipwa mafao yake hata kama mwajariwa hajakamilisha michango yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, kwa msingi huu, ni wazi *PSSSF* inawawajibisha wastaafu kwa makosa yake ya kushindwa kusimamia sheria kwa kuhakikisha mwajiri anawasilisha michango yake kwa wakati. Aidha, kupitia nyaraka za mahojiano yaliyofanywa na wadau, Kamati ilibaini kuwa suala hili limekuwa likifanywa na *PSSSF* na hakuna ushahidi wa vielelezo uliopata dhidi ya *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye mapendekezo.

KWA KUWA, kitendo cha *PSSSF*, kutengeneza mazingira ya kuwafanya baadhi ya Wastaafu kulipa michango ya Mwajiri ili waweze kulipwa mafao yao;

(i) Ni kinyume cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Sura ya 371 na kinaondoa imani ya mwajiriwa na mfuko huo;

(ii) Haipaswi kuvumiliwa na Bunge ambalo ndiyo lenye mamlaka ya utungaji wa Sheria;

(iii) Kinakinzana na lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huo kwa kuhakikisha ustawi wa Wanachama;

NA KWA KUWA, kutokurekebishwa kwa hali hiyo ni jambo linaloongeza kero miongoni mwa wananchi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe kuwa:-

(i) *PSSSF* inawarejeshea fedha za michango zilizolipwa na wastaafu na kuzidai fedha hizo kwa waajiri kama sheria ilivyoelekezwa;

(ii) Mifuko iache mara moja utaratibu wa kutoa namba za malipo kwa baadhi ya wastaafu ili walipe michango ambayo haijawasilishwa na mwajiri wakati wakifuatilia mafao yao; na

(iii) Mfuko ichukue hatua kali za kisheria kwa waajiri wasiyowasilisha michango kwa mujibu wa sheria.

KWA KUWA, utekelezaji wa Sera ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi imebainika kuwa na dosari ya kutoendana na miongozo na kanuni za Shirika za Kazi Duniani *(ILO);*

NA KWA KUWA, dosari hiyo inaathiri usalama wa mahali pa kazi na sifa ya nchi katika Jumuiya ya Kimataifa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye marejeo ya Sera hiyo ili kuendana na Kanuni na Miongozi ya Shirika ya *ILO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa miundombinu na vitendea kazi kwa Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi *(OSHA)*.

KWA KUWA, uhaba wa miundombinu hususan katika Ofisi za mikoa na wilaya zimekuwa ni changamoto za muda mrefu;

NA KWA KUWA, uhaba huo umesababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuathiri jukumu lao la kuwalinda wafanyakazi dhidi ya magonjwa na ajali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaanzimia kwamba: -

(i) Serikali itenge bajeti itakayokidhi mahitaji ya *OSHA* ili kuongeza ofisi katika mikoa na wilaya na vitendea kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kusogeza huduma karibu na wanachama pia; na

(ii) Serikali isimamie wakala kuongeza kasi ya kusajili maeneo ya kazi nchini na kutoa miongozo ya namna ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya magonjwa na ajali kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufanisi wa Utendaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)*.

KWA KUWA, kumekuwepo na kasi ndogo ya uandikishaji wa Wanachama waliopo katika sekta isiyo rasmi; pia ipo changamoto ya uelewa juu ya masuala mbalimbali yanayohusu fidia kwa wafanyakazi na taratibu za ulipaji wa fidia jambo linalosababisha wanachama wengi kukosa haki;

NA KWA KUWA, kutokuwepo na ofisi za mfuko katika mikoa na wilaya zote nchini kunaathiri ufikiwaji wa wanachama katika

maeneo yao, hivyo kuathiri makusanyo na ulipaji wa fidia stahiki kwa wakati;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe Mfuko:-

(i) Unaandaa mkakati wa kuwaandikisha wanachama waliopo katika sekta isiyo rasmi hasa wale wanaojishughulisha na shughuli hatarishi kama fundi ujenzi na watu wa migodini ili kuweza kuongeza idadi ya wanachama na kuwasaidia pindi wanapopata ajali kazini;

(ii) Unaandaa mkakati endelevu unaotekelezeka wa kutoa elimu kwa waajiri na waajiriwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwenye ofisi mbalimbali za wanachama juu ya masuala mahususi yanayohusu fidia kwa wafanyakazi na taratibu za ulipaji wa fidia.

(iii) Unaweka mkakati wa ujenzi wa ofisi kwenye mikoa na wilaya zote nchini ili kusogeza huduma jirani na wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ufinyu wa Bajeti katika Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini.

KWA KUWA, mwenendo wa mgao wa fedha za utekelezaji wa programu hii umekuwa ukishuka kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano kinyume na makubaliano ya matumizi ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi (*Skills and Development Levy-SDL)*;

NA KWA KUWA, kushuka kwa mgao wa fedha kumesababisha kushuka kwa idadi ya vijana wanaonufaika na programu kutoka wastani wa vijana 42,000 hadi kufikia 12,000 kwa mwaka, kinyume na Mpango wa Taifa wa Maendeleo unaotaka jumla ya vijana 681,000 kupatiwa mafunzo kwa kipindi cha miaka mitano, sawa na vijana 136,000;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali itenge na kutoa fedha za programu hii kwa kufuata makubaliano ya kutoa 1/3 ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi *(SDL)* kwa ajili ya kugharamia ukuzaji ujuzi kwa nguvu kazi iliyopo katika soko la ajira. Kufanya hivyo kutawezesha vijana wengi kupata ujuzi na kujiajiri;

(b) Serikali iharakishe zoezi la kufanya tathmini itakayosaidia kuona umuhimu wa kuunganisha Programu na Mifuko yote ya Uwezeshaji Wananchi na kuiunganisha kwa lengo la kuwa na mifuko michache ambayo itawawezesha vijana kupata ujuzi na kuwezeshwa mitaji ili kuwa na tija endelevu kwa wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Ajira za Ndani na Nje ya Nchi:

KWA KUWA, Nchi yetu haina Mamlaka ya Kusimamia Ajira za Ndani na Nje ya Nchi na jukumu hili linatekelezwa na Kitengo cha Huduma za Ajira chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa Mamlaka hiyo kunaathiri kwa kiasi kikubwa kasi ya uunganishwaji wa ajira za Watanzania nje ya nchi ukilinganisha na mataifa mengine, jambo linalopelekea kukosekana kwa mapato ya nchi na kipato cha Watanzania kwa ujumla;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ianze mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Ajira Nchini, ili kuwepo na chombo kinachosimamia ajira Nchini na hivyo kuwawezesha Watanzania wengi kupata fursa za ajira hasa ajira za ujuzi wa juu Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Dosari za Utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366:

KWA KUWA, utekelezaji wa sheria hii unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo Sheria kutompa mamlaka Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, kutokuwepo kwa kanuni mahususi za Vyama vya Wafanyakazi, mapungufu katika Katiba za Vyama vya Wafanyakazii;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinapekelea Ofisi ya Uratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Mashirikisho kushindwa kuratibu kwa ufanisi shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na mashirikisho na hivyo kuibuka na migogoro ya mara kwa mara katika Vyama hivyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye Marekebisho ya Sheria hii ili kuimarisha utekelezaji wake na kuipa nguvu ya Kiutendaji Ofisi ya Mratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Mashirikisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Nitazungumzia kuhusu ufanisi katika uratibu wa Mashirika yasisyo ya Kiserikali *(NGO's)*

KWA KUWA, upungufu wa rasilimali fedha na rasilimali watu hasa Wasajili Wasaidizi kunaathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali nchini;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa rasilimali fedha na rasilimali watu kumepelekea kushindwa kufuatilia kwa kina mashirika takribani 9,773 yaliyoenea maeneo mbalimbali Tanzania Bara na hivyo baadhi ya mashirika kujihusisha na shughuli ambazo ni kinyume na malengo ya usajili;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iongeze bajeti ya Wizara ili iweze kufuatilia na kuhakikisha kuwa mashirika yanafanya kazi kwa manufaa ya jamii na maslahi ya Taifa;

(ii) Serikali ichukue hatua za haraka na madhubuti ikiwa ni pamoja na kuyafuta Mashirika ambayo yanajihusisha na masuala ya mmomonyoko wa maadili kinyume na tamaduni za nchi, yanayojihusisha na utakatishaji fedha pamoja na mashirika yanayojihusisha na siasa wakati wa uchaguzi; na

(iii) Serikali ione umuhimu wa kuajiri Wasajili Wasaidizi watakaokuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum ili waweze kutekeleza jukumu la ufuatiliaji wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutolipwa kwa mikopo katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)*:

KWA KUWA, kumekuwa na mikopo ya muda mrefu iliyokopeshwa kwa Halmashauri, Wanawake na Vikundi mbalimbali nchini na haijarejeshwa.

NA KWA KUWA, kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunaathiri utolewaji wa mikopo kwa wanawake wengine wenye vigezo vya kupata mikopo hiyo na hivyo kuathiri nia njema ya Serikali ya kuwainua wanawake kiuchumi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iweke mkakati unaotekelezeka wa kuhakikisha fedha zillizokopeshwa zinarejeshwa na kutumika kama ilivyokusudiwa;

(ii) Serikali ibuni na kubainisha vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mtaji wa Mfuko na kuweza kuwanufaisha wanawake wengi zaidi; na

(iii) Serikali iweke mkakati wa kutoa elimu juu ya uwepo wa mfuko ili wanawake wengi wanufaike na mikopo inayotolewa na mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufanisi mdogo katika kuratibu shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo:

KWA KUWA, ipo changamoto ya uelewa mdogo miongoni mwa Wafanyabiashara Ndogondogo juu ya fursa za uwezeshaji zinazotolewa na Serikali kwa Wafanyabiashara hao ikiwemo Mikopo yenye masharti nafuu.

NA KWA KUWA, kukosekana kwa elimu hiyo kunaathiri kwa kiasi kikubwa mwamko wa wafanyabiashara hao kuchangamkia fursa hiyo na uandikishaji wa Vitambulisho vya Kidijiti, jambo linalorudisha nyuma azma ya Serikali ya kuwakwamua wafanyabiasha hao kiuchumi.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iandae mkakati endelevu wa utoaji wa elimu juu ya fursa hiyo ya mikopo ili Wafanyabiashara Ndogondogo kupata mikopo yenye masharti nafuu na kuweza kujikwamua kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha kwenye majukwaa au vyama, na mashirikisho ya Wafanyabiashara Ndogondogo; na

(ii) Serikali iongeze kasi ya utoaji wa vitambulisho vya kidijiti kwa wafanyabiashara ndogondogo, ili waweze kutambuliwa na kupata mikopo kutoka Taasisi mbalimbali za kifedha nchini na Mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto ya upungufu wa bajeti inayotengwa katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:

KWA KUWA, bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuwa ndogo licha ya kwamba Wizara hii ni Mtambuka na hivyo kuwa na majukumu mengi ya kiutendaji;

NA KWA KUWA, changamoto hiyo inaathiri ufanisi wa utendaji wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake na kutoa huduma stahiki;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze bajeti kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kutoa fedha hizo kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii. Ninaomba majina yote yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis kwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara hizi pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Bi. Marry Maganga, Katibu Mkuu na Bi. Zuhura Yunus, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu. Dkt.

John Jingu na Naibu Makatibu Wakuu, Ndugu Amon Anastaz Mpanju na Bi. Felister Peter Mdemu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Idelphonce Leonard, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja; baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, pia maoni na mapendekezo ya Kamati; sasa, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2024. Taarifa hii imejikita katika kuelezea shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha mwaka mmoja.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii imeundwa na sehemu kuu nne kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

(ii) Sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

(iii) Sehemu ya tatu inatoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi, na

(iv) Sehemu ya nne inatoa hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

### 1.3 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati unatokana na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inaeleza kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi wake. Aidha Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawasilisha Taarifa ya majukumu ambayo yametekelezwa kwa kipindi cha Mwaka 2024. Lengo ni kuonesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyo chini Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na kubainisha maeneo yenye mafanikio na yale yenye changamoto. Taarifa hii itakuwa ni nyenzo muhimu ya kuliwezesha Bunge lako tukufu kwa niaba ya

wananchi ambao ndiyo wamelipa Bunge jukumu hilo la kusimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania ili kuweza kushauri serikali hatua za kuchukua kwa maslahi ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 6(5) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ina wajibu wa kufanya masuala mbalimbali yaliyoanishwa katika Kifungu cha 7 (1) (a-d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo ni: -

(a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na

(d) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka 2024 Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Wizara hizo pamoja na taasisi zake.

(ii) Kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara inazozisimamia;

(iii) Uchambuzi wa Miswada mbalimbali ya Sheria.

(iv) Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025 za Wizara inazozisimamia.

(v) Kujadili taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba,2024); na

(vi) Kufuatilia Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Mwezi Februari, 2024.

### 1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 142(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Vikao vya kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kujua utendaji wao, mafanikio, changamoto na namna ya kutatua changamoto hizo;

(ii) Ziara za ukaguzi wa maeneo mbalimbali kwa lengo la kujionea utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake na kuzilinganisha na taarifa iliyochambuliwa na Kamati;

(iii) Kufanya uchambuzi wa taarifa za Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Maelezo ya Shughuli

**Mheshimiwa Spika**, eneo hili linaeleza kwa kina shughuli ambazo Kamati imefanikiwa kuzitekeleza kwa kipindi cha Mwaka 2024 kwa mujibu wa Kanuni. Katika kipindi hicho, shughuli Kuu zilizotekelezwa na Kamati ni kama ifuatavyo: -

(a) Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maazimio

(b) Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(c) Uchambuzi wa Miswada mbalimbali ya Sheria.

(d) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(e) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu kwa kipindi cha Nusu mwaka (Julai – Disemba, 2024);

(f) Uchambuzi wa Taarifa za utendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu na Taasisi zinazozisimamia; na

(g) Ziara za mafunzo.

**Kupokea Taarifa za utekelezaji wa Maazimio**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024. Lengo la kupokea taarifa hizi lilikuwa ni kufuatilia iwapo Serikali imezingatia Maazimo ya Bunge na kama imezingatia ni kwa kiasi gani yametekelezwa katika kuleta ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maazimio ya Bunge uliofanywa na Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hizi. Pamoja na utekelezaji mzuri wa maazimio hayo, Kamati imebaini kuwa yapo maazimio machache ambayo hayakutekelezwa. Kwa upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Maazimio ambayo hayakutekelezwa ni pamoja na Serikali kuongeza fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana, Serikali kufanya tathmini na kuunganisha Mifuko yote ya Uwezeshaji Wananchi kwa lengo la kuwa na mifuko michache ambayo itawezesha vijana kupata ujuzi na kuwawezesha kupata mitaji, Serikali kutoa fedha za Programu ya Taifa ya kukuza Ujuzi kulingana na makubalioano ya kutoa 1/3 ya SDL, Serikali kuongeza bajeti ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ili kukamilisha usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa Uendeshaji mashauri na utunzaji kumbukumbu katika Ofisi zake zote nchini.

Aidha, kwa upande wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, maazimio ambayo hayajatekelezwa ni pamoja na kuongeza kasi ya utoaji wa vitambulisho vya kidigitali kwa wafanyabiashara ndogondogo ili waweze kutambulika na kupata fursa mbalimbali, Serikali kuweka mikakati inayotekelezeka ya kuhakikisha fedha zilizokopeshwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) zinarejeshwa, Serikali kubuni na kubainisha vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mtaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na kuwanufaisha wanawake wengi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Maazimio yaliyofikiwa na Bunge yalilenga kuongeza tija katika shughuli zinazofanywa na Wizara hizi ili kufikia lengo mahsusi la kuleta Ustawi kwa Watanzania.

### 2.1.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilitekeleza takwa hilo la Kikanuni kwa kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo iilyotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (Fungu 65) na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu (Fungu 53). lengo la ziara hizo ni kujiridhisha juu ya tija inayopatikana katika miradi na programu zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kutokana na ziara hizo Kamati iliweza kuwianisha taarifa zinazotolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi iliyopo kwenye maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa mitatu ambayo ni Tabora, Mara na Mwanza kuanzia tarehe 12 – 20 Machi, 2024. Taarifa za kina kuhusu yaliyobainika katika Ziara hizo pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yaliwasilishwa katika Taarifa za Bajeti mnamo mwezi Aprili na Juni, 2024

### 2.1.2 Uchambuzi wa Miswada mbalimbali ya Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 97(1) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, ulielekeza Miswada mbalimbali ya Sheria iweze kuchambuliwa na kushughulikiwa na Kamati kwa Mujibu wa Kanuni. Miswada iliyoshughulikiwa na Kamati ni pamoja na;

(a) Muswada wa Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024, [*The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments), Bill, 2024]*

(b) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii Na.3 wa Mwaka 2024. [*The Social Security Laws (Amendment) Bill, 2024];*

(c) Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *[ The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024)]*

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuweza kushughulikia Miswada hii kwa namna inayofaa Kamati iliita wadau mbalimbali ili waweze kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yaliweza kuboresha maudhui yanayopatika katika Miswada hiyo. Aidha katika Muktadha huu Kamati inapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuridhia Miswada miwili iliyopitishwa na Bunge lako tukufu kuwa Sheria ya Nchi, ikiwa ni sehemu ya Juhudi za Serikali kuleta ustawi kwa Wananchi kwa kufanya maboresho ya Sheria mbalimbali.

**2.1.3 Kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za kina za Uchambuzi wa Bajeti za Wizara hizo na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ziliwasilishwa Bungeni Mwezi Juni, 2024.

**2.1.4 Kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba.2024)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kupokea, kuchambua na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2024) za Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu. Lengo la kufanya hivyo ilikuwa ni kuona mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha ili kuweza kuishauri Serikali kwa namna inayofaa hii inatokana na msisitizo kuwa Serikali inategemewa kufikia Disemba 2024 ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha uwe umefikia angalau asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

a) **Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**.

Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Waziri Mkuu ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 40,500,000,000** hadi kufikia Disemba 2024 kiasi cha **Shilingi 20,559,192,891** kimekusanywa sawa na **asilimia 50** ya lengo. Aidha kwa upande wa Bajeti Wizara imepokea kiasi cha **Shilingi 18,606,294,368** sawa na **asilimia 48** ya fedha iliyotengwa. Katika kiasi hicho fedha zilizopokelewa kwaajili ya miradi ya maendeleo ni **Shilingi 7,269,725,616** sawa na **asilimia 49.28** ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha si wa kuridhisha kwani upo chini ya asilimia 50.

**b) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 7,040,129,000** hadi kufikia Disemba 2024 kiasi cha **Shilingi 2,132,144,239** kimekusanywa sawa na **asilimia 30** ya lengo. Aidha kwa upande wa Bajeti Wizara imepokea kiasi cha **Shilingi 27,294,732,463** Sawa na **asilimia 40.20** ya kiasi cha **Shilingi Bilion 74.22** kilichoidhinishwa

na Bunge. Aidha fedha zilizopokelewa kwaajili ya miradi ya maendeleo ni **Shilingi 7,307,188,891** sawa na **asilimia 35.79** ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Wizara hii si wa kuridhisha. Kamati inatoa msisitizo kuwa Serikali itoe fedha katika Wizara hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

**2.1.5 Kufuatilia Utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Nyongeza ya 7(1)(d) Kamati ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, ajra na Wenye Ulemavu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kama ifuatavyo;-

**A. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika**, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa za utekelezaji kama ifuatavyo:-

**(i) Suala la Wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya michango wanayodaiwa waajiri wao.**

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 04 Juni, 2024 kwenye Kikao cha Arobaini cha Mkutano wa Kumi na Tano ulielekeza kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ishugulikie suala la Wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya michango wanayodaiwa waajiri wao ili waweze kulipwa mafao yao. Maelekezo hayo yalitolewa kufuatia Mwongozo ulioombwa na Mhe. Esther Nicholus Matiko, Mb kuhusu jambo lililotokea wakati wa kujibu Swali la Nyongeza la Mhe. Ally Mohamed Kassinge, Mb. Swali hilo lilihusu wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya waajiri wao ya michango kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba ninukuu maelekezo yako "Jambo hili Waheshimiwa Wabunge si rahisi kulitolea Mwongozo kwa sababu siko na takwimu hapa, lakini nalipeleka hili jambo kwa Kamati yetu ambayo Ofisi hii inaripoti kwake ili waweze kulifuatilia kwa ukamilifu kwa maana ya Serikali kule itapata nafasi ya kupeleka taarifa, Pia, kama iko sababu, waitwe Wakurugenzi hawa wa hii Mifuko yote hapa nchini, ili wakaeleze kule kwenye Kamati ni mazingira gani. Hapa siyo wa Serikali pekee pengine na wa Binafsi kwasababu mifuko yote iko chini ya Ofisi hii, basi waende kule wakaeleze ni mazingira gani wanamdai mwajiriwa fedha"

**Mheshimwa Spika,** kufuatia maelekezo yako, Kamati ilialika Wadau mbalimbali kuja mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu suala hilo vikiwemo Vyama vinavyounda TUCTA, pamoja na Umoja wa Wastaafu Tanzania (REAT).

**Mahojiano na Wadau waliofika mbele ya Kamati.**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa mahojiano ya wadau mbalimbali wakiwemo TUCTA na REAT walithibitisha kwamba kwa nyakati tofauti wamepokea malalamiko ya wastaafu kutakiwa kulipa madeni ya michango ambayo ilipaswa kulipwa na mwajiri ili waweze kulipwa mafao yao. Ushahidi wa maelelezo yao ni nyaraka za uthibitisho zilizowasilishwa **(Kielelezo Na. 1)**

**Mheshimiwa Spika,** upande wa Serikali, ulieleza kuwa Sheria na Miongozo ya Mifuko hairuhusu Mwanachama kulipa michango ya mwajiri ili alipwe mafao. Hata hivyo iliongezwa kuwa mazingira yanaweza kutokea na kusababisha wastaafu kulipa michango hiyo endapo Wastaafu watatumia namba za malipo zilizotolewa na Mfuko kwenda kwa Mwajiri.

**Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** kupitia mahojiano na nyaraka zilizowasilishwa, Kamati ilibaini kwamba baadhi ya wastaafu walilazimika kupewa nyaraka zenye Namba ya Malipo kwa ajili ya

kulipa madeni ya mwajiri ili waweze kulipwa mafao yao. Kamati ilitaka kujua ni namna na mazingira gani mstaafu anapata nyaraka yenye Namba ya Malipo. Serikali ilieleza kuwa Mfuko hutoa namba hiyo kwa mwajiri na mwajiri ndiye ambaye humpatia mstaafu namba hiyo ili alipe. Hata hivyo serikali ilishindwa kuwasilisha ushahidi wa namba ya malipo waliyotoa kwa mwajiri na ikaja kulipwa na mstaafu.

**Mheshimiwa Spika,** wastaafu hawa wanalazimika kulipa kwa kuwa hawana kingine wanachotegemea zaidi ya mafao yao. Suala hili si sawa hata kidogo hasa ikizingatiwa kuwa sheria haizuii mstaafu kulipwa mafao yake hata kama mwajiri hajakamilisha michango yake. Hivyo, basi kwa msingi huu ni wazi PSSSF inawawajibisha wastaafu kwa makosa yake yakushindwa kusimamia Sheria kwa kuhakikisha mwajiri anawasilisha michango yake kwa wakati. Aidha, kupitia nyaraka na mahojiano yaliyofanywa na wadau, Kamati ilibaini kuwa suala hili limekuwa likifanywa na PSSSF, na hakuna ushahidi na vielelezo uliopata dhidi ya NSSF.

**ii) Utekelezaji wa Wakala wa Usalama na Afya Mahala Pa Kazi (OSHA)**

**Mheshimiwa Spika,** OSHA ni chombo mahsusi kilichoanzishwa na Serikali kwa lengo la kusimamia Usalama na Afya mahali pa kazi Tanzania Bara kupitia Sheria Na 5 ya Mwaka 2003 ambapo usimamizi huo utapunguza ajali, magonjwa na vifo, aidha matokeo ya usimamizi huo ni kuongeza tija na uzalishaji mali na hatimaye kukuza pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Taarifa hii kwa kiasi kikubwa Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa majukumu ya OSHA hasa katika suala zima la kusimamia matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya ya Mwaka 2003. Mathalani ongezeko la usajili wa maeneo ya kazi ambapo limetokana na matumizi ya mfumo wa TEHAMA (Online registration), ukaguzi wa usalama maeneo ya kazi, upimaji wa afya, uchunguzi wa ajali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayofanywa na OSHA ya kuhakikisha kuwa ustawi wa wafanyakazi unaboreshwa, kamati imebaini kuwa Sera ya Usalama na Afya Mahala pa kazi ya Mwaka 2010 ni ya muda mrefu hivyo inahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuendana na Miongozo ya Kanuni za Shirika la Kazi Duniani (ILO). Aidha Wakala huu bado unaendelea kukabiliwa na changamoto za uhaba wa watumishi, uhaba wa Ofisi, vitendea kazi na uelewa mdogo wa masuala ya usalama na katika maeneo mbalimbali ya kazi.

**iii) Utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetokana na makubaliano kati ya Serikali na Sekta binafsi kupitia Maabara ya Mpango wa kuboresha mazingira ya Biashara Nchini ikiwa na lengo la kuboresha nguvu kazi ya Taifa kwa kuhakikisha inakuwa na ujuzi stahiki ili kuwa na tija katika uzalishaji na kupunguza hali ya Taifa kuajiri wageni kutoka nje, suala ambalo linawaongezea gharama za ufanyaji biashara nchini. Aidha Kamati ilielezwa kuwa kulikuwa na makubaliano ya matumizi ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi (Skills and Development Levy) kati ya Serikali na Waajiri 1/3 ya makusanyo ya SDL yatumike kugharamia ukuzaji ujuzi kwa nguvukazi iliyopo katika soko la ajira. Programu hiii ilikuwa ni ya miaka 10 kuanzia 2016/2017 hadi 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa licha ya kuwa na uhitaji mkubwa wa Vijana kupatiwa Ujuzi kupitia Programu hii, utolewaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha umekuwa ukishuka kila mwaka na kusababisha kushuka kwa wastani wa vijana kutoka 42,000 hadi kufikia 12,000 kwa mwaka kinyume na Mpango wa Taifa wa Maendeleo ambao unaeleza kuwa jumla ya vijana 681,000 wanatakiwa kupatiwa mafunzo kwa kipindi cha miaka 5, sawa na vijana 136,000 na Shilingi Billion 109.8 kwa mwaka. Aidha vijana wengi wanakosa mitaji ya kuanzisha shughuli za kiuchumi baada ya kupata mafunzo.

**iv) Utekelezaji wa Jukumu la Uratibu wa Uunganishaji Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi.**

**Mheshimiwa Spika,** suala la uunganishaji Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi ni moja ya jukumu linalotekelezwa na Kitengo cha Huduma za Ajira kwa kushirikiana na wadau wengine. Uratibu wa uunganishaji Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi linafanywa kwa kuzingatia Sheria ya Kukuza Huduma za Ajira Na.9 ya Mwaka 1999 pamoja na Kanuni za Mawaka Binafsi wa Ajira wa Mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2024 jumla ya Watanzania 5,057 wameunganishwa na fursa za ajira nje ya nchi ambapo asilimia 92.6 ya Watanzania waliounganishwa na fursa za ajira nje ya nchi walikuwa na ujuzi wa chini, asilimia 4.06 ujuzi wa kati na asilimia 3.34 walikuwa na ujuzi wa juu.

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao mbalimbali vilivyofanyika baina ya Kamati na Serikali, suala la kazi pamoja na ajira hususani kwa vijana, limekuwa likitawala majadiliano. Msingi wa majadiliano hayo, unatokana na nia thabiti ya Wajumbe kuona kwamba, masuala ya kazi na ajira yanapewa kipaumbele inavyostahili ili Serikali iwe na mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba, Watanzania na hasa vijana wananufaika na mikakati ya kuongeza fursa za ajira na kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kuwa kasi ya uunganishwaji wa ajira Watanzania nje ya nchi si wa kuridhisha ukilinganisha na mataifa mengine. Hii inatokana na kukosekana kwa Mamlaka mahususi inayoshughulikia masuala ya ajira za nje ya nchi jambo linalopekea kukosekana kwa mapato ya nchi na kipato cha Watanzania kwa ujumla. Hii inatokana na ukweli kwamba jukumu hili kubwa limewekwa kwenye Kitengo ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye ulemavu ambao hawajawezeshwa kibajeti na Watumishi. Mathalani kwa Mwaka 2024/2025 kilitengewa kiasi cha Shilingi 358,737,947, Watumishi 31 na Ofisi katika kanda nne za Dodoma, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam.

v) **Utekelezaji wa Majukumu ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kutoa fidia stahiki na toshelevu kwa wafanyakazi ambao wanapata ajali au magonjwa yatokanayo na kazi na ikiwa ni kifo fidia italipwa kwa wategemezi wao.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu umepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake, moja ya mafanikio hayo ni kuongezeka kwa usajili wa wanachama wapya, kuongezeka kwa kiwango cha makusanyo ya michango, kuogezeka kwa kiwango cha ulipaji wa fidia kwa wanufaika, kuongezeka kwa ukusanyaji wa Mapato yanayotokana na Uwekezaji, Kuimarisha utoaji wa huduma za Mfuko kwa njia ya kidigitali**.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ya mfuko huu, Kamati ilibaini kwamba zipo changamoto zinazokabili Mfuko, moja ya changamoto hizo ni ucheleweshaji wa kuwasilisha michango kutoka kwa baadhi ya waajiri jambo linaloathiri ufikiwaji wa malengo ya Mfuko kwa upande wa makusanyo; Uwasilishaji wa nyaraka pungufu kwa baadhi ya wanufaika; matarajio yasiyo halisi juu ya viwango vya fidia kwa baadhi ya wafanyakazi.

**vi) Utekelezaji wa Uratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Mashirikisho.**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inajukumu la kusajiri Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri na Mashirikisho kwa kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366 na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Vyama hivyo. Kamati ilielezwa kuwa mpaka sasa Ofisi imesajili Vyama vya Wafanyakazi Thelathini na Tatu (33) na Chama cha Waajiri Kimoja (1)

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi wa Taarifa hii, Kamati ilibaini Mapungufu yafuatayo ya kisheria;-

(a) Kukosekana kwa mamlaka ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Msajili hana mamlaka yoyote ya kisheria ya kuchukua hatua dhidi ya chama pindi itakapobainika kuwa Chama kimekiuka masharti ya usajili wake.

(b) Uwanda wa Usajili wa Wanachama. Vyama vimepewa mamlaka ya kusajili wanachama na vinatakiwa kueleza maeneo ya usajili wa wanachama bila kuweka mipaka ya Vyama hivyo kusajili na kuhudumia wanachama. Hali hiyo imesababisha baadhi ya Vyama kubainisha katika Katiba zao maeneo yote ya ajira nchini ya kuhudumia wanachama na hivyo kupelekea muingiliano na kuleta migogoro.

(c) Kutokuwepo kwa Kanuni Mahsusi za Vyama vya Wafanyakazi. Masuala ya Vyama vya Wafanyakazi yapo katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366 kwa jinsi Vifungu hivyo vilivyo havijitosherezi katika kuweka bayana masuala ya wafanyakazi na haki ya uhuru wa kujumuika hali inayopelekea migogoro katika tafsiri ya sheria.

(d) Mapungufu katika Katiba za Vyama vya Wafanyakazi. Katiba za Vyama hazijabainisha kwa uwazi wigo na mipaka ya usajili wa wanachama wao na hivyo kusababisha mgogoro baina ya Vyama katika kusajili wanachama kinyume na Kanuni ya 23(1) ya KAnuni za Ajira na Mahusiano Kazini. Aidha Katiba hizo zina mkangavyiko katika uratibu wa uitishwaji wa vikao na namna ya kufikia uamuzi ikiwa ni pamoja na akidi inayotakiwa ili kikao kiwe halali na baadhi ya Katiba hazijabainisha ukomo wa muda wa kukaa madarakani kwa viongozi hali inayosababisha migogoro ya mara kwa mara.

(e) Mapungufu katika Katiba ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA). TUCTA ndicho chombo

kinachounganisha nguvu ya Wafanyakazi kupitia vyama wanachama, hata hivyo Katiba ya TUCTA haina Ibara yoyote inayoeleza jukumu la TUCTA la kushughulikia migogoro ya wanachama wake na namna migogoro hiyo itakavyoshughulikiwa.

**vii) Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu ulianzishwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Sura 183 Kifungu cha 57 pamoja na Kanuni ya 67 ya Kanuni za Ujumla za Utekelezaji wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu za Mwaka 2012 ukiwa na lengo la kuchagiza uwezeshaji wa Watu wenye Ulemavu kushiriki kwenye shughuli za kijamii na kichumi ili kujiletea maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko huu ni pamoja na kukamilisha kwa Mpango kazi wa Taifa wa Ustawi na Haki kwa Watu wenye Ualbino, kukamilisha kwa mkakati wa taifa wa teknolojia saidizi kwa watu wenye ulemavu, kukamilisha na kusambaza Mfumo wa Kieletroniki na Kanzi data kwa Watu wenye Ulemavu, kutoa ruzuku ya Shilingi Milioni 200 kwa Vyama na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu.
Hata hivyo zipo changamoto zinazokabili Mfuko huu ikiwa ni pamoja na mapungufu kwenye Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na.9 ya Mwaka 2010 ikiwemo vifungu vinavyohusu Mfuko ili kuendana na hali ya sasa.

**viii) Mfumo wa Usimamizi wa Uendeshaji wa Mashauri wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ushauri wa Kamati Tume ilianzisha mchakato wa kusimika Mfumo wa Kidigital wa Usimamizi na Uendeshaji wa Mashauri *(Online Case Management System-OCMS).* Mfumo huu ulitengenezwa kati ya Mwaka 2020 hadi 2022 ambapo mfumo huu ni kwaajili ya kurahisisha usajili wa mashauri yanapofika Tume na kuwapangia Wasuluhishi na Waamuzi

kwaajili ya kusikiliza kupitia mfumo hali itakayorahisiha utendaji kazi wa Tume na kutoa haki kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa licha ya Mfumo huu kuwa ni wa muda mrefu lakini bado Ofisi katika Mikoa 9 hazijasimikwa mfumo huu. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iharakishe usimikaji wa Mfumo huu ili kuendana na uendeshaji wa kisasa wa mashauri kama ilivyo kwa Mahakama.

**B. WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua taarifa za utekelezaji zifuatazo:-

**(i) Uratibu wa Shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo.**

**Mheshimiwa Spika,** Jukumu hili la kuratibu shughuli za Wafanyabiashara ndogondogo lipo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Lengo la kuratibu kundi hili ni kutatua changamoto ya ajira ili kuwawezesha kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii na hatimae kujikwamua na kuchangia katika pato la Taifa. Makundi yanayoratibiwa yanajumuisha machinga, mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji, wasusi, washonaji nguo na makundi mengine ambayo pato ghafi halizidi Milioni Nne.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa moja ya shughuli zilizotekelezwa ni kutambua na kusajili na kutoa Vitambulisho vya kidigitali kote nchini ili kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo, ambapo jumla ya Wafanyabiashara 45,847 wamesajiliwa nchi nzima na kati ya hao 15,278 wamelipia gharama ya kitambulisho Shilingi 20,000 kupitia mfumo wa GePG. Aidha, vitambulisho hivyo vimeunganishwa na mifumo mingine ikiwemo mfumo wa Vitambulisho vya Taifa, Anwani ya Makazi, Taasisi za Fedha, Bima ya Afya na Mifuko ya

Hifadhi za Jamii; Utoaji wa Mikopo kupitia Benki ya Nmb yenye Riba ya asilimia 7 kwa Mwaka, ambapo Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi Bilioni 10.5 kwaajili ya kukopesha wafanyabiasha hawa na tayari Shilingi Bilion 5 zimepelekwa NMB kwa ajili ya kuanza kukopeshwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kasi ya uandikishaji wafanyabiashara ndogondogo si ya kuridhisha, jambo linalopelekea wafanyabiashara wengi kukosa fursa ya kupata mikopo na fursa nyingine zinazoweza kuwasaidia kujikwamua kiuchumi. Aidha Kamati ilibaini kuwa kundi kubwa la Wafanyabishara ndogondogo hawapo kwenye majukwaa au vyama vya mashirikisho jambo linalopelekea kushindwa kuwaunganisha na kuwaelemisha juu ya umuhimu wa kujiandikisha na fursa zilizopo. Kukosekana kwa kanzi data ya Wafanyabiashara ndogondogo kunapelekea kushindwa kujua mahitaji halisi ya Wafanyabiashara hao na kuweza kuwawezesha.

### (ii) Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO)

**Mheshimiwa Spika,** Mashirika yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakisajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya Mwaka 2002 chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu. Mashirika haya ni wadau muhimu ambao wamekuwa wakichangia maendeleo nchini, kupitia sekta za huduma za afya, elimu, maji na sekta za uchumi ikiwemo kilimo, ufugaji, nishati na madini. Kamati ilijulishwa kuwa jumla ya mashirika yaliyosajiliwa na kuwa hai ni mashirika 9,773 mpaka hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Mshirika yasiyo ya Kiserikali ndiyo yenye jukumu kubwa la kuratibu usajili wa Mashirika haya ikiwa pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera, kutuza Rejesta, kupitia mikataba yote ya fedha za ufadhili na kuratibu utendaji wa mashirika haya wakisaidiwa na Wasajili Wasaidizi ambao huteuliwa na Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka miongoni mwa Watumishi wa Umma kutoka katika Mikoa na Halmashauri kwa lengo la kusimamia na kuratibu mashirika

yasiyo ya kiserikali katika maeneo yao. Katika majadiliano na Wizara, Kamati ilibaini kuwa utendaji kazi wa Wasajili wasaidizi katika kufuatilia mashirika haya umekuwa hafifu kutokana na kuwa na majukumu mengi ya kiofisi kutoka kwenye ofisi zao za TAMISEMI**.**

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto kubwa inayokabili uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ni ufinyu wa bajeti ya kuwawezesha kufuatilia kazi zinazofanywa na mashirika ili kuona kama zinaendana na madhumuni ya usajili, mathalani katika Mwaka 2023/2024 Wizara iliweza kuyafikia Mashirika 1,662 kati ya Mashirika 9,242 yaliyosajiliwa; kumekuwa na changamoto ya baadhi ya Mashirka kujihusisha na masuala ya mmomonyoko wa maadili kinyume na tamaduni za Nchi, utakatishaji fedha na mashirika yanayojihusisha na siasa wakati wa uchaguzi; Baadhi ya Mashirika kutohuisha taarifa zao kwenye mfumo wa Kieletroniki jambo linalosababisha Ofisi ya Msajili kushindwa kuwa na taarifa sahihi hasa kwenye maeneo ambayo mashirika yanafanya kazi ikiwa ni pamoja na shughuli wanazozifanya.

### (iii) Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF)

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la kuanzishwa kwa mfuko ni kuwajengea wanawake mazingira ya upatikanaji wa mitaji ya uendeshaji wa miradi ya kiuchumi kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu. Aidha, kuanzishwa kwa Mfuko ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu una mtaji wa kiasi cha **Shilingi 1,273,733,291.16** ambapo fedha zilizopo kwenye akaunti ni **Shilingi 322, 537, 389** na **Shilingi 475,488,459.90** madeni yalipo Halmashauri ambayo hayajarejeshwa na **Shilingi 461,825,598** ni madeni ambayo Wizara iliwakopesha vikundi vya wajasiliamamli na mjasiriamali mmojammoja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kumekuwa na urejeshwaji usioridhisha kutoka Halmashauri na vikundi

vilivyokopeshwa hivyo kufanya mfuko kuwa na madeni ya muda mrefu na kupelekea kushindwa kutoa mikopo kwa walengwa.

**(iv) Uratibu wa Utekelezaji wa Mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto uliandaliwa kwa lengo la kupunguza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa asilimia 50. Mpango kazi huu una maeneo mahsusi nane (8) ya utekelezaji ambayo ni: Kuimarisha Uchumi wa Kaya; Mila na Desturi; Mazingira Salama katika Maeneo ya Umma; Malezi, Msaada kwa Familia na Mahusiano; Utekelezaji na Usimamizi wa Sheria; Utoaji wa Huduma kwa Waathirika wa Ukatili; Mazingira Salama Shuleni na Stadi za Maisha; na Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa kiasi kikubwa imeridhishwa na uratibu wa mpango huu na inaipongeza Wizara kwa kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi mkubwa. Katika kutekeleza matokeo mbalimbali yameonekana ikiwemo ukatili wa kimwili kwa wanawake kupungua kutoka 40% mwaka 2015 hadi kufikia 25%; ukatili wa kingono kwa wanawake kupungua kutoka 17% mwaka 2015 hadi 12%; vitendo vya ukeketaji kutoka 10% 2015 hadi 8%; kuongeza dawati la jinsia na watoto katika vituo vya polisi; kuanzishwa kwa madawati 104 katika maeneo ya sokoni; kuanzisha madawati ya jinsia 295 katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati.

**Mheshimiwa Spika,** uratibu wa mpango huu unakabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo; Afua za MTAKUWWA kutokupewa kipaumbele katika Mipango na Bajeti za Wizara za Kisekta ambapo hii imekuwa ni changamoto inayojirudia, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutokana na kutoshirikishwa kwa watoa maamuzi wenye mamlaka ya kisiasa katika Kamati ya Elekezi ya MTAKUWWA; Kuibuka kwa aina mpya za ukatili ikiwemo ukatili wa mitandaoni; Kutokuwepo kwa mifumo jumuishi na

shirikishi ya kielektroniki ya ukusanyaji wa taarifa na takwimu sahihi kwa wakati.

**2.2 Semina, Mafunzo na Ushiriki wa Matukio Mbalimbali.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, wajumbe walipata fursa ya kushiriki katika semina na warsha mbalimbali ambazo zililenga kuwajengea uwezo. Kamati inawashukuru wadau wote ambao walijitokeza katika kutoa semina za mafunzo na kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati. Semina na warsha hizo zimekuwa na manufaa katika kuongeza uelewa wa Wajumbe katika sekta mbalimbali zinazosimamiwa na Kamati na hivyo kuiwezesha Kamati kutoa ushauri wenye tija. Ni imani ya Kamati kuwa ushirikiano huo utaendelea katika kuijengea Kamati uwezo kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO**

**3.1 Maoni ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia utekelezaji wa shughuli za Kamati, katika kipindi cha Mwaka 2024, Kamati ina maoni yafuatayo;-

**3.1.1 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.**

(a) Mifuko kutosimamia kwa ukamilifu Waajiri kutoa Michango ya Wanachama kwa wakati inapelekea baadhi ya Wastaafu Wastaafu kulipa michango ya mwajiri pindi wanapofuatilia mafao yao.

(b) Kutokufanyiwa marejeo kwa Sera ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi ya Mwaka 2010 kunapelekea kushindwa kuendana na miongozo na Kanuni za Shirika la Kazi Duniani (ILO).

(c) Kutokuwepo kwa Chombo kinachosimamia program zinazotolewa kwa Vijana kunapelekea kukosekana kwa ufuatiliaji thabiti wa proramu hizi na kusababisha kutopatikana kwa tija zinazokusudiwa.

(d) Uhaba wa watumishi, upungufu wa miundombinu kama Ofisi hususani Mikoani na maeneo ya vijijini na vitendea kazi kunasababisha OSHA kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuathiri utendaji wa Taasisi.

(e) Mapungufu katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366 inapelekea Ofisi ya Uratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Mashirikisho kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(f) Kutokuwepo kwa Mamlaka inayosimamia ajira za Nje Nchini kunapelekea kuwa na ufanisi hafifu katika kuwatafutia Watanzania fursa za ajira Nje ya Nchi.

**3.1.2 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

(a) Elimu isiyotoshelevu na endelevu kuhusu fursa za uwezeshaji kwa Wafanyabiashara Ndogondogo ikiwemo Mikopo yenye riba nafuu inayotolewa na Serikali, inaathiri kwa kiasi kikubwa mwamko wa Wafanyabiashara hao kuchangamkia fursa hiyo na uandikishaji wa Vitambulisho vya Kidijitali.

(b) Uwepo wa Wasajili Wasaidizi ambao ni Waajiriwa wa TAMISEMI na wenye majukumu mengi ya kazi katika Ofisi zao kunaathiri kwa kiasi kikubwa utendaji kazi wa Wasajili hao katika kufuatilia kazi zinazofanywa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

(c) Ufinyu wa bajeti katika Idara ya Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali inaathiri kwa kiasi kikubwa kutekeleza jukumu la kufuatilia kazi zinazofanywa na mashirika ili kuona kama zinaendana na madhumuni ya usajili.

(d) Uwepo wa Makazi mengi ya Wazee na mahitaji machache baadhi ya maeneo kumepelekea kwa kiasi kikubwa ongezeko la gharama ya kuyatunza makazi hayo.

(e) Madeni makubwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kunaathiri utolewaji wa mikopo kwa wanawake na hivyo kunaathiri tija iliyokusudiwa kutokana na mikopo hiyo.

(f) Kutokuzipa kipaumbele Afua za MTAKUWWA katika mipango ya bajeti ya wizara za Kisekta, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kunaathiri utekelezaji wa mpango huu.

### 3.2 Mapendekezo

**Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**

#### 3.2.1 Changamoto ya Wafanyakazi wanaostaafu kulazimika kulipa madeni ya michango wanayodaiwa waajiri wao.

**KWA KUWA**, Kitendo cha PSSSF kutengeneza mazingira ya kuwafanya baadhi ya Wastaafu kulipa michango ya Mwajiri ili waweze kulipwa mafao yao,

(i) Ni kinyume cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Sura 371 na kinaondoa imani ya mwajiriwa kwa Mfuko huo;

(ii) Hakipaswi kuvumiliwa na Bunge ambalo ndio lenye mamlaka ya utungaji wa Sheria;

(iii) Kinakinzana na lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huo wa kuhakikisha ustawi wa Wanachama.

**NA KWA KUWA,** Kutokurekebishwa kwa hali hiyo ni jambo linaongeza kero miongoni mwa wananchi.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe kuwa**;**

(i) PSSSF inawarejeshea fedha za michango zilizolipwa na baadhi ya Waastafu na kuzidai fedha hizo kwa Waajiri kama Sheria inavyoelekeza;

(ii) Mifuko iache mara moja utaratibu wa kutoa Namba za Malipo kwa Wastaafu ili walipe michango ambayo haijawasilishwa na Mwajiri wakati wakifuatilia mafao yao; na

(iii) Mifuko ichukue hatua kali za kisheria kwa waajiri wasiowasilisha michango kwa mujibu wa Sheria.

**3.2.2 Dosari za Utekelezaji wa Sera ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi ya Mwaka 2010.**

**KWA KUWA**, utekelezaji wa Sera ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi umebainika kuwa na dosari ya kutoendana na miongozo na Kanuni za Shirika la Kazi Duniani (ILO);

**NA KWA KUWA, dosari hiyo inaathiri usalama mahala pa kazi** na sifa ya Nchi katika Jumuiya ya Kimataifa;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye marejeo ya Sera hiyo ili kuendana na Kanuni na Miongozo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO).

**3.2.3 Uhaba Miundombinu na vitendea kazi kwa Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (OSHA)**

**KWA KUWA**, uhaba wa miundombinu hususani Ofisi katika Mikoa na Wilaya zimekuwa ni changamoto za muda mrefu;

**NA KWA KUWA**, Uhaba huo umesababisha OSHA kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuathiri jukumu lao la kuwalinda wafanyakazi dhidi ya magonjwa na ajali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: **-**

(i) Serikali itenge bajeti itakayokidhi mahitaji ya OSHA ili kuongeza Ofisi katika Mikoa na Wilaya na vitendea kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi nakusogeza huduma karibu na Wanachama;

(ii) Serikali isimamie Wakala kuongeza kasi ya kusajili maeneo yote ya kazi nchini na kutoa miongozo ya namna ya kuwalida wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya magonjwa na ajali kazini;

### 3.2.4 Ufanisi wa Utendaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

**KWA KUWA**, kumekuwepo na kasi ndogo ya uandikishaji wa Wanachama waliopo katika Sekta isiyo rasmi na pia ipo changamoto ya uelewa juu ya masuala mbalimbali yanayohusu fidia kwa wafanyakazi na taratibu za ulipaji wa fidia jambo linalosababisha wanachama wengi kukosa haki zao;

**NA KWA KUWA,** kutokuwepo na Ofisi za Mfuko katika Mikoa na Wilaya zote nchini kunaathiri ufikiwaji wa wanachama katika maeneo yao hivyo kuathiri makusanyo na ulipaji wa fidia stahiki kwa wakati;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe Mfuko: **-**

(i) unaandaa Mkakati wa kuwaandikisha Wanachama waliopo katika Sekta isiyo rasmi hasa wale

wanaojishughulisha na shughuli hatarishi kama Fundi Ujenzi na Watu wa Migodini ili kuweza kuongeza idadi ya wanachama na kuwasaidia pindi wanapopata ajali kazini.

(ii) unaandaa mkakati endelevu unaotekelezeka wa kutoa elimu kwa Waajiri na waajiriwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwenye Ofisi mbalimbali za Wanachama juu ya masuala mahususi yanayohusu fidia kwa wafanyakazi na taratibu za ulipaji wa fidia.

(iii) unaweka mkakati wa ujenzi wa Ofisi kwenye Mikoa na Wilaya zote nchini ili kusogeza huduma jirani na wanachama.

**3.2.5 Ufinyu wa Bajeti katika Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini.**

**KWA KUWA**, mwenendo wa mgao wa fedha za utekelezaji wa program hii umekuwa ukishuka kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano kinyume na makubaliano ya matumizi ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi (Skills and Development Levy-SDL)

**NA KWA KUWA**, kushuka kwa mgao wa fedha kumesababisha kushuka kwa idadi ya vijana wanaonufaika na Programu kutoka wastani wa vijana 42,000 hadi kufikia 12,000 kwa mwaka kinyume na Mpango wa Taifa wa Maendeleo unaotaka jumla ya vijana 681,000 kupatiwa mafunzo kwa kipindi cha miaka mitano, sawa na vijana 136,000.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali itenge na kutoa fedha za program hii kwa kufuata makubaliano ya kutoa 1/3 ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi (SDL) kwa ajili ya kugharamia ukuzaji ujuzi kwa nguvu kazi iliyopo katika soko la ajira. Kufanya hivyo kutawezesha vijana wengi kupata ujuzi na kujiajiri.

(b) Serikali iharakishe zoezi la kufanya tathmini itakayosaidia kuona umuhimu wa kuunganisha Programu na Mifuko yote ya Uwezeshaji Wananchi na kuingushanisha kwa lengo la kuwa na mifuko michache ambayo itawezesha vijana kupata ujuzi na kuwezeshwa mitaji ili kuwa na tija endelevu kwa wanufaika.

### 3.2.6 Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Ajira za Ndani na Nje ya Nchi

**KWA KUWA**, Nchi yetu haina Mamlaka ya Kusimamia Ajira za Ndani na Nje ya Nchi na jukumu hilo linatekelezwa na Kitengo cha Huduma za Ajira chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira n Wenye Ulemavu;

**NA KWA KUWA,** Kukosekana kwa Mamlaka hiyo kunaathiri kwa kiasi kikubwa kasi ya uunganishwaji wa ajira Watanzania nje ya nchi ukilinganisha na mataifa mengine jambo linalopekea kukosekana kwa mapato ya nchi na kipato cha Watanzania kwa ujumla;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,** Serikali ianze mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya ajira Nchini ili kuwepo na chombo kinachosimamia ajira Nchini na hivyo kuwezesha Watanzania wengi kupata fursa za ajira hasa ajira za ujuzi wa juu Nje ya Nchi.

### 3.2.7 Mapungufu katika Utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366.

**KWA KUWA,** utekelezaji wa sheria hii unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo Sheria kutompa mamlaka ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, Kutokuwepo kwa Kanuni Mahsusi za Vyama vya Wafanyakazi, Mapungufu katika Katiba za Vyama vya Wafanyakazii;

**NA KWA KUWA,** changamoto hizo zinapekelea Ofisi ya Uratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Mashirikisho kushindwa kuratibu kwa ufanisi Shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Mashirikisho na hivyo kuibuka kwa migogoro ya mara kwa mara katika Vyama hivyo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali ifanye Marekebisho ya Sheria hii ili kuimarisha utekelezaji wake na kuipa nguvu ya Kiutendaji Ofisi ya Mratibu wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Mashirirkisho;

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu.**

**3.2.8 Ufanisi katika uratibu wa Mashirika yasisyo ya Kiserikali (NGO)**

**KWA KUWA**, upungufu wa rasilimali fedha na rasilimali watu hasa Wasajili Wasaidizi kunaathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali nchini;

**NA KWA KUWA**; kukosekana kwa rasilimali fedha na rasilimali watu kumepelekea kushindwa kufuatilia kwa kina mashirika takribani 9,773 yaliyoenea maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na hivyo baadhi ya mashirika kujihusisha na shughuli ambazo ni kinyume na malengo ya usajili;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba:

(i) Serikali iongeze bajeti ya Wizara ili iweze kufuatilia na kuhakikisha kuwa mashirika yanafanya kazi kwa manufaa ya jamii na maslahi ya Taifa kwa ujumla; na

(ii) Serikali ichukue hatua za haraka na madhubuti ikiwa ni pamoja na kuyafuta Mashirika ambayo yanajihusisha na masuala ya mmomonyoko wa maadili kinyume na tamaduni za Nchi, yanayojihusisha na utakatishaji fedha

pamoja na mashirika yanayojihusisha na siasa wakati wa uchaguzi.

(iii) Serikali ione umuhimu wa kuajiri Wasajili Wasaidizi watakaokuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalumu ili waweze kutekeleza jukumu la ufuatiliaji wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa ufanisi zaidi.

### 3.2.9 Kutolipwa kwa mikopo katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF)

**KWA KUWA,** kumekuwa na mikopo ya muda mrefu iliyokopeshwa kwa Halmashauri, Wanawake na Vikundi mbalimbali nchini na haijarejehswa.

**NA KWA KUWA,** kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunaathiri utolewaji wa mikopo kwa wanawake wengine wenye vigezo vya kupata mikopo hiyo na hivyo kuathiri nia njema ya Serikali ya kuwainua wanawake kiuchumi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iweke mkakati unaotekelezeka wa kuhakikisha fedha zilizokopeshwa zinarejeshwa na kutumika kama ilivyokusudiwa.;

(ii) Serikali ibuni na kubainisha vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mtaji wa Mfuko na kuweza kuwanufaisha wanawake wengi zaidi;

(iii) Serikali iweke mkakati wa kutoa elimu juu ya uwepo wa mfuko ili wanawake wengi wanufaike na mikopo inayotolewa na mfuko huu.

### 3.2.10 Ufanisi mdogo katika kuratibu shughuli za Wafanyabiashara Ndogondogo.

**KWA KUWA**, Ipo changamoto ya uelewa mdogo miongoni mwa Wafanyabiashara Ndogondogo juu ya fursa za uwezeshaji

zinazotolewa na Serikali kwa Wafanyabiashara hao ikiwemo Mikopo yenye masharti nafuu.

**NA KWA KUWA,** Kukosekana kwa elimu hiyo kuna athiri kwa kiasi kikubwa mwamko wa Wafanyabiashara hao kuchangamkia fursa hiyo na uandikishaji wa Vitambulisho vya Kidijitali, jambo linalorudisha nyuma adhma ya Serikali ya kuwakwamua wafanyabiasha hao kiuchumi.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iandae mkakati endelevu wa utoaji wa elimu juu ya fursa hiyo ya mikopo ili Wafanyabiashara Ndogondogo waweze kupata mikopo yenye masharti nafuu na kuweza kujikwamua kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha kwenye majukwaa au vyama vya mashirikisho ya Wafanyabiashara Ndogondogo.

(ii) Serikali iongeze kasi ya utoaji wa vitambulisho vya kidijitali kwa wafanyabiashara ndogondogo ili waweze kutambuliwa na kupata mikopo kutoka Taasisi mbalimbali za kifedha nchini na Mamlaka za Serikali.

### 3.2.11 Changamoto ya Upungufu wa Bajeti inayotengwa katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu.

**KWA KUWA**, Bajeti inayotengwa kwaajili ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuwa ndogo licha ya kwamba Wizara hii ni Mtambuka na hivyo kuwa na majukumu mengi ya kiutendaji.

**NA KWA KUWA**, changamoto hiyo inaathiri ufanisi wa utendaji wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake na kutoa huduma stahiki;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali iongeze bajeti kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na kutoa fedha hizo kwa wakati kama

zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA

### 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe.Fatma Hassan Toufiq, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe.Riziki Said Lulida, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe.Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe.Tecla Mohamedi Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
11. Mhe. Khamis Yusufu Mussa, Mb.
12. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
13. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
14. Mhe. Alli Hassan Omar King, Mb.
15. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
16. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb.
17. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
18. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
19. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb.
20. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
21. Mhe. Januari Yusuph Makamba, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Mhe. Patrobas Katambi Naibu Waziri. Aidha tunampongeza Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mhe. Mwanaidi Ali Khamis, Mb kwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara zao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara hizi pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Bi. Marry Maganga Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Dkt. John Jingu na Manaibu Katibu Wakuu Bw. Amon Anastaz Mpanju na Bi. Felister Peter Mdemu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Idelphonce Leonard, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge Ustawi na Maendeleo ya Jamii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Fatma Hassan Toufiq, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
Februari, 2025

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa, ninamwita Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba Taarifa yote ya Kamati, iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Taarifa yetu ina kurasa zisizopungua 63.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hiyo inaweka sharti la lazima kwa kila Kamati kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake, kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, Sehemu ya Pili inatoa maelezo kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Sehemu ya Tatu, imeainisha maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zimeonesha kuwa, baadhi ya maazimio yalitekelezwa na mengine yanaendelea kutekelezwa. Mfano, azimio lililoripotiwa kutekelezwa ni kuhusu Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)* kuwezeshwa kisheria kwa kuwekewa Kanuni

chini ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuipa mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma za Bima ya Afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji umeonesha kuwa, Kifungu Na. 7 cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kimeipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini *(TIRA)* majukumu kwa lengo la kusimamia utoaji wa huduma za bima nchini na Kanuni Na. 19(1)(e) ya Kanuni ya Bima ya Afya kwa Wote inaipa *TIRA* mamlaka ya kudhibiti utoaji huduma za bima ya afya kupitia skimu za bima zilizoainishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo baadhi ya maazimio yanaendelea kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati thabiti ya kushirikisha Sekta Binafsi *(Public Private Partnerships - PPP)* na kurahisisha uwekezaji wa viwanda vya dawa pamoja na vifaa tiba nchini, ili kukidhi soko la ndani na nje ya nchi. Bohari kuu ya Dawa *(MSD)* kupewa mtaji, kufufua Kiwanda cha Dawa cha Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries)* na kuongeza uzalishaji katika Kiwanda cha Dawa cha Keko *(Keko Pharmaceutical Industries)* ambacho Serikali ya Tanzania ina 70% ya hisa ya umiliki. Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge wakati wote, ili kutoa mrejesho wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji ulibainisha maazimio ambayo hayajatekelezwa kikamilifu. Mfano, maazimio hayo ni pamoja na maazimio kuhusu udhibiti wa chakula na vipodozi, mamlaka kurejeshwa katika Mamlaka ya Vifaa Tiba *(TMDA)* na fedha zilizoidhinishwa na Bunge hususan fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limejidhihirisha katika fedha zilizoainishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ambapo hadi kufika mwishoni wa mwaka jana (Juni, 2024) fedha zilizotolewa ni kwa kiwango cha 52% tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS),* uchambuzi umebainisha kwamba, sehemu

kubwa ya maazimio imefanyiwa kazi. Hata hivyo, baadhi ya maazimio yanaendelea kufanyiwa kazi. Maazimio hayo ni pamoja na kutekelezwa kwa ufuatiliaji; mfano ni azimio kuhusu kutenga na kutoa fedha za ndani kwa wakati kwa ajili ya mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ambayo yanaendelea kutekelezwa na yale ambayo yameshatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara za utekelezaji wa miradi ya maendeleo Kamati ilitembelea miradi mitano na kwa uchambuzi imebaini ya kwamba, makusanyo ya maduhuli katika kipindi cha nusu ya mwaka (Julai, 2024 – Desemba, 2024) hali ya makusanyo ya maduhuli ni ya wastani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hsadi Desemba, 2024 jumla ya shilingi 358,101,667,833.18 zilikusanywa, ambayo ni sawa na 47% ya malengo yaliyowekwa ya kiasi cha shilingi 756,866,060,248.00. Kielelezo namba moja kinaonesha mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kiasi cha shilingi bilioni 1.3837 kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika miradi ya maendeleo hadi kufikia Desemba, 2024 jumla ya Shilingi 595,915,328,104.07 zilitolewa ambazo ni sawa na 45% ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha za ndani ya miradi ya maendeleo si ya kuridhisha sana kwani hadi Desemba, 2024 kimetolewa kiasi cha 41% tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Fungu 92 imebainika kuwa hali ya upatikanaji wa fedha ni ya kuridhisha. Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Miradi ya Maendeleo shilingi 17,808,981,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo shilingi 13,266,498,000 ambapo hadi kufikia Desemba

2024 zimepokelewa kiasi cha shilingi 10,506,372,717.52 ambayo ni sawa na 79% ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizotolewa umeoneshwa katika Kielelezo Na.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa ulitoa maelekezo kwa Kamati mbili za Bunge ambazo ni Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo kufanya kikao cha pamoja ili kushughulikia malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada ya afya katika vyuo vya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa maelekezo hayo ulitokana na maombi ya umoja wa vyuo binafsi vya afya na kati Tanzania *(Association of Private Health Colleges in Tanzania-(APHECOT)*yaliyowasilishwa kwako. Kwa mamlaka yako ulielekeza kifanyike kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo ili kushughulikia malalamiko ya *APHECOT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao hivyo yalibainika maazimio matatu ambayo yalitolewa kama ushauri kwa Serikali. Ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Wadau washirikishwe, wapewe elimu ya kutosha kuhusu vigezo vya udahili na kuanza kutumika katika Mwaka wa Masomo 2025/2026;

(ii) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(NACTVET)* litekeleze majukumu iliyopewa kwa mujibu wa Sheria, Sura namba 129 ikiwemo majukumu iliyoyakasimu kwa Wizara ya Afya; na

(iii) Kianzishwe chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya kati vya afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya, ili kuwezesha uendeshaji bora wa mafunzo ya kada ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(NACTVET);* lilitekeleza majukumu iliyopewa kwa mujibu wa Sheria namba 129 ikiwemo majukumu iliyoyakasimu kwa Wizara ya Afya. Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilieleza kuwa, jukumu la kuratibu utahini na mitihani linalotekelezwa na Wizara ya Afya, litekelezwe na taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo; Wizara ya Afya imeelekezwa kuanzisha mchakato wa kuzijengea uwezo taasisi za mafunzo zilizo chini yake, ili ziweze kuendesha mitihani yake yenyewe na namba tatu; uanzishwaji wa chombo mahususi cha usimamizi wa uendeshaji wa vyuo vya kati vya Afya vilivyo vya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya ilieleza kuwa imeanza mchakato wa kukianzisha chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya afya, ili kuimarisha usimamizi wa mafunzo kwenye vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa mpaka Oktoba, 2024 ni pamoja na kuandaa rasimu ya andiko na dhana ya uanzishwaji wa chombo hicho kwa ajili ya usimamizi wa mafunzo kwenye Vyuo vya Afya vya Serikali na kuundwa Kamati Maalum ya kukusanya maoni yatakayotekelezwa na uanzishwaji wa chombo hicho husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali izingatie na kutekeleza ushauri uliotolewa kwa ajili ya kuboresha suala zima la elimu ya kada ya afya katika vyuo vya kati kwani vyuo hivyo vimekuwa msaada mkubwa katika kuzalisha wataalam mbalimbali ambao husaidia kutoa huduma bora za afya kwa wananchi katika ngazi zote za huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utendaji wa Wizara na taasisi zake. Imefahamika kuwa *Medical Store Department (MSD)* imeweza kuongeza mapato kutoka shilingi bilioni 378.77 Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kufika kiasi cha fedha shilingi bilioni

553.114 kwa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 46%. Aidha, kumekuwa na ongezeko la ununuzi wa bidhaa za afya kutokana na uzalishaji wa ndani, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 22.1 zilinunuliwa ikiwa sawa na ongezeko la 57% kutoka kiasi cha shilingi bilioni 14.1 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio haya yameendana sambamba na kuanza uzalishaji wa mipira ya mikono *(examination gloves)* katika Kiwanda cha Mipira cha Idofi Njombe, ambapo jumla ya mipira milioni nne imezalishwa kuanzia Februari – Juni 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, *MSD* inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazosababisha kutokutekeleza majukumu yake ipasavyo. Moja ya changamoto kubwa ya *MSD* ni uhaba wa mtaji. Ikumbukwe kuwa suala la mtaji la Bohari Kuu ya Dawa limekuwa ni hitaji la muda mrefu kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uzalishaji, ununuzi, utunzaji wa bidhaa pamoja na usambazaji kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufika Mwezi Juni, 2024 kilitolewa kiasi cha shilingi bilioni 100 tu kama sehemu ya mtaji ambayo ni sawa na 17.8% ya mtaji wote. Kiasi ambacho kimetumika kuhudumia mitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya, kuimarisha mahusiano na wazabuni mbalimbali kwa kulipa madeni ambayo Bohari ilikuwa inadaiwa. Aidha, ni dhahiri kuwa kiasi kilichotolewa hakitoshi kutekeleza majukumu ya Bohari ya Dawa kwa ufanisi, kwani ni kiasi kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi. Kwa sasa Bohari ya Dawa bado inahitaji kiasi cha shilingi bilioni 461 kama sehemu ya mtaji ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF)*; Kamati imefuatilia hali ya Mfuko wa Bima ya Afya hadi kufika Juni 2024 na kubaini kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato kutoka shilingi bilioni 756 kufikia shilingi bilioni 756.48, ukilinganisha na

shilingi bilioni 696.72 zilizokusanywa katika *Financial Year* 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa usajili wa vituo vya matibabu; vimefika 10,004 nchini kote, ukilinganisha na vituo 9,186 mwaka 2022/2023. Vilevile, kuimarika kwa matumizi ya *TEMAHA* katika kutekeleza majukumu ya Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Uchakataji wa Madai *(Claims Management Information System)* umewezeshwa kuchakata madai na kupunguza ushiriki wa daktari *(automatic claims proceeding)* na hivyo kuondoa ushiriki wa kuchakata madai kwa *manual*. Licha ya mafanikio na kupiga hatua kadhaa za mafanikio katika kufanikisha malengo ya kuanzishwa kwake, lakini bado kuna changamoto mbalimbali zinazoathiri hali ya mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ni pamoja na kuwepo vitendo vya udanganyifu wa watumiaji wa kadi za Bima ya Afya, kuwepo kwa mwamko mdogo wa wananchi kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya kutokana na kutokutolewa kwa elimu kuhusu umuhimu wa huduma ya Bima ya Afya katika Taifa, na kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza *(Non-Communicable Diseases)* na gharama za matibabu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Kamati imebaini kuwa hatua mbalimbali zimefikiwa, ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa kanuni za Bima ya Afya zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali, Toleo Na. 809 la Mwaka 2024. Vilevile, kufunguliwa kwa akaunti ya Mfuko wa Kugharamia Wasio na Uwezo kwa ajili ya kuhifadhi fedha na kutambuliwa kwa idadi ya watu wasio na uwezo wanaohitaji kugharamiwa huduma za afya, ambapo kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, Tanzania Bara ina kaya 3,917,457 zisizo na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya kaya hizo zisizo na uwezo, kuna kaya 1,264,978 ambayo ni sawa na asilimia 32.3,

zimetambuliwa kama kaya zenye umaskini uliokithiri. Zinanufaika na huduma ya *TASAF (The Tanzania Social Action Fund)*, ambapo Serikali itaanza na kundi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa mfuko wa kugharamia watu wasio na uwezo kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote imebaini kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imebainisha vyanzo vya kugharamia kundi hilo la wananchi vinavyokadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 173.5. Hadi kufika Novemba 2024, kiwango kilichokusanywa na Serikali kwa ajili ya kugharamia watu wasio na uwezo ni shilingi bilioni 47.13 tu, sawa na 27%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya watoto wachanga nchini, Kamati imebaini kuwa, takribani 75% ya vifo vya watoto wachanga, vinatokana na watoto kuzaliwa kabla ya wakati (Njiti), changamoto ya upumuaji baada ya kuzaliwa na maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa, watoto wachanga 24 hufariki kwa kila vizazi katika vizazi hai 1,000. Hali hii inaashiria nchi bado hatujafanya vizuri sana katika eneo hili, hasa ikizingatiwa kwamba Malengo ya Dunia ya Mwaka 2030 *(Sustainable Development Goals – SDG's)* kiashiria *(target)* namba 3.2, ni kupunguza vifo vitokanavyo na watoto wachanga hadi kufika vifo 12 kwa vizazi 1000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matokeo hayo, kuna changamoto kadhaa zinazosababisha jamii kushindwa kupata huduma iliyopaswa na kushindwa kuondokana na tatizo hilo. Changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa gharama kubwa za huduma za afya ya akili pamoja na wananchi, kwani wananchi wengi wameshindwa kumudu gharama za matibabu. Hivyo kukosa huduma stahiki na kuwepo kwa uhaba wa rasilimali watu kama Madaktari Bingwa wa Afya ya Akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika uimarishaji wa huduma za Matibabu ya Kibingwa, na Ubingwa Bobezi,

zimeendelea kuimarishwa kwa kiwango kikubwa nchini, kwani zinatolewa na kupatikana katika Hospitali zote za Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi katika utendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS);* imebainika kuwa, utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI umeleta matokeo chanya, ikiwemo: kupungua kwa idadi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka maambukizi 61,281 mwaka 2020, hadi kufika maambukizi 60,000 mwaka 2023; kupungua kwa idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI, kutoka vifo 32,639 mwaka 2020, mpaka kufika vifo 25,000 mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada madhubuti zinahitajika katika mapambano dhidi ya UKIMWI, ikiwemo kutatua changamoto zilizobainika wakati wa utekelezaji wa mkakati huo. Aidha, utatuzi wa changamoto hizi utaleta matokeo chanya na ya moja kwa moja, ikiwa ni pamoja na kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, imebainika kuwa, kiwango kikubwa cha fedha za utekelezaji wa afua za UKIMWI, kama vile afua za tohara kwa wanaume, kinga, tiba na matunzo ya VVU, usambazaji wa kondomu na utoaji wa elimu kuhusu maambukizi ya VVU zimekuwa zikitolewa na wafadhili mbalimbali kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa mashirika yasiyo ya Kiserikali umekua na manufaa makubwa sana kwa jamii na nchi yetu kwa ujumla, ambapo nchi imepiga hatua kubwa katika kupunguza maambukizi ya UKIMWI na kufika 4.4%, kwa mujibu wa *Tanzania Health Impact Survey* ya mwaka 2022/2023, kutoka asilimia tano mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na mapendekezo, kwenye maoni na mapendekezo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kusimamia upatikanaji na utolewaji wa huduma za afya zenye ubora na usawa kwa jamii yote nchini kwa ujumla na kuifanya jamii kuwa na afya njema na ni hitaji na rasilimali za

thamani kwa kila mwananchi. Bila afya njema ni vigumu mtu kufanya kazi, kufurahia maisha na kufanikisha malengo yake, kwani afya njema huchangia moja kwa moja katika uwezo wa mtu wa kuzalisha mali, kuishi kwa furaha na kuwa na maisha yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto mbalimbali zilizobainika, ambazo utatuzi wake utasaidia kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya nchini. Kwa sababu hiyo, ninaomba kutoa mapendekezo ambayo Bunge lako Tukufu litayaazimia kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya tunaanza na kiwango kidogo cha utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo:

KWA KUWA, Fedha zilizoidhinishwa za miradi ya maendeleo zimetolewa kwa kiwango kidogo sana kwa 41%, tu hadi kufika Disemba 2024.

NA KWA KUWA, kiasi hicho kidogo cha fedha pasipo kuzingatia wakati, kitaathiri utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo iliyokusudiwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa wakati, ili miradi iliyokusudiwa ikamilike kwa muda uliokusudiwa na kuwanufaisha wananchi na Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, lishe duni:

KWA KUWA, nchi yetu inakabiliwa na changamoto kuu tatu za kilishe, ambazo ni utapiamlo wa lishe pungufu, utapiamlo wa upungufu wa madini na vitamini, pamoja na utapiamlo wa lishe ya kuzidi.

NA KWA KUWA, changamoto hii ya lishe inasababisha jamii yetu kuwa na afya isiyo bora, jambo linalochangia kuongezeka

kwa magonjwa yasiyoambukizwa yanayotokana na lishe pungufu na lishe ya kuzidi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

(1) Serikali itengeneze na itekeleze mpango wa Taifa wa lishe kwa haraka, ili kuboresha masuala ya lishe; *(Makofi)*

(2) Iongeze kasi ya kutoa elimu ya lishe kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na mitandao mbalimbali ya kijamii;

(3) Ifanye tafiti zitakazosaidia kutoa majibu ya kutatua changamoto ya udumavu; na

(4) Iongeze virutubisho kwenye vyakula vinavyotumika *(food fortification)* katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi. Mfano shuleni, gerezani, na kwenye vituo vya kulelea watoto yatima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa mtaji wa Bohari ya Dawa *(MSD)*:

KWA KUWA, Bohari Kuu ya Dawa kwa sasa inakabiliwa na uhaba wa mtaji wa shilingi bilioni 461.5;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari ya Dawa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itoe mtaji wa shilingi bilioni 461 kwa Bohari ya Dawa, kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za msingi ambazo ni uzalishaji, ununuzi, utunzaji, na usambazaji wa bidhaa za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya:

KWA KUWA, Kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kimetamka kuanzisha mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo.

NA KWA KUWA, jitihada kadhaa zimefanyika ikiwa ni pamoja na kubainisha vyanzo vya fedha vya mfuko huo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iwashirikishe wadau kutoka sekta binafsi katika kuchangia fedha za mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za uendeshaji wa Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF)*:

KWA KUWA, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* umekua ukikumbwa na changamoto kadhaa kama vile kupitwa wakati kwa Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF)*, Sura Na. 395, uwepo wa udanganyifu katika matumizi ya Bima ya Afya (ile kadi), na ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza na gharama za matibabu yake;

NA KWA KUWA, changamoto hizo husababisha athari hasi katika uendeshaji na usimamizi wa mfuko huo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(1) Ifanye marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya, Sura Na. 395, ili kuitambua Sekta Binafsi ya Afya ambayo ni mdau muhimu katika Sekta ya Afya;

(2) Iimarishe mifumo ya *TEHAMA* ili kulipa watoa huduma za afya kwa wakati;

(3) Kudhibiti udanganyifu wa matumizi ya bima ya afya; na

(4) Kutoa elimu ya jamii kuhusu umuhimu wa huduma ya bima ya afya na mtindo bora wa maisha, kwa lengo la kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa magonjwa ya UKIMWI, magonjwa ya ngono na homa ya ini:

KWA KUWA, jamii imekuwa ikikumbwa na kuathiriwa na ongezeko la maradhi kama UKIMWI, magonjwa ya ngono, na homa ya ini;

NA KWA KUWA, jitihada mbalimbali zimefanyika ikiwemo kuundwa kwa mpango jumuishi wa kudhibiti magonjwa haya ya pamoja, lakini bado hazijatosheleza, kwani jamii imekua ikiathirika kwa kiasi kikubwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mikakati ya kutenga fedha za ndani kwa ajili ya mapambano ya magonjwa ya ngono na homa ya ini. Iongeze kasi ya utoaji elimu kuhusu maambukizi ya magonjwa ya ngono na homa ya ini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa rasilimali watu:

KWA KUWA, Sekta ya Afya inakabiliwa na upungufu wa rasilimali watu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kiwango cha asilimia 55,

NA KWA KUWA, upungufu huo wa rasilimali watu umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa sana utoaji wa huduma za afya hapa nchini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kama ifuatavyo: -

(i) Serikali itoe kipaumbele cha ajira kwa sekta hii muhimu, ili huduma za Sekta ya Afya ziweze kupatikana kwa ngazi zote, kwa wakati na katika ubora unaostahili;

(ii) Iendelee kutoa ufadhili wa masomo kwa wataalamu wa afya, ili kupata mafunzo ikiwemo mafunzo ya kibingwa na Ubingwa Bobezi, katika vyuo vya ndani na nje ya nchi; na

(iii) Itoe kipaumbele cha ajira kwa wataalamu wanaojitolea kutoa huduma za afya katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini; Namba tatu, narudia; itoe kipaumbele cha ajira kwa wataalamu wanaojitolea kutoa huduma za afya katika vituo mbalimbali vya afya, na huduma za afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la matibabu ya afya ya akili:

KWA KUWA, kumekuwa na ongezeko kubwa la matibabu ya afya ya akili;

NA KWA KUWA, ongezeko hilo linasababisha jamii kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi na kupungua kwa uwezo wa kuzalisha mali, kushindwa kuishi kwa furaha, na kukosa maisha yenye tija;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, moja, Serikali iimarishe huduma za afya ya akili kwa kuhakikisha vituo vyote vya kutoa huduma za afya nchini vinawezeshwa kutoa angalau huduma za msingi za afya ya akili; na

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, ihakikishe elimu ya afya ya akili inatolewa kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vya watoto wachanga nchini:

KWA KUWA, takwimu za vifo vya watoto wachanga bado ziko juu, kwa kiwango cha vifo 24 kila mwezi kwa kila vizazi 1000;

NA KWA KUWA, jitihada mbalimbali zilizofanywa zimepunguza vifo hivyo, lakini bado hazijatosheleza.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, iongezwe wodi maalumu *(NICU – Neonatal Intensive Care Unit)* katika vituo vya kutolea afya nchini, kwa ajili ya huduma za watoto wachanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iongezwe vifaa tiba kwa ajili ya huduma za watoto wachanga, na waongezwe wataalam wa kuhudumia watoto wachanga kwenye vituo vyote vya afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Sheria ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa Chembechembe za Viungo vya Mwili wa Binadamu, na kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hiyo, kwa kulinda haki za binadamu, kuhakikisha usalama wa afya kwa wananchi na kuzuia biashara haramu za viungo vya mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa maambukizi ya VVU kwa vijana walio kati ya miaka 15 – 24:

KWA KUWA, matokeo ya utafiti wa viashiria vya UKIMWI Tanzania mwaka 2022/2023 yameonesha kuwa, ongezeko kubwa la VVU kwa kundi la vijana waishio na miaka 15 – 24;

NA KWA KUWA, ongezeko hilo linahatarisha afya za vijana wengi, na kufupisha ndoto zao kwa kupoteza maisha katika umri mdogo pale wanaposhindwa kuanza huduma za tiba na matunzo;

KWA HIYO BASI, Bunge liazimie kwamba, Serikali iongeze jitihada za ziada katika kutoa elimu kuhusu njia bora ya kujikinga na VVU kwa kundi hili;

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu, itoe elimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia huduma za tiba na matunzo kwa vijana wanaogundulika na maambukizi ya *HIV* na UKIMWI:

KWA KUWA, hali ndogo ya mwamko inachangia kuchelewa kufika sababu ya 95% ya kwanza;

NA KWA KUWA, inalenga watu wote wanaoishi na VVU kupima na kujua hali zao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupima ili kujua hali zao za maambukizi ya UKIMWI, kwani 95% ya sasa bado ipo chini kwa 82.7%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujumuishaji wa masuala ya UKIMWI kwenye taasisi za umma:

KWA KUWA, ujumuishaji wa masuala ya UKIMWI kwenye taasisi za umma unakabiliwa na changamoto kama vile ufinyu wa bajeti na ushirikiano usioridhisha;

NA KWA KUWA, changamoto hizo hufifisha jitihada za taasisi na sekta katika kudhibiti maambukizi ya UKIMWI;

KWA HIYO BASI, Bunge liazimie, lihakikishe kuwa taasisi na sekta zake zinatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza mkakati wa kudhibiti maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ihakikishe taasisi na sekta zake zinashirikiana kwa ukaribu na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, katika uratibu shughuli za udhibiti wa maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; ninapenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi, kwa namna unavyoliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, ninakushukuru kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa huzuni kubwa na majonzi makubwa, ninataka kunatoa pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu, kwa kuondokewa na mpendwa wetu aliyekuwa Makamu wa Kamati hii na Mkurugenzi wetu Mteule wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* Kanda ya Afrika, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, aliyefariki tarehe 27 Novemba 2024. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Afya, ninamshukuru sana

Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Naibu wake na Mheshimiwa Mhagama na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Mollel. Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ismail Rumatila na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Elias Magembe, pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati katika utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kwa ushirikiano mzuri ambao wamenipa kama Mwenyekiti wakati wote. Ninaomba majina yao yatambuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa hoja, ninaomba nilikumbushe Bunge hili Tukufu, tarehe ya leo ambayo ni tarehe 4, Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ninapenda Bunge letu waweze kulijua hili na waweze kuona kwamba kuna tukio gani muhimu linatokea nchini katika siku ya leo, ambalo limeweka *landmark* kwa dunia na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, anapokea tuzo ya *Bill Gates Foundation* ya kufanikisha kushusha vifo vya watoto kutoka vifo 556 mpaka kufikisha vifo 104. Rekodi hii Waheshimiwa Wabunge, rekodi hii ya Mheshimiwa Rais wetu haijawahi kutokea toka kipindi chochote cha kuanzishwa kwa Taifa letu. Kwa hiyo, ni imani yangu Wabunge wote mtaungana na watoa tuzo kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu na kumtia moyo kwa mafanikio haya makubwa yakushusha vifo vya watoto wadogo, kutoka 556

mpaka 504. Ninawapongeza sana watu wa *Bill Gates Foundation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya UKIMWI na likubali maoni na mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI KWA MWAKA 2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Mwezi Februari 2024 hadi Januari 2025. Kanuni hiyo imeweka sharti la lazima kwa kila Kamati kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake, kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Sehemu hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inayohusu utangulizi, inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati na njia zilizotumika na Kamati katika kutekeleza majukumu yake;

(ii) Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi, inatoa ufafanuzi kamili kuhusu shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto; na

(iii) Sehemu ya Tatu, inabainisha maoni ya jumla kuhusu matokeo ya uchambuzi na kutoa mapendekezo kwa ajili ya uamuzi wa Bunge. Aidha, sehemu hii inahitimisha taarifa na kutoa hoja ili Bunge liweze kupokea na kukubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo huu utaliwezesha Bunge lako kuona mtiririko wa Taarifa kwa mawanda yaliyokusudiwa na kubaini kiini cha mapendekezo yatakayotolewa na muktadha wake.

**1.3 Njia zilizotumika katika kutekeleza majukumu**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge naomba kutaja njia zilizotumika wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Njia hizo ni: -

(i) Kutafakari hali ya shughuli za Wizara na Taasisi zake na kuibua ajenda;

(ii) Kuomba Taarifa Maalumu za Utekelezaji wa shughuli za Wizara na Taasisi zake ili kuzichambua na kuzijadili;

(iii) Kufanya majadiliano na Wizara ili kupata undani wa hali halisi; na

(iv) Kufanya majumuisho ya masuala yaliyojitokeza ili kuwa na maoni ya jumla kuhusu masuala hayo na kuandaa mapendekezo.

**1.4 Madhumuni ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge. Madhumuni ya Taarifa hii ni kubainisha mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025. Lengo ni kuonesha mambo yanayohitaji kuboreshwa ili Bunge liyajadili na kuweza kuyatolea maamuzi kwa kuzingatia madaraka yake kwa mujibu wa **ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**1.5 Msingi wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa shughuli za Kamati unatokana na madaraka ya Bunge kwa mujibu wa ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inalitambua Bunge kuwa chombo chenye madaraka kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake vyote. Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba inaweka msingi wa Bunge kuunda Kamati za Bunge kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Vilevile, Kanuni ya 137 ya Kanuni za Bunge ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge imeanzisha Kamati za Kudumu za Bunge na kufafanua majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 5 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaainisha Kamati Kumi na Moja za Kudumu za Bunge katika kundi la Kamati za Kisekta. Miongoni mwa Kamati hizo, ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Majukumu ya jumla ya Kamati hizo yamebainishwa kwenye kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Majukumu hayo ni: -

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo Pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na

(iv) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (9) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia shughuli za: -

(i) Wizara ya Afya; na

(ii) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - (TACAIDS).

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inahusu shughuli za Kamati ya Kisekta na maudhui yake yanagusa Sekta ya Afya na mambo mtambuka yanayohusu masuala ya UKIMWI. Sehemu hii ya Taarifa inafafanua shughuli za Kamati na uchambuzi wa mambo yaliyobainika. Mambo hayo yanajenga msingi wa maoni na mapendekezo yanayohitaji uamuzi wa Bunge.

### 2.2 Ufafanuzi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati zililenga kubainisha iwapo utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara na Taasisi zake, unawezesha maisha bora kama ilivyokusudiwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025. Aidha, ili kukamilisha azma ya Bunge kuwa sauti na chombo halisi cha uwakilishi wa Wananchi; Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali kuhusu shughuli za umma katika sekta ya Afya zilizingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ufafanuzi wa shughuli hizo ni kama ifuatavyo: -

**2.2.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa spika**, Ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni moja ya shughuli muhimu za Kamati zinazofanikisha utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Shughuli hii hufanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge ambapo ilihusisha kubaini na kutambua miradi inayostahili kutembelewa. Jumla ya miradi mitano (5) ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka 2023/2024 na inayotekelezwa na Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) ilitembelewa na kukaguliwa katika Mkoa wa Mwanza, Geita na Singida.

**2.2.2 Kushughulikia Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hii ilihusu uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kazi hii ilifanyika tarehe 18 hadi 27 Machi, 2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotokana na shughuli ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na uchambuzi wa bajeti yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Ni matumaini ya Kamati kuwa, Serikali inaendelea kuzingatia maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa wakati huo ili kuboresha utendaji katika shughuli zake za kila siku.

**2.2.3 Kushughulikia malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada za Afya katika vyuo vya kati**

**Mheshimiwa Spika**, Itakumbukwa kuwa ulitoa maelekezo kwa Kamati mbili za Kudumu za Bunge ambazo ni Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo kufanya kikao cha pamoja ili kushughulikia malalamiko

dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada za Afya katika vyuo vya kati.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa maelekezo hayo ulitokana na maombi ya Umoja wa Vyuo Binafsi vya Afya vya Kati Tanzania, *[Association of Private Health Colleges in Tanzania-(APHECOT)]* yaliyowasilishwa kwako. Umoja huo kwa mara ya kwanza uliomba kibali chako ili viongozi wake wakutane na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Kwa busara zako, uliridhia Kamati iliyolengwa ikutane na *APHECOT* ambapo siku ya Ijumaa, tarehe 17 Mei, 2024 Kamati ilikutana na kuanza kulifanyia kazi suala la malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili katika vyuo vya kati vya Afya.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao hicho, *APHECOT* waliwasilisha malalamiko dhidi ya vigezo vipya vya udahili wa kada za Afya katika vyuo vya kati kwa kada ya Fiziotherapia, Famasia na Uuguzi na Ukunga ambavyo vilitarajiwa kuanza kutumika katika Mwaka wa masomo 2024/2025. Kwa kuzingatia wigo wa Wizara zinazohusika katika suala hilo, Kamati iliomba ridhaa yako ili kupata nafasi ya kukutana na Wizara ya Afya kwa pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kupata mtazamo wa Serikali kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mamlaka yako, ulielekeza kifanyike kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo ili kushughulikia malalamiko ya *APHECOT*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati mbili ulizozielekeza kukutana zilifanya kikao cha pamoja siku ya Jumatano, tarehe 5 Juni, 2024, Alhamis, tarehe 6 Juni, 2024 na Jumanne, tarehe 11 Juni, 2024. Katika vikao hivyo yaliibuka maazimio matatu ambayo yalitolewa kama ushauri kwa Serikali. Ushauri huo ni:-

(i) Wadau washirikishwe na wapewe elimu ya kutosha kuhusu vigezo vipya vya udahili kabla ya kuanza kutumika katika Mwaka mpya wa masomo 2025/2026;

(ii) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) litekeleze majukumu lililopewa kwa mujibu wa sheria sura namba 129 ikiwemo majukumu lililoyakasimu kwa Wizara ya Afya; na

(iii) Kuanzishwe chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya kati vya afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya ili kuwezesha uendeshaji bora wa mafunzo ya fani za kada ya afya.

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 18 Oktoba, 2024 Serikali iliwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati ikiwa ni sehemu ya maagizo yaliyotolewa ili yawasilishwe katika vikao vya Kamati vya mwezi Oktoba, 2024. Taarifa hiyo iligusia masuala yote yaliyoshauriwa na Kamati na kuonesha namna utekelezaji unavyoendelea. Utekelezaji huo ni kama ifuatavyo: -

(i) Uelimishaji na ushirikishwaji wa wadau kuhusu vigezo vipya vya udahili kabla ya Mwaka mpya wa masomo 2025/2026; Serikali kupitia Wizara ya Afya ilieleza kuwa itaandaa vikao vya wadau wa mitaala ya mafunzo kwa kila mtaala ili kupata maoni yao yatakayosaidia kufanya maboresho ya mitaala hiyo. Kwa kipindi cha Disemba, 2024 hadi Mei, 2025 wadau wataelimishwa kuhusu uandaaji wa mitaala na taratibu za kufuata iwapo mdau hajaridhika na maboresho yaliyofanyika kwenye mitaala. Aidha, Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Septemba, 2025 mitaala iliyohuishwa itasambazwa ili kuanza kutumika kwenye Mwaka wa masomo 2025/2026 utakaoanza mwezi Oktoba, 2025;

(ii) Kuhusu Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) litekeleze majukumu lililopewa kwa mujibu wa sheria sura namba 129 ikiwemo majukumu lililoyakasimu kwa Wizara ya Afya; Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilieleza kuwa jukumu la kuratibu utahini na mitihani linalotekelezwa na Wizara ya Afya, litekelezwe na taasisi husika za mafunzo na Wizara ya Afya imeelekezwa kuanzisha mchakato wa kuzijengea uwezo taasisi za mafunzo zilizo chini yake ili ziweze kuendesha mitihani yake zenyewe; na

(iii) Uanzishwaji wa chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya kati vya Afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya; Serikali kupitia Wizara ya Afya ilieleza kuwa imeanza mchakato wa kuanzisha chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya afya ili kuimarisha usimamizi wa mafunzo kwenye vyuo hivyo. Hatua iliyofikiwa mpaka mwezi Oktoba 2024 ni pamoja na kuandaa rasimu ya andiko dhana la uanzishwaji wa chombo cha usimamizi wa mafunzo kwenye vyuo vya Afya vya Serikali na kuundwa kamati maalumu ya kukusanya maoni yatakayowezesha uanzishwaji wa chombo hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali izingatie na kutekeleza ushauri uliotolewa kwa ajili ya kuboresha suala zima la elimu ya kada za Afya katika vyuo vya kati, kwani vyuo hivyo vimekua ni msaada mkubwa katika kuzalisha wataalam mbalimbali ambao husaidia kutoa huduma bora za Afya kwa wananchi katika ngazi zote za huduma za Afya nchini.

**2.2.5 Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai 2024 – Disemba, 2024**

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli hii ililenga kubainisha iwapo mwenendo wa utekelezaji wa bajeti unalingana na matarajio ya Bunge. Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai - Disemba 2024) kutoka Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

Mambo makuu katika Taarifa hizo yalihusu makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo la makusanyo pamoja na upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa. Uchambuzi wa mambo yaliyobainika unabainishwa katika Taarifa hii sambamba na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu matokeo ya uchambuzi huo.

**2.2.6 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utendaji**

**Mheshimiwa Spika,** Kupokea na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ni

mojawapo ya njia za kufuatilia shughuli za umma. Taarifa hizo, zilijadiliwa kwa kulinganishwa na msingi, madhumuni na majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake ili kuona hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kuboresha ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za utendaji ulilenga kuliwezesha Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali inavyostaili kuhusu Sekta ya Afya pamoja na mapambano dhidi ya UKIMWI. Lengo hilo linatimizwa kwa Kamati kuripoti Bungeni matokeo ya shughuli hizo kwa kubainisha masuala yaliyojitokeza, maoni na mapendekezo kuhusu mambo hayo chini ya Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

**2.3 Matokeo ya Shughuli za Kamati kuhusu Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyobainishwa katika Taarifa hii, lengo na utaratibu wa Kamati kuwasilisha Taarifa hii Bungeni ni kuliwezesha Bunge kupitisha mapendekezo yanayoweza kufanyiwa kazi wakati wa mchakato wa uandaaji wa bajeti na utekelezaji wa bajeti. Ili kufanikisha hilo, masuala yaliyojitokeza wakati wa shughuli za Kamati yanabainishwa kwa kila sekta. Kwa upande wa sekta ya Afya chini ya Wizara ya Afya, uchambuzi unabainisha mambo mbalimbali ikiwemo changamoto. Ufafanuzi wa matokeo hayo ya uchambuzi ni kama ifuatavyo: -

**2.3.1 Hali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zimeonesha kuwa, baadhi ya maazimio yametekelezwa na mengine yanaendelea kutekelezwa. Mfano wa maazimio yaliyoripotiwa kutekelezwa ni azimio kuhusu Serikali kutoa kipaumbele cha ajira kwenye Sekta ya Afya katika ngazi mbalimbali ili huduma ziweze kupatikana kwa wakati na katika ubora unaostahili na azimio kuhusu Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kuwezeshwa kisheria kwa kuwekewa Kanuni chini ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuipa mamlaka ya

kudhibiti utoaji wa huduma za Bima ya Afya nchini. Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji umeonesha kuwa, hadi kufikia mwezi Disemba, 2024 watumishi 13,193 waliajiriwa na Serikali. Aidha, Kifungu Na. 7 cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kimeipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) majukumu kwa lengo la kusimamia utoaji wa huduma za Bima ya Afya nchini na Kanuni namba 19 (1)(e) ya Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote inaipa TIRA mamlaka ya kudhibiti utoaji huduma za bima ya afya kupitia skimu za bima zilizosajiliwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa maazimio yanayoendelea kufanyiwa kazi ni pamoja na kuweka mikakati thabiti ya kushirikisha sekta binafsi *(Public Private Partinership - PPP)* na kurahisisha uwekezaji wa viwanda vya dawa pamoja na vifaa tiba nchini ili kukidhi soko la ndani na nje, Bohari kuu ya Dawa (MSD) kupewa mtaji, kufufua Kiwanda cha Dawa cha Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries)* na kuongeza uzalishaji katika Kiwanda cha Dawa cha Keko (*Keko Pharmaceutical Industries)* ambacho Serikali imewekeza kwa asilimia 70. Hivyo, Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge wakati wote ili kutoa mrejesho wa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji ulibainisha maazimio ambayo hayajatekelezwa kikamilifu. Mfano wa maazimio hayo ni pamoja na maazimio kuhusu udhibiti wa chakula na vipodozi kurejeshwa kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na fedha zilizoidhinishwa na Bunge hususan fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa wakati. Hili limejidhihirisha katika fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ambapo hadi kufika mwisho wa mwaka Juni, 2024 fedha zilitolewa kwa kiwango cha asilimia 52 tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Uchambuzi umebainisha kwamba, sehemu kubwa ya maazimio imefanyiwa kazi. Hata hivyo, baadhi ya maazimio yanaendelea kufanyiwa kazi. Maazimio hayo ni muhimu kutekelezwa na ufuatiliaji unapaswa kuendelea. Mfano wake ni pamoja na azimio kuhusu kutenga na kutoa fedha za

ndani kwa wakati kwa ajili ya mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI. Taarifa iliyowasilishwa ilionesha kuwa, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mpango wa uendelevu wa mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini *(HIV Response Sustainability Roadmap)* ili kupata rasilimali endelevu za ndani katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI bila kutegemea msaada kutoka kwa wafadhili.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile Taarifa ilifafanua zaidi kwamba, TACAIDS imefanya mapitio ya Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 na kuandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya UKIMWI ya mwaka 2001 Toleo la mwaka 2025 pamoja na Mkakati wa utekelezaji wa Sera husika. Hatua inayoendelea sasa ni kupata maoni ya wadau ambayo ni hatua muhimu ya wadau kushauri kuhusu mapendekezo yaliyotolewa kwenye Sera. Marekebisho ya Sera yamepangwa kukamilika katika mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulihakikishia Bunge kuwa, Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ambayo yanaendelea kutekelezwa na yale ambayo hayakutekelezwa.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ulifanyika ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa bajeti. Taarifa zilizowasilishwa zilibainisha masuala yafuatayo: -

#### (a) Mwelekeo wa Kukusanya Pungufu ya Lengo

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kwamba Makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai, 2024 hadi Disemba, 2024) ni ya wastani. Hadi mwezi Disemba 2024 jumla ya **Shilingi 358,101,667,833.18** zilikusanywa sawa na asilimia 47 ya lengo lililowekwa la kiasi cha **Shilingi 756,866,060,248.00**.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi umeonesha maeneo matatu ya makusanyo kwa Wizara ya Afya. Maeneo hayo ni Hospitali za

Rufaa za Mikoa, Makao Makuu ya Wizara na Taasisi, Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda. Aidha, imebainika kuwa Makao Makuu ya Wizara imekusanya kiwango cha juu ikilinganishwa na makusanyo kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kwenye Taasisi, Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba 1.

**KIELELEZO NA 1:** Mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli kutoka kwenye vyanzo vya Wizara ya Afya

| NA. | TAASISI | KIASI KILICHOKADIRIWA KUKUSANYWA (2024/2025) | KIASI KILICHOKUSANYWA (JULAI – DISEMBA, 2024) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Makao Makuu ya Wizara | 70,828,500,189.69 | 35,119,182,493.51 | 50 |
| 2. | Hospitali za Rufaa za Mikoa | 134,171,499,810.31 | 63,894,499,018.42 | 48 |
| 3. | Taasisi, Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda | 551,866,060,248.00 | 259,087,986,321 | 47 |
| | **JUMLA** | **756,866,060,248.00** | **358,101,667,833.18** | **47** |

***Chanzo;*** *Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai - Disemba, 2024)*

**(b) Upatikanaji wa kiasi kidogo cha fedha iliyoidhinishwa na Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Afya (Fungu 52) ilitengewa kiasi cha **Shilingi 1,311,837,466,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2024, jumla ya **Shilingi 595,915,328,104.07** zilipokelewa, sawa na asilimia 45 ya fedha zilizoidhinishwa kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba 2.

**KIELELEZO NA 2:** Ulingano wa Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizotolewa

| MATUMIZI | KIASI KILICHOIDHINISHWA 2024/2025 | KIASI KILICHOTOLEWA (JULAI – DISEMBA 2024) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 484,935,496,000.00 | 196,766,008,662.05 | 41 |
| Matumizi Mengineyo | 147,331,724,000.00 | 50,294,262,772.44 | 34 |
| Maendeleo Ndani | 416,258,609,000.00 | 171,996,259,387.21 | 41 |
| Maendeleo Nje | 263,311,637,000.00 | 176,858,797,282.37 | 67 |
| **JUMLA** | **1,311,837,466,000.00** | **595,915,328,104.07** | **45** |

***Chanzo;*** *Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai - Disemba, 2024)*

**Mheshimiwa Spika,** Imebainika kuwa, hali ya upatikanaji wa fedha za ndani zinazotolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo si ya kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Disemba 2024 fedha za ndani za maendeleo zilizotolewa ni asilimia 41 tu ya fedha zote zilizoidhinishwa. Hii inaonesha kuwa kiasi cha **Shilingi 171,996,259,387.21** ndicho kimetolewa kutoka katika kiasi cha **Shilingi 416,258,609,000.00** cha fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa kutoa fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo sio mzuri kwani hali hii inakwamisha utekelezaji wa miradi kwa wakati na kurudisha nyuma maendeleo ya sekta ya Afya. Aidha, kwa kiasi kikubwa imebainika kuwa baadhi ya miradi ya maendeleo inatekelezwa moja kwa moja kwa fedha kutoka nje ya nchi bila ya uwepo wa fedha za ndani. Hali hii inadhihirisha kuna utegemezi wa nchi katika kutekeleza miradi yake. Hivyo, ni muhimu Serikali ikatoa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya sekta ya Afya mapema ili miradi itekelezwe na kukamilika ndani ya muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Fungu 92), imebainika kuwa hali ya upatikananji wa fedha ni ya kuridhisha. Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 17,808,981,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,542,483,000.00** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 13,266,498,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Disemba 2024, fedha za Matumizi ya Kawaida zimepokelewa **Shilingi 2,048,884,916.00** sawa na **asilimia 45.** Aidha, fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo zimepokelewa **Shilingi 10,506,372,717.52** sawa na **asilimia 79** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizotolewa umeoneshwa katika kielelezo namba 3.

**KIELELEZO NA 3:** Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizotolewa (TACAIDS)

| MATUMIZI | KIASI KILICHOIDHINISHWA 2024/2025 | KIASI KILICHOTOLEWA (JULAI – DISEMBA 2024) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 1,817,358,000.00 | 862,022,166.00 | 47 |
| Matumizi Mengineyo | 2,725,125,000.00 | 1,186,862,750.00 | 44 |
| Maendeleo Ndani | 1,880,000,000.00 | 940,000,000.00 | 50 |
| Maendeleo Nje | 11,386,498,000.00 | 9,566,372,717.52 | 84 |
| **JUMLA** | **17,808,981,000.00** | **12,555,257,633.52** | **70** |

***Chanzo****; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS (Julai - Disemba, 2024)*

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya hali ya upatikanaji wa fedha kuwa inayoridhisha, lakini bado imebainika kuwa kwa kiasi kikubwa baadhi ya miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi. Hali hii inadhihirisha kwamba kuna utegemezi wa nchi katika kutekeleza miradi yake. Hivyo, ni muhimu Serikali kufikiri na kujipanga kuwa na fedha za ndani kwa wingi bila kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kudhibiti UKIMWI.

### 2.3.3 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji za Wizara ya Afya

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa za utendaji ulifanyika kwa kuoanisha hali ya utendaji na uendeshaji, matarajio ya wananchi, Ilani ya CCM, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano pamoja na Sera na Sheria. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha ifuatavyo: -

#### (a) Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu makuu ya Bohari Kuu ya Dawa ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Afya kwenda kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za Afya na vile vya binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya. Katika kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa kwa sasa MSD inatumia Mpango Mkakati wa Tatu wa Taasisi ambao ni wa miaka mitano (2021-2026).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa ya Utendaji wa Bohari ya Kuu ya Dawa hadi kufikia mwezi Juni, 2024, umebainisha masuala yafuatayo: -

(i) Kuongezeka kwa mapato kutoka **shilingi bilioni 378.77** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia kiasi cha **shilingi bilioni 553.114** kwa mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la **asilimia 46**;

(ii) Kuimarika kwa utimizaji wa mahitaji ya vituo vya kutolea huduma kutoka asilimia 75 mwaka wa fedha 2022/2023 na kufikia asilimia 86 kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Kuongeza ununuzi wa bidhaa za afya kutoka kwa wazalishaji wa ndani ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, bidhaa za afya zenye thamani ya **shilingi bilioni 22.1** zilinunuliwa ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 57 kutoka kiasi cha **shilingi bilioni 14.1** kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na

(iv) Kuanza uzalishaji wa mipira ya mikono *(examination gloves)* katika kiwanda cha mipira ya mikono cha Idofi Njombe, ambapo jumla ya mipira ya mikono **milioni 4** imezalishwa kuanzia mwezi Februari hadi Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio hayo yaliyotokana na utendaji mzuri, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Bohari Kuu ya Dawa zinazosababisha kutokutekeleza majukumu yake ipasavyo. Moja ya changamoto kubwa ni uhaba wa Mtaji. Ikumbukwe kuwa suala la mtaji kwa Bohari Kuu ya Dawa limekua ni hitaji la muda mrefu ambapo mtaji wa kiasi cha **shilingi bilioni 561.5** umekua ukihitajika kwa ajili ya kuwezesha shughuli za Uzalishaji, Ununuzi na Utunzaji wa bidhaa za afya kwa ufanisi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2024 kilitolewa kiasi cha **shilingi bilioni 100** tu kama sehemu ya mtaji sawa na asilimia 17.8 ya mtaji wote. Kiasi hicho kimetumika kuhudumia mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya na kuimarisha mahusiano na wazabuni mbalimbali kwa kulipa madeni ambayo Bohari inadaiwa. Ni dhahiri kuwa kiasi kilichotolewa hakitoshi kutekeleza majukumu ya Bohari kwa ufanisi kwani ni kiasi kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi. Kwa sasa Bohari ya Dawa bado inahitaji kiasi cha **shilingi bilioni 461.5** kama sehemu ya mtaji ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**(b) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria, Sura 395 kutokana na mabadiliko katika Sekta ya Afya yaliyoanza miaka ya 1990. Lengo la mfuko huu lilikua kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watumishi wa umma na wategemezi wao. Katika kutekeleza Sera ya Afya ya mwaka 2007, marekebisho mbalimbali yamefanyika katika mfuko huo kwa lengo la kupanua wigo wa wanachama na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ambapo kwa sasa mfuko unahudumia makundi mbalimbali ya wanachama ikiwemo Waheshimiwa Wabunge, Kampuni Binafsi, Wanafunzi, Wajasiriamali, Wakulima, Watoto na watu binafsi

kupitia utaratibu wa vifurushi vya bima ya afya ambavyo wananchi wanajiunga kwa hiari.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefuatilia hali ya Mfuko wa Bima ya Afya hadi kufikia Juni, 2024 na kubaini mambo yafuatayo: -

(i) Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato kufikia **shilingi bilioni 756.48** ukilinganisha na **shilingi bilioni 696.72** zilizokusanywa mwaka 2022/2023;

(ii) Kuongezeka kwa usajili wa vituo vya matibabu kufikia **10,004** nchini kote ukilinganisha na vituo **9,186** mwaka 2022/2023; na

(iii) Kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu ya mfuko, mfano mfumo wa uchakataji wa madai, *[Claims Management Information System (CMIS)]* umewezeshwa kuchakata madai na kupunguza ushiriki wa daktari *(automatic claims processing)*.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya mfuko kupiga hatua kadhaa katika kufanikisha malengo ya kuanzishwa kwake lakini bado kuna changamoto mbalimbali zinazoathiri hali ya mfuko. Changamoto hizo ni: -

(i) Kuwepo kwa vitendo vya udanganyifu wa matumizi ya kadi ya Bima ya Afya;

(ii) Kuwepo kwa mwamko mdogo wa wananchi kujiunga na huduma ya Bima ya Afya kutokana na kutokutolewa kwa elimu kuhusu umuhimu wa huduma ya Bima ya Afya; na

(iii) Kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza *(Non-Communicable Diseases)* na gharama za matibabu yake.

**(c) Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 1 Novemba, 2023 Bunge lako tukufu lilitunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisaini kuwa Sheria rasmi mnamo tarehe 19 Novemba, 2023. Sheria hiyo, ilitangazwa rasmi katika gazeti la Serikali Toleo Namba 48 la tarehe 1 Desemba, 2023 kuwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Namba 13 ya Mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kufuatilia utekelezaji wa Sheria hiyo, imebainika hatua zilizofikiwa ni pamoja na: -

(i) Kuandaliwa kwa Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote, zilizotangazwa kupitia gazeti la Serikali Toleo Namba 809 la mwaka 2024;

(ii) Kufunguliwa kwa akaunti za mfuko wa kugharamia wasio na uwezo kwa ajili ya kuhifadhi fedha; na

(iii) Kutambuliwa kwa idadi ya watu wasio na uwezo wanaohitaji kugharamiwa huduma za Afya, ambapo kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, Tanzania Bara ina kaya **3,917,457** zisizo na uwezo. Kati ya kaya hizo zisizo na uwezo, kuna kaya **1,264,978** sawa na asilimia 32.3 zimetambuliwa kama kaya zenye umasikini uliokithiri na zinanufaika na huduma za TASAF *(The Tanzania Social Action Fund)* ambapo Serikali itaanza na kundi hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu mwenendo wa mfuko wa kugharamia watu wasio na uwezo kupitia sheria ya bima ya afya kwa wote, imebainika kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imebainisha vyanzo mahsusi vya kugharamia kundi hilo la wananchi vinavyokadiriwa kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni 173.5**. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2024, kiwango kilichokusanywa ni **shilingi bilioni 47.13** tu sawa na asilimia 27.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kukamilika kwa baadhi ya hatua kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Sheria ya

Bima ya Afya kwa wote, bado kuna hatua nyingine zinaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha utekelezaji huo unafanyika bila kikwazo. Hatua hizo ni pamoja na ukamilishaji wa miongozo ya usimamizi na udhibiti wa bima ya afya; ukamilishaji wa kitita cha mafao cha bima ya afya kwa wote; utoaji wa elimu kwa umma kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya kwa kuyafikia makundi mbalimbali katika jamii; na kuendelea na mazungumzo na wadau mbalimbali kwa lengo la ukusanyaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia kundi la watu wasio na uwezo.

**(d) Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCoP)**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango huu jumuishi wa kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini *(National AIDS, Sexually Transmitted Diseases (STI's) and Hepatitis Control Program - NASHCoP)* umetokana na kuhuishwa kwa uliokua Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI ulioanzishwa mwaka 1998. Lengo la huu mpango ni kuongeza wigo kwa kutoa huduma changamano kwa magonjwa haya matatu na kwa watu wote hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kuwa jukumu kuu la mpango ni kutoa miongozo ya kitaalamu katika kudhibiti Virusi vya UKIMWI (VVU), Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini pamoja na kuhakikisha huduma zinazotolewa zinazingatia miongozo ya kuzuia maambukizi mapya na kutoa huduma za tiba zenye ubora kwa wenye maambukizi. Katika kutekeleza jukumu hilo kuna malengo mbalimbali yaliyowekwa ambayo ni pamoja na kupunguza maambukizi mapya ya VVU, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto; kuimarisha huduma za uzuiaji, uchunguzi na upimaji wa VVU, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini; kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini; kupambana na vikwazo na kukosekana kwa usawa katika utoaji wa huduma za VVU, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini; na kuimarisha mifumo ya afya iliyo endelevu na stahimilivu katika utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya Serikali kuchukua hatua mbalimbali kupambana na moja ya janga la kitaifa ambalo ni maradhi, kwa kuanzisha mpango jumuishi wa kudhibiti magonjwa haya matatu kwa wakati mmoja. Bado kuna changamoto ambazo zinahitaji utatuzi wa muda mfupi na muda mrefu ikiwa ni pamoja na ukosefu wa elimu kuhusu magonjwa hayo matatu na ufinyu wa bajeti ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa afua za kudhibiti magonjwa haya matatu.

**(e) Mikakati na Mipango ya kuimarisha lishe nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango jumuishi wa pili wa Kitaifa wa Lishe *(National Multisectoral Nutrition Action Plan - NMNP) 2021/22 – 2025/26* umeendelea kutekelezwa ambapo kupitia mpango huo Serikali imetekeleza afua za lishe zilizothibitishwa kuwa na matokeo makubwa ili kukabiliana na matatizo ya utapiamlo wa lishe duni *(under-nutrition)* na lishe ya kuzidi *(Obesity)*.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa afua za lishe zenye matokeo makubwa ni pamoja na kutoa matone ya Vitamin A na dawa za minyoo ya tumbo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano; kutoa vidonge vya madini chuma na foliki; kutibu utapiamlo mkali; unyonyeshaji na ulishaji sahihi wa watoto; kutoa elimu ya lishe kwa jamii na kuimarisha mpango wa kuongeza virutubishi kwenye vyakula. Aidha, ipo mikakati mbalimbali iliyopangwa kutekelezwa na inayotekelezwa ili kuimarisha lishe nchini ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa mpango wa Taifa wa lishe; kutoa elimu ya chakula na lishe kwa vijana balehe; kuhuisha sera ya chakula na lishe; kampeni ya mtu ni afya; na mpango jumuishi wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na matatizo makuu matatu ya kilishe ambayo ni utapiamlo wa lishe pungufu, utapiamlo wa upungufu wa madini na vitamini pamoja na utapiamlo wa lishe ya kuzidi. Ni muhimu kwa Serikali kuweka nguvu na msisitizo zaidi katika afua zinazoonekana kuleta matokeo chanya na makubwa kwa jamii ili kuwa na jamii yenye

afya bora, isiyo na magonjwa yanayotokana na lishe duni na kuandaa kizazi chenye afya bora.

**(f) Hali ya vifo vya watoto wachanga nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa tafsiri ya kitaalamu watoto wachanga ni watoto waliozaliwa hai, wenye umri wa siku 0 hadi 28 toka kuzaliwa. Imebainika kuwa takribani asilimia 75 ya vifo vya watoto wachanga hutokea ndani ya siku 7 baada ya kuzaliwa na sababu kuu ya vifo hivyo ni kuzaliwa kabla ya wakati, changamoto ya upumuaji baada ya kuzaliwa na maambukizi.

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu zinaonesha kuwa watoto wachanga 24 hufariki kwa kila vizazi hai 1000, hali hii inaashiria nchi kutofanya vizuri katika eneo hili hasa ikizingatiwa kwamba malengo ya dunia ya mwaka 2030 *(Sustainable Development Goals-SDG's)* kiashiria *(target)* namba 3.2 ni kupunguza vifo vya watoto wachanga hadi chini ya vifo 12 kwa kila vizazi hai 1000.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya jitihada mbalimbali kufanyika katika kuhakikisha vifo vya watoto wachanga vinapungua ili kufikia malengo ya kidunia ifikapo mwaka 2030, lakini bado vifo hivyo ni tatizo kubwa kwa jamii yetu kutokana na changamoto kadhaa zinazofifisha jitihada za kupunguza vifo hivyo ikiwemo uhaba wa vyumba maalum vya kulaza watoto wenye changamoto, upungufu wa vifaa tiba na uhaba wa wataalam wa kuhudumia watoto wachanga. Hivyo ni muhimu kwa Serikali kuendeleza jitihada zitakazosaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto zinazojitokeza kwa ajili ya kufikia malengo ya kidunia.

**(g) Huduma za Afya ya Akili**

**Mheshimiwa Spika,** Huduma za afya ya akili hapa nchini zinatolewa kwa kuzingatia Sera, Miongozo na Sheria mbalimbali. Uratibu wa huduma hizi hufanyika kwa kufuata ngazi za usimamizi wa huduma za Afya ambapo Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili - Mirembe ndiyo imepewa hadhi ya kitaifa kama hospitali ya juu

kabisa ya rufaa katika utoaji na usimamizi wa huduma za afya ya akili nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekua na ongezeko la matatizo ya afya ya akili nchini, hii ni kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizofanyika ikiwemo tafiti ya hali ya viashiria hatarishi vya Magonjwa yasiyoambukiza uliofanyika mwaka 2023 *(STEPS Survey, 2023)* na kujumuisha hali ya afya ya akili. Imebainika kuwa asilimia 20.6 ya watu wazima miaka 18 hadi 69 walikuwa na dalili za ugonjwa wa sonona, kati yao wanaume ni asilimia 17.6 na wanawake ni asilimia 23.3. Tafiti hiyo pia inaonesha kuwa asilimia 11.4 ya watu wenye dalili za ugonjwa wa sonona wapo kwenye tiba na asilimia 12.9 wanapatiwa huduma za kisaikolojia. Aidha, asilimia 13.8 ya watu wote waliohojiwa katika tafiti hiyo walikuwa na hali ya kutaka kujiua ambapo asilimia 18.2 walikuwa wanawake na asilimia 8.0 walikuwa wanaume. Kutokana na Taarifa hizi za kitafiti inaashiria ukubwa wa tatizo na mahitaji yaliyopo katika jamii yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutatua matatizo ya afya ya akili na kuhakikisha jamii inakua salama, kumekua na mikakati mbalimbali ambayo imekua ikitekelezwa na imeleta matokeo chanya na ya moja kwa moja kwa jamii. Matokeo hayo ni kama vile kuongeza upatikanaji wa huduma kupitia ujenzi na ukarabati wa majengo ya kliniki za methadone; kuongezeka kwa idadi ya watalaam wa afya ya akili; kuimarika kwa uratibu wa huduma za afya ya akili kupitia kuundwa kwa bodi ya taifa ya afya ya akili; na kuimarika kwa huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia wakati wa majanga/maafa.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na matokeo hayo, bado kuna changamoto kadhaa zinazosababisha jamii kushindwa kupata huduma inavyopaswa na kushindwa kuondokana na tatizo hilo. Changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa gharama kubwa za huduma za afya ya akili kwa taasisi na wananchi kwani wananchi wengi wameshindwa kumudu gharama za matibabu hivyo kukosa huduma stahiki; na kuwepo kwa uhaba wa rasilimali watu kama madaktari bingwa wa afya ya akili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye jamii yoyote na nchi kwa ujumla, kuwa na afya njema ya akili ni hitaji na ni rasilimali ya thamani sana kwa kila mwananchi. Bila afya njema ya akili ni vigumu mtu kufanya kazi, kufurahia maisha na kufanikisha malengo yake kwani afya njema huchangia moja kwa moja katika uwezo wa mtu wa kuzalisha mali, kuishi kwa furaha, na kuwa na maisha yenye tija. Hivyo, mikakati madhubuti na ya upesi inahitajika kama sehemu ya njia za kutatua tatizo la afya ya akili kwenye jamii.

**(h) Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango huu ulianzishwa mahususi mwaka 1990 kwa ajili ya kuratibu na kusimamia shughuli za udhibiti wa Malaria nchini ili kuweza kufikia malengo ya kutokomeza Malaria ifikapo mwaka 2030. Kwa sasa Serikali ipo katika utekelezaji wa mpango mkakati wa Malaria wa sita wa mwaka 2021 hadi 2025, ambao umelenga kupunguza kiwango cha maambukizi ya Malaria kutoka asilimia 7.5 mwaka 2017 hadi kufikia kiwango cha chini ya asilimia 3.5 ifikapo mwaka 2025 na hatimae kutokomeza ugonjwa huo nchini ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika,** Mafanikio mbalimbali yaliyotokana na mapambano dhidi ya Malaria yamechochewa na kuwepo kwa mpango wa kudhibiti Malaria nchini. Mafanikio yaliyobainika ni kama ifuatavyo: -

(i) Kupungua kwa maambukizi ya Malaria kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 8.1 mwaka 2023; na

(ii) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na Malaria kutoka vifo 6,311 mwaka 2015 hadi kufikia vifo 1,954 mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo yaliyotokana na utekelezaji wa mpango, Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo ni: -

(i) Upungufu wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa afua muhimu za Malaria, ikiwemo afua ya utumiaji wa viua viluwiluwi *(biolarviciding)* na upuliziaji wa dawa za kuua wadudu ndani ya nyumba *(indoor residual spraying)*;

(ii) Ukosefu wa elimu ya kutosha kwa jamii kuhusu njia za udhibiti wa Malaria; na

(iii) Matishio ya kibaiolojia kama vile usugu wa vimelea vya malaria dhidi ya dawa na usugu wa mbu dhidi ya viuatilifu aina ya pareto.

**Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu kwa Serikali kuendelea na jitihada mbalimbali zenye matokeo chanya katika kudhibiti Malaria ili kuweza kufikia malengo ya dunia ya kutokomeza Malaria ifikapo mwaka 2030.

**(i) Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kutekeleza majukumu yake, ilifanikiwa kutembelea na kukagua utendaji kazi wa baadhi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa. Hospitali zilizotembelewa ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Chato, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa – Bugando, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kati – Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, Hospitali ya Rufaa ya Amana – Dar es Salaam, Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo (MOI) na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

**Mheshimiwa Spika,** Imebainika kuwa kazi kubwa imefanyika na inaendelea kufanyika hasa katika uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu ya kutolea huduma kama vile ujenzi wa majengo na usimikaji wa mifumo ya TEHAMA; na upatikanaji wa vifaa tiba

vya kisasa vya kibingwa na ubingwa bobezi. Hali hiyo huchangia kupatikana na kutolewa kwa huduma bora za afya zinazowanufaisha wananchi. Aidha, kumekua na watanzania wenye moyo wa upendo na wazalendo kwa nchi yao wanaojitoa kuisaidia jamii kwa kukamilisha baadhi ya miundombinu ya huduma za afya kwa fedha zao binafsi kama ujenzi wa jengo la huduma za Saratani katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha kutoka kwa Spanish Tiles Limited and Karibu Camps Limited na ujenzi wa jengo la kituo cha damu salama na vifaa vyake, wodi maalumu ya kisasa (V.I.P), wodi ya kisasa ya watoto wachanga yenye vitanda 60, jengo la kisasa la wagonjwa mahututi (ICU) lenye vitanda 8 na jengo la karakana ya viungo bandia pamoja na vifaa vyake katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa kutoka kwa Asas Group of Companies Limited.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya jitihada mbalimbali zinazofanyika kuboresha huduma za afya kwenye Hospitali hizo, lakini bado kuna changamoto kadhaa zinazosababisha huduma kutokutolewa kwa kiwango kinachotakiwa. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na: -

(i) Uhaba wa watumishi;

(ii) Uhaba wa majengo kwa ajili ya kutolea huduma; na

(iii) Ufinyu wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Hali hii inahitaji jitihada madhubuti ambazo zitatatua moja kwa moja changamoto hizo ili kuzidi kuimarisha zaidi huduma zinazotolewa katika Hospitali za Rufaa nchini.

**(j) Uimarishaji wa huduma za Matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi**

**Mheshimiwa Spika**, Huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi zimeendelea kuimarishwa kwa kiwango kikubwa

nchini, kwani zimekua zikitolewa na kupatikana katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali maalumu na Hospitali ya Taifa. Miongoni mwa huduma hizo ni pamoja na uanzishaji wa huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu zinazolenga kusaidia na kuokoa maisha ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Uanzishaji wa huduma hii unawarahisisishia wananchi wenye mahitaji kupata huduma ndani ya nchi ambapo gharama si kubwa ukilinganisha na nje ya nchi kama ilivyokuwa awali. Aidha, upatikanaji wake utachangia kuongeza mapato ndani ya nchi kwa kuwa gharama za matibabu ambazo zingelipwa nje ya nchi sasa zitabaki ndani ya nchi. Vilevile, uanzishwaji wa huduma hii unachochea tiba utalii ambapo watu kutoka nchi nyingine hutembelea nchini kwa lengo la kupata matibabu jambo linalochangia kukua kwa tiba utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia umuhimu na faida za utoaji wa huduma hizi nchini, ni muhimu sasa Serikali iweke mazingira mazuri ya utoaji na upatikanaji wa huduma hii kwa kuhakikisha kunakuwepo na Sheria zinazosimamia utoaji wa huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu zitakazozingatia usalama na maadili ya kibinadamu.

### 2.3.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za utendaji ulifanyika kwa kuoanisha hali ya utendaji na uendeshaji wa shughuli za Tume kwa upande mmoja na matarajio ya wananchi, Ilani ya CCM, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Sera na Sheria kwa upande mwingine. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha masuala yaliyojitokeza kama ifuatavyo: -

#### (a) Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania 2021/22 – 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** Katika kudhibiti UKIMWI, kumekua na utekelezaji wa Mikakati mbalimbali ambayo huratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). Kwa sasa unatekelezwa Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI ambao uliandaliwa kuwezesha utekelezaji wa mwitikio shirikishi wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI nchini. Mkakati huo umekua na malengo mbalimbali ikiwemo kupunguza idadi ya maambukizi mapya kutoka 61,281 mwaka 2021 hadi kufikia maambukizi 15,000 mwaka 2026; kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto hadi kufikia chini ya asilimia 5 mwaka 2026 kutoka asilimia 7.9 mwaka 2021; kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na UKIMWI kutoka vifo 32,639 mwaka 2021 hadi vifo 17,913 mwaka 2026; kutokomeza unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) ifikapo mwaka 2026; na kufikia shabaha za kimataifa za asilimia 95-95-95 zinazohusu kupima na kutibu ifikapo mwaka 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Tangu kuanza kutekelezwa kwa Mkakati huo ambao umetekelezwa kwa miaka minne mpaka sasa, imebainika kuwepo kwa matokeo chanya kwa jamii ambayo ni: -

(i) Kupungua kwa idadi ya maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU) kutoka maambukizi 61,281 mwaka 2020 hadi maambukizi 60,000 mwaka 2023;

(ii) Kupungua kwa idadi ya vifo vitokanavyo na UKIMWI kutoka vifo 32,639 mwaka 2020 hadi vifo 25,000 mwaka 2023;

(iii) Kupungua kwa kiwango cha ubaguzi na unyanyapaa utokanao na VVU kutokana na elimu ambayo imeendelea kutolewa kwa jamii na wadau mbalimbali;

(iv) Kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kutoka asilimia 7.9 mwaka 2020 hadi asilimia 7.0 mwaka 2023; na

(v) Kufikia shabaha ya pili kwa asilimia 98 kati ya shabaha tatu za kimataifa za asilimia 95-95-95, ambapo shabaha ya pili

inahusu waliotambua hali zao kuwa kwenye huduma ya tiba na matunzo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika safari yoyote yenye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto, hii ni kwa nukuu ya methali isemayo ***"hakuna mashaka yasiyo na mtihani"***. Changamoto kadhaa zimebainika katika utekelezaji wa mkakati huo, ambazo ni: -

(i) Kuongezeka kwa maambukizi ya VVU kwa makundi maalumu na maeneo yenye vichocheo zaidi vya maambukizi wakiwemo wachimbaji wa madini, wavuvi, waendesha pikipiki (bodaboda), madereva wa magari ya masafa marefu, wajidunga, vijana walio kati ya miaka 15 - 24;

(ii) Kuwepo kwa mwamko mdogo wa watu kujitokeza kupima na kujua hali zao za maambukizi hali inayochangia kuchelewa kufikia shabaha ya asilimia 95 ya kwanza; na

(iii) Kuwepo kwa visa vya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

**Mheshimiwa Spika,** Jitihada madhubuti zinahitajika katika mapambano dhidi ya UKIMWI ikiwemo za kutatua changamoto zilizobainika wakati wa utekelezaji wa mkakati huo. Aidha, utatuzi wa changamoto hizo utaleta matokeo chanya na ya moja moja ikiwa ni pamoja na kuutokomeza UKIMWI nchini ifikapo mwaka 2030.

**(b) Utekelezaji wa afua za Virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI kutoka kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali**

**Mheshimiwa Spika,** Udhibiti wa maambukizi ya VVU na UKIMWI umekua ukifanyika kwa ushirikiano baina ya Serikali na taasisi/mashirika yasiyo ya kiserikali. Kumekua na mikakati mbalimbali inayounganisha mipango kazi ya wadau wa VVU na UKIMWI ili kuchangia katika kufikia malengo yaliyowekwa Kitaifa. Mikakati hiyo ni zana inayotumiwa na Serikali na wadau wa

maendeleo katika kufuatilia utekelezaji wa mwitikio wa VVU na UKIMWI kwa mujibu wa sera na sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Imebainika kuwa kwa kiwango kikubwa fedha za utekelezaji wa afua za Virusi vya UKIMWI kama vile afua ya tohara kwa wanaume, kinga, tiba na matunzo ya VVU, usambazaji wa kondomu na utoaji wa elimu kuhusu maambukizi ya VVU zimekua zikitolewa na wafadhili mbalimbali kutoka nje ya nchi. Wafadhilli haoni pamoja na Serikali ya watu wa Marekani kupitia Mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na UKIMWI *(PEPFAR)*na Mfuko wa Dunia wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria *(GFATM)*. PEPFAR imekua ikitoa fedha za kutekeleza afua hizo kupitia mashirika yasiyo ya kiserikali na wakala *(Agencies)*ambazo ni *Centre for Disease Control (CDC),* Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa *(USAID), Department of Defence (DOD)*. Miongoni mwa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotekeleza afua za VVU na UKIMWI nchini ni pamoja na *Management and Development for Health (MDH); The Henry Jackson Foundation Medical Research International (HJFMRI); International Centre for Aids Care and Treatment Programs (ICAP); Tanzania Health Promotion Support (THPS); Elizabeth Glaser Paediatric AIDS Foundation (EGPAF); na Family Health International (FHI360)*.

**Mheshimiwa Spika,** Mashirika hayo yanatekeleza afua za VVU na UKIMWI kwa kuzingatia Mkakati wa Tano wa Kudhibiti UKIMWI nchini pamoja na Mkakati wa ushirikishaji mashirika yasiyo ya kiserikali katika mwitikio wa kitaifa wa UKIMWI (*NGO Engagement Strategy for National HIV Response)*. Ushiriki wa mashirika yasiyo ya kiserikali umekua na manufaa makubwa sana kwa jamii na nchi kwa ujumla ambapo nchi imepiga hatua kubwa katika kupunguza maambukizi ya UKIMWI kufikia asilimia 4.4 kwa mujibu wa *Tanzania Health Impact Survey (THIS)* 2022-2023 kutoka asilimia 5.0 mwaka 2016-2017, lengo likiwa ni kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika,** Ni dhahiri kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali ikiwemo yale yenye asili ya Tanzania yanatekeleza afua

za VVU na UKIMWI kwa kutegemea fedha za wafadhili, hali hii sio nzuri kwa wadau hao na nchi kwa ujumla kwani inasababisha utegemezi uliokithiri. Aidha, utegemezi huo unaliweka Taifa katika sintofahamu ikiwa wafadhili wataacha kutoa fedha hizo na hivyo Taifa kukosa uhakika wa fedha za mapambano endelevu dhidi ya VVU na UKIMWI.

**(c) Ujumuishaji wa Masuala ya UKIMWI *(mainstreaming)* kwenye Taasisi na Sekta za Umma**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 88(g) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, 2020 – 2025 kinasema kuhusu kuhuisha na kujumuisha masuala ya UKIMWI *(mainstreaming)* kwenye taasisi na sekta zote ambazo zina mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI, zikiwemo sekta ya ujenzi, uchukuzi, uvuvi na madini. Katika kufuatilia namna Serikali inatekeleza suala la ujumuishaji wa masuala ya UKIMWI kwenye Taasisi na Sekta za Umma, imebainika kuwa kuna hatua mbalimbali zimekua zikichukuliwa kwenye Sekta ya Uvuvi, Madini, Viwanda na kwenye jeshi la Magereza ambazo zimekuwa chachu katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la kujumuisha masuala ya UKIMWI kwenye taasisi na sekta za umma ni kuimarisha juhudi za kudhibiti UKIMWI kwa kuunganisha nguvu za sekta mbalimbali. Licha ya kujumuisha masuala ya UKIMWI katika Taasisi na Sekta za Umma, bado kuna changamoto za kitaasisi na kisekta zinazojitokeza katika udhibiti wa UKIMWI zinazosababisha malengo kutofikiwa kikamilifu. Miongoni mwa changamoto hizo ni ufinyu wa bajeti katika utekelezaji wa mkakati wa kudhibiti maambukizi ya VVU, Kifua Kikuu na Magonjwa yasiyoambukiza; ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu maambukizi ya VVU hasa kwa jamii za wavuvi, uhaba wa watumishi wa afya katika jeshi la magereza na ushirikiano usioridhisha kati ya sekta na Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania ambao ndio waratibu wa shughuli za udhibiti wa maambukizi ya VVU na UKIMWI nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufikia malengo ya kidunia ya kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030, zinahitajika jitihada

madhubuti kwa kila sekta kushiriki mapambano dhidi ya UKIMWI. Hivyo ni rai ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inasimamia vyema taasisi na sekta zake ziweze kushiriki kikamilifu ili kupata nguvu ya pamoja kama Taifa katika udhibiti wa janga hilo.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO**

**3.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Maoni na Mapendekezo ya Taarifa hii yamezingatia nyenzo muhimu ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi 2020 – 2025, Mpango Mkakati wa 5 wa Sekta ya Afya, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2021/22 – 2025/26 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (lengo namba 3).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kusimamia upatikanaji na utolewaji wa huduma za Afya zenye ubora na usawa kwani kwenye jamii yoyote na nchi kwa ujumla, kuwa na afya njema ni hitaji na ni rasilimali ya thamani kwa kila mwananchi. Bila afya njema ni vigumu mtu kufanya kazi, kufurahia maisha na kufanikisha malengo yake kwani afya njema huchangia moja kwa moja katika uwezo wa mtu wa kuzalisha mali, kuishi kwa furaha, na kuwa na maisha yenye tija. Hata hivyo, katika safari yoyote yenye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto, hii ni kwa nukuu ya methali *isemayo* ***"hakuna mashaka yasiyo na mtihani"***. Zipo changamoto mbalimbali zilizobainika ambazo utatuzi wake utasaidia kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya nchini. Kwa sababu hiyo, naomba kutoa mapendekezo ambayo Bunge lako Tukufu litayaazimia kwa ajili ya utekelezaji.

### 3.2 Wizara ya Afya

#### 3.2.1 Kiwango kidogo cha utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo

**KWA KUWA**, Fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimetolewa kwa kiwango kidogo cha asilimia 41 tu hadi kufika mwezi Disemba, 2024,

**NA KWA KUWA**, Kiasi hicho kidogo cha fedha pasipokuzingatia wakati kitaathiri utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo iliyokusudiwa,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa wakati ili miradi iliyokusudiwa ikamilike katika muda uliokusudiwa na kuwanufaisha wananchi.

#### 3.2.2 Lishe Duni

**KWA KUWA**, Nchi yetu inakabiliwa na changamoto kuu tatu za kilishe ambayo ni utapiamlo wa lishe pungufu, utapiamlo wa upungufu wa madini na vitamini pamoja na utapiamlo wa lishe ya kuzidi,

**NA KWA KUWA**, Changamoto hii ya kilishe inasababisha jamii yetu kuwa na afya isiyo bora, jambo linalochangia kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza yanayotokana na lishe pungufu na lishe ya kuzidi,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali –

(i) Itengeneze na itekeleze Mpango wa Taifa wa lishe kwa haraka ili kuboresha masuala ya lishe;

(ii) Iongeze kasi ya kutoa elimu ya lishe kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na mitandao mbalimbali ya kijamii;

(iii) Ifanye tafiti zitakazosaidia kutoa majibu ya kutatua changamoto ya udumavu; na

(iv) Iongeze virutubisho kwenye vyakula vinavyotumika katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi. Mfano Shuleni, Gerezani na kwenye vituo vya kulelea watoto yatima.

**3.2.3 Uhaba wa Mtaji kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD)**

**KWA KUWA**, Bohari Kuu ya Dawa kwa sasa inakabiliwa na uhaba wa mtaji wa **Shilingi bilioni 461.5**,

**NA KWA KUWA**, Kukosekana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali itoe mtaji wa **Shilingi bilioni 461.5** kwa Bohari kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za msingi ambazo ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Afya.

**3.2.4 Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote**

**KWA KUWA**, Kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa wote kimetamka kuanzisha mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo,

**NA KWA KUWA**, Jitihada kadhaa zimefanyika ikiwa ni pamoja na kubainisha vyanzo vya fedha za mfuko huo,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali iwashirikishe wadau kutoka sekta binafsi katika kuchangia fedha za mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo.

**3.2.5 Changamoto za Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**KWA KUWA,** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umekua ukikumbwa na changamoto kadhaa kama vile –

(i) Kupitwa wakati kwa sheria ya Mfuko (NHIF), Sura Namba 395;

(ii) Uwepo wa udanganyifu katika matumizi ya bima ya afya; na

(iii) Ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza na gharama za matibabu yake.

**NA KWA KUWA**, Changamoto hizo husababisha athari hasi katika uendeshaji na usimamizi wa mfuko huo,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali -

(i) Ifanye marekebisho ya Sheria ya NHIF, Sura Namba 395 ili kuitambua Sekta binafsi ya Afya ambayo ni mdau muhimu wa afya;

(ii) Iimarishe mifumo ya TEHAMA ili kulipa watoa huduma za afya kwa wakati na kudhibiti udanganyifu wa matumizi ya bima ya afya; na

(iii) kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa huduma ya bima ya afya na mtindo bora wa maisha kwa lengo la kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

**3.2.6 Udhibiti wa UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa Ya Ini**

**KWA KUWA**, Jamii imekua ikikumbwa na kuathiriwa na ongezeko la maradhi kama UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini,

**NA KWA KUWA**, Jitihada mbalimbali zimefanyika ikiwemo kuundwa kwa mpango jumuishi wa kudhibiti magonjwa hayo kwa

pamoja lakini bado hazijatosheleza kwani jamii imekua ikiathirika kwa kiasi kikubwa,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali –

(i) Iweke mikakati ya kutenga fedha za ndani kwa ajili ya mapambano ya Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini; na

(ii) Iongeze kasi ya utoaji wa elimu kuhusu maambukizi ya Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini.

**3.2.7 Upungufu wa Rasilimali Watu**

**KWA KUWA**, Sekta ya Afya inakabiliwa na upungufu wa rasilimali watu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kiwango cha **asilimia 55**,

**NA KWA KUWA**, Upungufu huo wa rasilimali watu umekuwa ukiathiri utoaji wa huduma bora za afya nchini,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali –

(i) Itoe kipaumbele cha ajira kwenye Sekta hii muhimu ili huduma za afya ziweze kupatikana katika ngazi zote kwa wakati na katika ubora unaostahili;

(ii) Iendelee kutoa ufadhili wa masomo kwa wataalam wa afya ili kupata mafunzo ikiwemo mafunzo ya kibingwa na ubingwa bobezi katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi; na

(iii) Itoe kipaumbele cha ajira kwa wataalam wanaojitolea kutoa huduma za afya katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini.

**3.2.8 Ongezeko la Matatizo ya Afya ya Akili**

**KWA KUWA**, Kumekuwa na ongezeko kubwa la matatizo ya afya ya akili nchini,

**NA KWA KUWA**, Ongezeko hilo linasababisha jamii kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi, kupungua kwa uwezo wa kuzalisha mali, kushindwa kuishi kwa furaha na kukosa maisha yenye tija,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali –

(i) Iimarishe huduma za afya ya akili kwa kuhakikisha vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini vinawezeshwa kutoa angalau huduma za msingi za afya ya akili;

(ii) Ihakikishe elimu ya afya ya akili inatolewa kwa jamii; na

(iii) Iongeze watalaam wa kutoa huduma za afya ya akili.

**3.2.9 Kurejesha Jukumu la Udhibiti wa Chakula na Vipodozi kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**KWA KUWA**, Udhibiti wa Chakula na Vipodozi ulihamishiwa katika Shirika la Viwango Tanzania - TBS kupitia marekebisho ya Sheria Sura Namba 219,

**NA KWA KUWA**, Chakula, Dawa na Vipodozi vinauhusiano mkubwa hivyo, kupelekwa kwa jukumu hilo chini ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambayo ni Taasisi isiyohusiana na masuala ya afya hivyo kunaondoa dhana ya udhibiti unaozingatia athari za kiafya,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali irejeshe kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)udhibiti wa chakula na vipodozi kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwani bidhaa za chakula na vipodozi zinahusiana moja kwa moja na afya ya jamii.

**3.2.10 Vifo vya watoto wachanga nchini**

**KWA KUWA**, Takwimu za vifo vya watoto wachanga bado zipo juu kwa kiwango cha vifo 24 kwa kila vizazi hai 1000,

**NA KWA KUWA**, Jitihada mbalimbali zilizofanyika kupunguza vifo hivyo bado hazijatosheleza,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali: -

(i) Iongeze wodi maalum *(NICU - Neonatal Intensive Care Unit)* katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya huduma za watoto wachanga;

(ii) Iongeze vifaa tiba kwa ajili ya huduma za watoto wachanga; na

(iii) Iongeze wataalam wa kuhudumia watoto wachanga.

**3.2.11 Maambukizi ya Ugonjwa wa Malaria**

**KWA KUWA**, Maambukizi ya Ugonjwa wa Malaria bado yapo juu sana kwa kiwango cha asilimia 8.1,

**NA KWA KUWA**, Maambukizi hayo yamekua yakisababisha athari mbalimbali ikiwemo vifo kwani kwa takwimu za mwaka 2023 imeonekana kulikuwa na vifo 1,954 vitokanavyo na Malaria,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali –

(i) Itoe elimu kwa jamii kuhusu njia sahihi za udhibiti wa Ugonjwa wa Malaria; na

(ii) Itenge fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa afua muhimu za udhibiti wa Ugonjwa wa Malaria ikiwemo afua ya matumizi ya viuadudu na viua viluwiluwi.

**3.2.12 Kukosekana kwa Sheria ya kusimamia huduma ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa Chembechembe na Viungo vya Mwili wa Binadamu**

**KWA KUWA**, Huduma za uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu hazina sheria rasmi,

**NA KWA KUWA**, Kufanyika kwa huduma hizo bila uwepo wa sheria rasmi kunaweza kusababbisha athari hasi kwa jamii ikiwa ni pamoja na kukiukwa kwa haki za binadamu na kuibuka kwa biashara haramu ya viungo vya binadamu,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Sheria ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu ili kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hiyo kwa kulinda haki za binadamu, kuhakikisha usalama wa afya kwa wananchi na kuzuia biashara haramu ya viungo vya mwili wa binadamu.

**3.3 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

**3.3.1 Utegemezi wa fedha za wafadhili katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI**

**KWA KUWA**, Kiwango kikubwa cha utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI nchini hutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi,

**NA KWA KUWA**, Ufadhili huo ukifikia ukomo unaweza kusababisha kwa kiasi kikubwa nchi kupunguza kasi ya kupambana na janga hilo kwa kukosa fedha za kutosha,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali itekeleze kikamilifu mpango wa uendelevu wa mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini *(HIV Response Sustainability Roadmap)* ili kupata rasilimali endelevu za ndani katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI bila kutegemea msaada kutoka kwa wafadhili.

**3.3.2 Kuongezeka kwa Maambukizi ya VVU kwa Vijana Walio Kati ya Miaka 15 – 24**

**KWA KUWA**, Matokeo ya utafiti wa viashiria vya UKIMWI Tanzania (THIS - 2022/2023) yameonesha kuna ongezeko kubwa la maambukizi ya VVU kwa kundi la vijana walio kati ya miaka 15 - 24,

**NA KWA KUWA**, Ongezeko hilo linahatarisha afya za vijana wengi na kufupisha ndoto zao kwa kupoteza maisha katika umri mdogo pale wanaposhindwa kuanza huduma za tiba na matunzo,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali –

(i) Iongeze jitihada zaidi katika kutoa elimu kuhusu njia bora za kujikinga na maambukizi ya VVU kwa kuyafikia makundi maalum kama vile vijana; na

(ii) Itoe elimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia huduma za tiba na matunzo kwa vijana wanaogundulika kuwa na maambukizi.

**3.3.3 Mwamko mdogo wa jamii kujitokeza kupima na kujua hali ya maambukizi**

**KWA KUWA**, Kumekua na mwamko mdogo kwa wana jamii kujitokeza kupima na kujua hali zao, hasa kwa jamii zilizopo kwenye mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI kama vile jamii za wavuvi na migodi,

**NA KWA KUWA**, Hali ya mwamko mdogo inachangia kuchelewa kufikia shabaha ya asilimia 95 ya kwanza, inayolenga watu wote wanaoishi na VVU kupima na kujua hali zao za maambukizi,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupima ili kujua hali zao za maambukizi kwani asilimia 95 ya kwanza bado ipo chini kwa asilimia 82.7.

**3.3.4 Ujumuishaji wa Masuala ya UKIMWI *(mainstreaming)* kwenye Taasisi na Sekta za Umma**

**KWA KUWA**, Ujumuishaji wa masuala ya UKIMWI kwenye taasisi na sekta za umma unakabiliwa na changamoto kama vile–

(i) Ufinyu wa bajeti katika utekelezaji wa mkakati wa kudhibiti maambukizi ya VVU na UKIMWI; na

(ii) Ushirikiano usioridhisha kati ya taasisi na sekta za umma pamoja na Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania ambao ndio waratibu wa shughuli za udhibiti wa maambukizi ya VVU na UKIMWI nchini.

**NA KWA KUWA**, Changamoto hizo hufifisha jitihada za taasisi na sekta katika udhibiti wa maambukizi ya VVU na UKIMWI,

**KWA HIYO BASI**, **Bunge linaazimia kwamba**, Serikali –

(i) Ihakikishe taasisi na sekta zake zinatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza mkakati wa kudhibiti maambukizi ya VVU; na

(ii) Ihakikishe taasisi na sekta zake zinashirikiana kwa ukaribu na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika kuratibu shughuli za udhibiti wa maambukizi ya VVU.

**3.4 HITIMISHO**

**3.4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kukushukuru na kukupongeza kwa namna unavyoliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Aidha, nakushukuru kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa huzuni na majonzi makubwa natoa pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na

mpendwa wetu, aliyekua Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii na Mkurugenzi Mkuu Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile (Mb) aliyefariki tarehe 27 Novemba, 2024. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake, Amina.

**Mheshimiwa Spika**, Nawashukuru sana Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama (Mb) - Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Abdallah Shekalage, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ismail Rumatila na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Elias Magembe pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Bernadeta Kasabango Mushashu, Mb "
4. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb "
5. Mhe. Christopher Olonyokie Ole Sendeka, Mb "
6. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb "
7. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb "
8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb "
9. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb "
10. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb "
11. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb "
12. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb "
13. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb "
14. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb "
15. Mhe. Seif Salum Seif, Mb "

16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb "
17. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb "
18. Mhe. Agness Mathew Marwa, Mb "
19. Mhe. Jacquline Andrew Kainja, Mb "

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

**3.4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Elibariki Emmanuel Kingu, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU**
**YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**

04 Februari, 2025

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imetolewa, imeungwa mkono. Ahsante Mwenyekiti kwa taarifa sahihi na nzuri.

Sasa tunaanza kuchangia, ninamwita Mheshimiwa Jesca Jonathani, ajiandae Mheshimiwa Neema, ajiandae Mheshimiwa Festo.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote kwanza nitoe shukurani kwa Serikali katika taarifa yao nimeona hapa kwamba wametujengea bwalo la chakula katika Chuo chetu cha Ruaha, sisi Iringa tunakiita *CBTI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa inaendelea kusema kwamba litakamilika Mei, nipende tu kutoa taarifa kwamba limeshakamilika tayari na wanafunzi wetu wa Chuo kile cha Maendeleo ya Jamii wanakwenda *field*. Kwa hiyo, watakaporudi mwezi Aprili wataanza rasmi kutumia, ninawapongeza sana kwa hilo lakini pia niwashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa chuo kile sasa kinachukua wanafunzi wengi, bado tuna tatizo na changamoto kubwa sana ya usafiri. Kwa hiyo, Wizara mnaweza mkaona namna ambavyo mnaweza mkatusaidia na kusema ukweli nimshukuru sana Mkuu wa Chuo kwa sababu amefanya kazi kubwa ya kusimamia lile bwalo kisasa kabisa na niwapongeze walimu wote wa Chuo chetu kile cha Ruaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya niipongeze pia Kamati kwa mchango wao wa mwisho kuona umuhimu wa elimu ya afya ya akili na kusisitiza Serikali ichukue hatua madhubuti kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa afya ya akili nchini, ninawashukuru sana. Pamoja na pongezi bado kuna taarifa maendeleo ya jamii na nilichangia kwenye Bunge lililopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna shida ya kupeleka fedha za mikopo kwa wafanyabiashara wadogowadogo ambazo zilikuwa zimetengwa karibu shilingi bilioni 22.9, lakini pia kuna fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya machinga shilingi bilioni 18.8. Kwa masikitiko makubwa sana tulichangia kwa uchungu kwamba fedha hizi ziende kwa wale wafanyabiashara wadogo zikawasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo makubwa sana Serikali imefanya na hapa kuna vitu vikubwa sana Kamati

zimesoma inabidi vifanyike. Bado tunaendelea kufanya *extension* kubwa sana kwenye masuala ya afya na tunaendelea kulalamika kila siku kwamba tunatakiwa tuongeze vifaatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda mbali sana katika maazimio ambayo ametoka kusoma Mwenyekiti wa Kamati, moja ya maazimio wametoa kwa ajili ya maambukizi makubwa ya VVU kwa vijana wetu wa miaka 15 mpaka 24 maazimio yao wanasema tutoe elimu ya kutosha kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa tuna matatizo makubwa matatu kwenye utapiamlo, kuzidi sana au kupungua sana. Zaidi ya kutoa elimu, Bunge lako Tukufu linaona kuna umuhimu wa kuwezesha jamii na ndio maana tukapendekeza hapa Serikali ichukue *initiatives* kuhakikisha kwamba tunapeleka mikopo kwa vijana wetu ili wapate kazi za kufanya, kwa sababu tunapoongelea utapiamlo pamoja na kwamba tutaongelea kwa Watoto, lakini ule mwingine hata sisi watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana unaambiwa hata ukiwa tu na kitambi ni utapiamlo, umekula umezidisha au ukipunguza chakula na yenyewe pia ni utapiamlo. Leo hii vijana wetu walio wengi au tulio wengi tunakula chakula kilichopo, hatuli chakula kwa mahitaji ya mwili unaotaka, lakini hii yote ndiyo inapelekea utapiamlo. Hii inasababishwa na hali ya uchumi kuwa duni au umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongea hapa kuhusu watoto wachanga, watoto wachanga wanaopokuwa katika mazingira ya uchanga tunategemea wazazi au mama awe naye karibu mtoto mchanga. Mtoto anapokuwa kwenye *level* ya *primary school* mpaka sekondari *O' level* tunategemea atakuwepo chini ya uangalizi wa wazazi, lakini anapotoka hapo anapokuwa nje kwenye *society* anategemea sisi jamii nyingine na Serikali iingie kwa kina kuhakikisha tunawaangalia hawa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana wengi wapo mitaani wamejiajiri ndiyo tunasema ni machinga, ndiyo tunasema

wafanyabiashara wadogo na walio wengi ni wa kiume. Wale wengi walio wa kike tunashukuru Serikali imeonesha namna ambavyo wamefanya uwezeshaji wa uchumi kwa wanawake na mpango walionao kuendelea kuwawezesha wanawake. Hizi fedha shilingi bilioni 18 ni kitu gani kwenda kuwawezesha vijana wetu ili watupunguzie utapiamlo kwenye hii nchi. Shilingi bilioni 22 ni kitu gani twende tukawawezeshe vijana wetu ili tuendelee kuwa na kizazi bora kwenye hii nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana sasa hivi siyo tu wanakula kilichopo, wameamua tu kunywa pombe kujizima *data*. Tuna vijana wanakunywa pombe mpaka unajiuliza niongee na nitoe wito kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Serikali ina dhamana ya kuwalea watoto hawa, hebu tuangalie hizi pombe tunazoruhusu na hapa ninafikiri ni suala mtambuka, Wizara nyingi zinaingia: ipo Viwanda na Biashara, ninajua kuna vijana na kutakuwa na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, awakusanye wenzake wakae waone namna gani wana-*rescue* hili kundi la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akiwa amelewa atakumbukaje hata ukimwelimisha kwamba anatakiwa atumie zana hizi kufanya mapenzi asipate maambukizi. Leo hii kuna vipombe vinanywewa mpaka *alcohol* 40, 30 watoto wanakunywa. Nimekwenda kwenye ziara siku moja, ninafanya mkutano nikapata kero kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama hata wale wengine wanaouza pombe vilabuni nao wamekuwa wakemia, kwenye zile pombe kuna vitu wanaongeza. Sisi wengine tumekuwa tulikuwa tunaona bibi zetu, babu zetu wanakunywa ulanzi mpaka wanafariki hawajawahi kupata matatizo ya figo, hawajawahi ungua maini, hawajawahi ungua nini maisha yanaendelea, lakini vijana wa leo umri huo huo wa miaka 15 mpaka 24 akinywa pombe tu mfululizo miezi miwili ameshakufa, ameungua ukimwangalia haeleweki akili imekufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuone Wizara wana taratibu gani pamoja na kutoa elimu. Naomba niongeze azimio lingine, azimio lingine liwe ni pamoja na kupambana na vile vitu vyote vinavyochochea kufanya ngono zembe ikiwepo ulevi uliokithiri. Tusitoe tu elimu ili kuwakinga hawa; lakini pamoja na kupambana na vitu kama hivi ambavyo vinachochea ngono zembe lazima pia tupambane kuhakikisha kwamba tunawawezesha kiuchumi watoke huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo unaleta hoja tu kwamba hizi shilingi bilioni 22 zilizotakiwa zipelekwe kwa wafanyabiashara wadogo wadogo hazikwenda eti kwa sababu taasisi inayotakiwa kukopesha haikutokea kwa muda, kwa hiyo fedha hazikupelekwa kweli? Serikali imekosa taasisi ya kwenda kukopesha vijana wetu kuwasaidia wapate hiyo mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 18 zimeombwa, kibali hakikuombwa sijui zimevuka mwaka. Hizo shilingi bilioni 22 ni kiasi gani cha hela ambacho tunashindwa kusema tutoe tu hata sadaka wala haifiki hata fungu la kumi la mapato ya nchi yetu kwa ajili ya ku-*rescue* vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayaongea haya leo ukienda huko mitaani kama Waheshimiwa Wabunge huwa tunahudhuria misiba na labda haijafanyika *analysis* sasa hivi vijana wetu wanafariki sana. Wana matatizo ya figo wengi, wana shida za kupumua (mapafu) wengi lakini cha msingi hapa vijana hawa uwezeshaji wao kiuchumi bado ni duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ni vijana ambao tumewekeza kwa kiasi kikubwa kuwajengea shule za kata, kujenga vyuo vikuu, kujenga vyuo vya kati, tumewajengea hizo hospitali wanazaliwa vizuri, wanakwenda hospitali za wilaya wanazaliwa vizuri, baada ya kutoka pale wanakwenda kuishia kwenye kitu kidogo tu pombe. Yaani dozi wanayopewa vijana hawa ya pombe haiendani na uzito wao. Anakwenda kutumia

*alcohol* 30 wakati yeye mwenyewe ukiangalia uzito wake 50, kilo 50, kilo 60 wana-*faint*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii yetu ni nani atakayeilinda kama siyo sisi viongozi tuliopewa dhama tukaamua kuingia? Sisi tutengeneze sheria na utaratibu. Sasa nimekwenda kwenye ziara wale akinamama wanaopika pombe na wanaouza pombe wanalalamika kwamba wanaojumua pombe hawawalipi, wale wajumua pombe ninawauliza, wanasema madamu walevi wenyewe ndiyo kama unavyowaona wamechoka, hawana kitu tunawakopesha tu hawatulipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hawa ndiyo akinamama waliokopa hela huko hazirudi kwenye Mfuko wa *WFP* sijui huko hazirudi na hawa huku wanakunywa wanajiua, baada ya kujiua wanataka mashine za *dialysis* kwenye kila kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ndio wanaokwenda kuzaa au wanaoa wanawapa ujauzito mabinti wale watoto wanazaliwa kutokana na masuala ya ulevi wanakwenda kuzaliwa kabla ya umri tunapata watoto njiti wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanza kuhangaika hapa na *surfactant* ya kuwasaidia watoto kwa gharama kubwa, lakini kumbe *solution* ilikuwa ni kuwa-*rescue* hawa wazazi ili mwendelezo wa hilo tatizo usiendelee tuwe tumejiokoa kwenye mambo mengine...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninawapongeza Kamati kwa hoja nzito ambazo wamezitoa na tunaomba maazimio yao yafanyiwe kazi. Ninaomba Wizara ikae iangalie suala la ulevi uliokithiri. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Neema, jiandae Mheshimiwa Festo Sanga, jiandae Mheshimiwa Kainja.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hii hoja ambayo imewasilishwa na Wenyeviti wa Kamati hapo mbele. Awali ya yote ningependa kutumia nafasi hii kuendelea kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna wanavyofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Kwenye Kamati tulijadili mambo mengi mengine yameweza kuingia katika taarifa lakini mambo mengine hayakuweza kuingia lakini niseme tu kuna baadhi ya mambo ningependa kuyaongelea kama sehemu ya kukazia au kutoa ushauri kwa Bunge letu ili mnapokuwa mnatoa maelekezo kwa Serikali yaweze kufanyiwa kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona katika taarifa suala la wastaafu kulazimika kupewa nyaraka zenye namba ya malipo kwa ajili ya kulipa madeni ya waajiri wao ili wapate mafao limeonekana na ni ukweli kwamba hata ningekuwa ni mimi kama hiyo ndiyo fursa ya kuweza kunifanya nipate mafao yangu ningeweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi maalum kwa Bunge lako Tukufu kuielekeza mifuko ambayo ilibainika watumishi wao walitoa namba za malipo kwa watumishi wastaafu wakaenda kulipa, zile fedha zirejeshwe. Pia, ningeomba Bunge lako Tukufu litusaidie kutoa maelekezo kwa Serikali iwe ni marufuku na mwiko kwa mtumishi yeyote kushindwa kulipwa mafao yake eti kwa sababu wao walishindwa kufuatilia michango yao kwa waajiri wao. Kwa hiyo, hilo nilitamani kama Bunge tuweze kulichukua na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujielekeza pia kwenye programu ya kukuza ujuzi nchini. Tunaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kufanya jitihada ya kuendelea kuwajengea vijana wetu ujuzi mbalimbali. Tulifanya ziara tuliwaona vijana, tuliwakuta ni vijana wenye furaha, lakini ilionekana kwamba

katika lengo la Serikali lilikuwa ni kuwafikia vijana 136 kwa mwaka. Mpaka sasa hivi Serikali inafikia vijana 12,000 tu ambao ni sawasawa na 8.82% tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina maombi kuwaelekeza Serikali kuwa na lengo na dhamira ya dhati, ya kuhakikisha wanafikia hili lengo la vijana 136,000 na kama haiwezekani basi angalau wafike 50%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na changamoto wakati wa mafunzo kwamba ule muda wanaopewa vijana, muda hautoshi kwa hiyo, kuna baadhi ya vitu unakuta hawafundishwi wanapokuwa kwenye hayo mafunzo na vyeti wakati mwingine unakuta hawapatiwi kwa sababu hawajafuzu ile *course* ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu lisaidie kuielekeza Serikali kwamba wanapokuwa wanatoa mafunzo haya wazingatie muda maalum wa yale mafunzo. Pia, watusaidie kuwapatia wale vijana vifaa ambavyo wataenda kuanzia kazi baada ya pale. Haina maana watu vijana wanapatiwa mafunzo, halafu baada ya hapo wanakuwa wanarudi nyumbani kukaa hawajapewa mkopo, hawajapewa vifaa na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, kumekuwepo na hizi programu mbalimbali kwenye Wizara tofauti za kukuza ujuzi kwa vijana. Mfano tunafahamu Kilimo wana programu ya *BBT,* lakini Wizara ya Mifugo pia ina namna inavyoendelea kukuza vipaji vya vijana, lakini tunaona kwenye Michezo, TAMISEMI wana programu ambazo zinasaidia kukuza ujuzi kwa vijana. Hakuna bodi ambayo imewekwa kwa ajili ya kuratibu hizi programu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kupitia Bunge lako hili Tukufu, Serikali iweze kuiwezesha hii Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye upande wa ajira, kazi, vijana na wenye ulemavu waweze kuwa na uratibu ili tuwe na namna nzuri ya kupata *data* za vijana ambao wajengewa uwezo. wasipokuwa na uratibu madhubuti

kwa ajili ya hawa vijana tutakuwa tunafanya kama marudio, kijana huyo huyo anaenda kujengewa uwezo huku, anaenda kujengewa uwezo huku kitu ambacho kinakuwa siyo kizuri kwa masilahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kwenye suala la mikopo, tunafahamu dhamira ya Serikali kuanzisha mifuko ya mikopo kwenye Wizara mbalimbali kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ilikuwa ni nia njema kabisa lakini kumekuwa na mtiririko au mwendelezo wa kupanga bajeti ambayo itatolewa kwenye hii mifuko ya mikopo, lakini haiendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kwenye hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii tunaona shilingi bilioni moja ilikuwa imetengwa, kwamba iwe inatolewa kila mwaka kwenye mfuko wa vijana, *the same applied* lakini hizi fedha haziendi *almost six years* mpaka saa hizi hawajapatiwa hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuta ile mifuko inadumaa haina fedha lakini na kwa ile fedha ambayo ipo ambayo inakuwa *revolved,* yaani ile fedha ambayo ilitolewa awali ambayo inatakiwa iwe *revolved* fedha nyingi zipo kwenye halmashauri hawarejeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba kupitia Bunge lako hili Tukufu kama sehemu ya Maazimio ya Bunge, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI azielekeze halmashauri zake kuhakikisha zinatoa hizo fedha kwenye hiyo mifuko yaani zirejeshwe hizo fedha badala ya fedha hizo za Wizara kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuongelea suala la benki ambazo zinaenda kwa wananchi kuwafungulia akaunti kwa lazima kwa kigezo kwamba watawapatia mikopo. Imekuwa ni changamoto, watu wanafunguliwa akaunti halafu katika kufunguliwa akaunti wanaahidiwa mikopo, mikopo hawapewi fedha zao za kufungulia akaunti zinaenda na wakati mwingine zinapotelea huko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kesi hii ambayo kwa kweli haituweki vizuri kwa wananchi wetu, Serikali yetu inaonekana ina watu wababaishaji ambao hawawezi ku-*control* hizi benki kuchukua hizo fedha kwa wananchi. Ninajaribu tu ku-*imagine* ukiongelea wananchi laki tano wakachangishwa shilingi 10,000 kufungua akaunti ni *almost* shilingi bilioni tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika hili pia ninataka kuomba Serikali ielekeze benki zote ambazo walienda kufungua akaunti kwa kigezo kwamba watatoa mikopo wapeleke fedha kwa wananchi. Mbaya zaidi wanatutumia wanasiasa tufanye hamasa kwa wananchi wetu kitu ambacho kinatuweka kwenye hali ngumu ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niweze kuchangia kwenye upande wa afya kidogo. Tumekuwa na utaratibu wa kwamba rufaa zote zinazotolewa kwenye nchi yetu uelekeo ni India. Ninatamani kufahamu kwamba, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha sasa tunaongeza nchi za kutoa rufaa, kama tutakuwa na wagonjwa ambao wamezidiwa? Hawezekani kila kesi ni India, kwa nini kusiwe na nchi nyingine mbadala, ambazo nazo tunaweza tukafanya nazo kazi kwa upande wa afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kupewa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Kainja na Mheshimiwa Maige.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Jambo la kwanza naomba niunge mkono hoja ya Kamati hii, hoja ambayo imekusudia kuboresha sana maeneo ya Sekta ya Afya. Jambo la pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa tuzo, ya kushusha vifo vya watoto kutoka 556 hadi 104, ambayo majira haya ya mchana, saa sita, anakabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzo ya *Bill Gate Goalkeepers Award* ni kitu kikubwa kwa Taifa letu. Kwa kweli, sisi tunaona kwa macho kuimarika kwa Sekta ya Afya nchini kumepunguza sana vifo vya watoto kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na Chama Cha Mapinduzi kwa sababu, hili lilikuwa ni mkakati wake wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia mambo mawili; la kwanza, ni kuhusu bima ya afya kwa wote, lakini nitachangia kuhusu *MSD.* Mwenyekiti wa Kamati amezungumza na nimpongeze Mheshimiwa Kingu kwa kusoma vizuri hotuba yake na tumemwelewa vizuri. Kama mdau ninapenda pia, kuipongeza Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bima ya afya kwanza nianze kwa kumpongeza Dkt. Irene Isaka, Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Bima ya Afya, *madam* huyu ambaye ni mchumi kwa kweli, tumeona mabadiliko kwenye ukusanyaji wa mapato wa mfuko huu. Ambapo unaona mapato sasa yamekuwa kutoka ukusanyaji wa shilingi bilioni 696 yameenda shilingi bilioni 756. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaleta tafsiri ya kwamba, watendaji na wasaidizi wa Mheshimiwa Rais ambao amekuwa akiwaamini kwenye nafasi zao wanafanya kazi vizuri sana. Lazima tumpongeze Dkt. Irene Isaka popote alipo, chapa kazi na sisi kama Wabunge tutakuunga mkono na tutaendelea kumuunga mkono kwa sababu, tunaona mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni akinamama wanaonesha kwamba, wanaweza wakiaminiwa na wameaminika kwa kweli, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kuboresha suala la bima ya afya, Kamati imezungumza suala la kuimarisha mifumo. Moja kati ya changamoto kubwa ambayo tunaipata ni mifumo

kutokusomana. Kitendo cha mifumo kutokusomana kunafanya mfuko uingie shoti au hasara kwenye mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* anaripoti anasema mwaka 2020 hadi mwaka 2022 Serikali au Mfuko wa Bima ulilipa shilingi bilioni 14 kinyume na utaratibu kutokana na kupewa taarifa *fake* kutokana na kwamba, mifumo ilikuwa haisomani kwenye vituo vya kutoa huduma kwenye eneo la bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Maazimio ya Kamati aliyoyasema kwamba, lazima mifumo ya afya isomane na naliunga mkono hilo kwa sababu, imekuwa ndiyo kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba, mifumo yote nchi hii ni lazima isomane, ili kuondoa upotevu wa mapato na kuondoa hasara ambazo zimekuwa zikijitokeza kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni muhimu sana kwa sababu, pia, tunaenda kwenye bima ya afya kwa wote, ili mfuko huu uwe imara. Ni lazima ukusanyaji wa mapato uwe imara, lakini ni lazima malipo yanayolipwa yawe ni malipo sahihi, siyo ya udanganyifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* amekuwa akiripoti mara kwa mara kwamba, unakuta bima ni ya mwanaume halafu inasomeka kule imetumika na mwanamke, ni kwa sababu ya kutokusomeka kwa mifumo. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali tuunge mkono jitihada za mifumo kusomana kwenye eneo la bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimpongeze Dkt. Irene Isaka kwamba, vituo vya kutolea huduma vimeongezeka kutoka 9,186 hadi 14,000. Hili ni jambo kubwa kwamba, tunaendelea kumsogelea Mtanzania, kwa ajili ya kuweza kumtolea na kumpatia huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili linastahili kujipongeza. Kwenye Bunge la Bajeti lililopita Mheshimiwa Dkt. Mwigulu

Nchemba na Waziri wa Afya, alisimama hapa akaainisha vyanzo vya kuweza ku-*support* Mfuko wa Bima ya Afya kwa watu wasiojiweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunakiri hapa, tunazungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wamekusanya zaidi ya shilingi bilioni 47, Bunge ni lazima tuipongeze Serikali kwa hatua hizi kwa sababu, wakati tunazungumza miezi sita iliyopita tulikuwa na shilingi sifuri, leo hii tunazungumza tuna shilingi bilioni 47 zimekusanywa, kwa ajili ya kuwezesha Mfuko wa Bima ya Afya kwa watu ambao hawajiwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwamba, Serikali ina nia, Serikali imekusudia kuhakikisha bima ya wote inawezekana Tanzania. Hili ni jambo la kujipongeza na Bunge ni lazima lijipongeze kwa sababu, jambo ambalo lilikuwa limelipitisha sasa linafanyika na limeanza kukusanya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kuimarisha Mfumo wa *Claims Management Information System* ni vyema Serikali ikalifanya hili jambo kwa uharaka sana kwa sababu, tusipofanya kwa uharaka bado tutakuwa na changamoto ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo kipo Makete na madai yanatakiwa yaende Dar es Salaam, kama mifumo haijasomana ni lazima tutaendelea kupata changamoto kwenye Mfuko wetu wa Bima ya Afya. Kwa hiyo, ninaiunga mkono Serikali na Kamati kwenye maazimio waliyotoa kwamba, kuhakikisha lazima bima yetu iweze kusomeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwenye jambo la *MSD*. Tunapozungumzia *MSD* tunazungumzia ununuzi, uzalishaji na utunzaji wa vifaa vya afya kwa maana ya dawa na vitu vingine ambavyo vinahusika na vifaa vya afya. *MSD* ya kwetu Serikali inahitaji mtaji wa karibu shilingi bilioni 561, kama sikosei, kwa ajili ya kufanikisha uzalishaji, ununuzi na utunzaji wa vifaa vya afya.

Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 100, tupongeze kwa jitihada hiyo ambayo ni sawasawa na 17.5%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuikumbushe Serikali, tunapoimarisha bima ya afya kwa wote ni lazima tuimarishe na mfuko wa upatikanaji wa dawa kwa maana ya bohari. Hivi vitu viwili vikiwa imara kwenye nchi Sekta ya Afya inakuwa salama na inakuwa ni ya kuaminika. Sasa ni muhimu sana Serikali tukachukua hii *initiative,* tunahitaji shilingi bilioni 456, ili tuweze kuuwezesha mfuko uwe *full funded* na uweze kuhudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayezungumza niseme wazi, ninatoka Mkoa wa Njombe ambako kimejengwa Kiwanda cha Kuzalisha *Gloves* na katika mahitaji makubwa ya hospitali ni *gloves (examination gloves)*. Mkoa wetu umejengwa hicho kiwanda na tayari kimeshazalisha *gloves* 4,000,000, hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni lazima tuipongeze Serikali yetu. Badala ya kuagiza *gloves* kutoka nje sasa *gloves* zinapatikana ndani ya nchi hii, kwa ajili ya ku-*support* huduma ya afya kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, ni lazima tumuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uwekezaji kwenye hii bohari, hizi fedha ambazo zinahitajika tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha iangalieni, bohari ikiwa imara dawa zikapatikana, ndivyo ambavyo bima ya afya kwa wote pia, itakuwa na tija kwa Watanzania, ambapo wakienda kwenye vituo vya afya watapata huduma na dawa kwa uhakika, hii inaweza ikawa imetu-*support.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla, waangalie Mfuko wa Bohari *(MSD)* uweze kupata fedha, kwa ajili ya uwekezaji. Mtaji unaohitajika ni shilingi bilioni 400 na pointi ni hela ambayo nadhani ipo ndani ya uwezo, shilingi bilioni 461 ipo ndani ya uwezo kabisa wa kui-*support* bohari hii iweze kuleta tija kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kabisa Mkurugenzi kwa sababu, pia na yeye ameongeza ukusanyaji wa mapato. Mkurugenzi wa bohari ameongeza ukusanyaji wa mapato kutoka shilingi bilioni 378.77 amefikia shilingi bilioni 553, siyo kiwango kidogo, siyo haba. Ni nini wanachokihitaji? Ni kwamba, tuwapatie fedha ya mtaji, ili iweze kufanya kazi ambayo imekusudiwa na Watanzania waweze kupata vifaa tiba kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niipongeze Serikali yangu kwa utekelezaji wa ilani ambao unafanyika kwenye Sekta ya Afya, hususani kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa kiwango kikubwa, kama Mheshimiwa Rais ambavyo amefanya leo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kainja, wajiandae Mheshimiwa Maige na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia taarifa hii ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Kwanza, kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima. Vilevile, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kuwasilisha vizuri taarifa ya Kamati. Nawapongeza sana Wanakamati wote wa Kamati Afya na Masuala ya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna anavyofanya kazi katika Sekta ya Afya, amehakikisha anaboresha huduma. Vilevile, tuzo ambayo ameipata mchana wa leo, ambapo amepunguza vifo kutoka 556 mpaka 104, hiyo imekuwa ni dhima yake kubwa kuhakikisha vifo vya mama na mtoto tunafikia kwenye asilimia sifuri. Kwa hivyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuchangia taarifa ya Kamati, naomba nianze kwa kuchangia katika Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Ni wakati sasa wa Serikali kuhakikisha

inatekeleza kikamilifu mpango wa utekelezaji wa kukamilisha afua za UKIMWI ambao waliuzindua Tarehe Mosi Disemba, 2024 na mpango huu ulikuwa ni shirikishi katika sekta zote nchini, kuhakikisha tunatekeleza rasilimali za ndani ya nchi ili kuweza kudhibiti na kupambana na VVU pamoja na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nipende kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imeona tuna haja kubwa ya kuwa na mpango madhubuti ambao ni wa ndani wa kujiwezesha sisi wenyewe, kama Taifa, ili tuweze kujisimamia sisi kama sisi, kuhakikisha afua hizi za UKIMWI tunajisaidia kwanza, kabla ya kupata fedha kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kabisa tunaelewa Tume yetu ya Kudhibiti UKIMWI inategemea asilimia kubwa ya fedha kutoka kwa wafadhili wa nchi za nje na hususani Serikali ya Marekani, kwenye mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani, vilevile Mfuko wa Dunia wa UKIMWI, Malaria pamoja na Kifua Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya 2024/2025 katika Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* 86% ilikuwa ni fedha za nje ambazo ni sawa na shilingi bilioni 11.336 ukilinganisha na fedha za ndani ambazo ni 14%, sawa na shilingi bilioni 1.880. Kitu ambacho unaona kwa uwiano huo na tukiangalia sasa hivi wenzetu wa Marekani, Rais ametangaza anasitisha huduma katika mfuko wake huo wa dharura. Sasa hatujajua mfuko ule utasimamishwa kwa muda gani. Kama Taifa tunajipangaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishauri Serikali mpango ule ambao tuliuzindua Tarehe Mosi Disemba, 2024 wa kuhakikisha tunajisimamia tuendelee kuusimamia uweze kufanya kazi, ili kuondoa sintofahamu kwa wananchi ambao wana VVU, ambao wanatumia dawa na ambao hawatumii dawa. Inakuwa ni taharuki katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi ambao unafanyika katika nchi yetu;

naipongeza sana Serikali, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuhakikisha huduma za afya bora zinapatikana nchini. Huduma ambazo tulikuwa tunazifuata nchi za nje, kama upandikizaji wa figo, zinapatikana nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, huduma hizi zinapatikana Muhimbili, hasa za uoteshaji, utunzaji na upandikizaji wa chembe za viungo vya binadamu, zinapatikana Muhimbili pamoja na Hospitali yetu ya Kanda, ya Benjamini Mkapa. Sasa ni takribani miaka nane, lakini huduma hii inatolewa bila kuwa na sheria; hatuna sheria ya huduma hii hapa nchini ambayo itaweza kumlinda mtoa huduma na mpokea huduma ili kuondoa athari za wasiwasi wa mpokea huduma kulingana na uhakika wa afya yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iweze kuja na Muswada, ili tuweze kutunga Sheria itakayoisimamia huduma hii ambayo inaendelea kutolewa nchini na imeshafika miaka nane kama ambavyo nimesema. Vilevile, tukiwa na Sheria itaweza kutusaidia kuepukana na biashara ya viungo vya binadamu, tunasema chembe za viungo vya mwili wa binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kutunza haki za kibinadamu. Tumekuwa na matukio mengi ya kutisha ya ukatili ambapo viungo vya binadamu vinatolewa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuja na Muswada tutengeneze sheria, ili tuweze kufanya matibabu haya ambayo Mheshimiwa Rais ameruhusu na amegharamia madaktari bingwa, pamoja na vifaa ambapo inatolewa ndani ya nchi yetu katika hospitali zetu mbili za Taifa na kanda. Sheria pekee ndiyo itaweza kumlinda daktari na kumlinda anayeweza kupatiwa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Almas Maige, jiandae Mheshimiwa Lulida.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii iliyopo mezani kwetu leo, inayohusu Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo ninayodhani ni muhimu, lakini pia, naona kwamba, yanahusu ushauri wa Bunge kwa Serikali. Nayo ni Shirika letu la *OSHA* au Mamlaka ya *OSHA* ambayo yanasimamia usalama na afya mahali pa kazi na pia, *SDL* ule mfuko wa kuendeleza ujuzi wa wafanyakazi na vilevile kuendeleza ujuzi wa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi *(OSHA)*. *OSHA* ilipoanzishwa na Sheria Na.5 ya Mwaka 2003, ilikuwa na malengo na makusudio mahususi kusimamia usalama wa afya mahali pa kazi hivyo, kupunguza ajali na magonjwa ya waajiriwa au vifo mahali pa kazi. Aidha, matokeo ya usimamizi huo wa *OSHA* ungeongeza tija na uzalishaji wa mali na hatimaye kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *OSHA* ina changamoto moja sasa kwamba, Sera ile ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2010 imepitwa na wakati, imekuwa nje ya Miongozo na Kanuni za *ILO*. Hili ni Shirika la Kazi Duniani ambalo limesimamia ajira na shughuli za ajira na kusimamia waajiri, wafanyakazi, vyama vya wafanyakazi na vyama vya waajiri. Makao yake Makuu ya hili Shirika yapo Geneva na kila mwaka Tanzania inawakilishwa kule na waajiri, yenyewe kama Serikali, vyama vya wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kwenda kule Geneva tunaridhia kanuni na miongozo hii, lakini *OSHA* ili ifanye kazi vizuri ni lazima iwe na tija. Tija hii itatokana na sera ya usalama na afya mahali pa kazi endapo itaboreshwa, lakini pia, *OSHA* inakabiliwa na matatizo makubwa sana. Moja, ni upungufu wa kupanuka katika maeneo mengine ya nchi yetu, ipo sehemu chache sana. Vilevile, *OSHA* ina upungufu wa wafanyakazi na majengo maeneo ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu programu ya kukuza ujuzi na utumishi nchini, mpango umeanzishwa. Mpango mahususi ni muhimu na ulifikiwa kwa makubaliano kati ya waajiri wa sekta binafsi na Serikali, ikiwa ni sehemu kubwa ya kuboresha mazingira ya biashara nchini *(easy of doing business)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hii ikisimamiwa vizuri na kufaulu itapunguza ajira zisizo na lazima kwa wageni na pia, itatibu suala la waajiri kutafuta watumishi nje ya nchi na hivyo, kupunguza fursa kwa vijana wetu kuajiriwa hapa nchini. Waajiriwa wa kigeni wana gharama kubwa sana na hivyo, kuongeza gharama za wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hii inagharamiwa na waajiri, waajiri wanatozwa tozo ya asilimia 3.5 kwa kila mwajiriwa na tozo hii inatengeneza hela ambazo zinatakiwa ziende sasa kwa ajili ya *Skills Development Levy,* ambayo hii kodi kwa makubaliano ya Serikali na waajiri theluthi moja ya *SDL* itumike katika *program* ya kukuza waajiri, ujuzi na theluthi moja nyingine iende kwa ajili ya kukuza mikopo ya elimu ya juu. Nini kinatokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipewa na takwimu za kusikitisha kwamba fedha hii haitoki Hazina licha ya kulipiwa na waajiri. Idadi ya watarajiwa waliotakiwa kufundishwa au kupewa ujuzi huu imeshuka kutoka vijana 42,000 mpaka leo 12,000 kwa mwaka na sababu ilikuwa hela haipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maendeleo ulilenga kufundisha au kutoa ujuzi kwa watu au vijana 681,000 kupitia ujuzi ndani ya miaka mitano. Sasa vijana 136 kwa mwaka, lakini sasa hivi vijana wachache wapatao 12,000 tu wanapatikana. Hii ni upungufu mkubwa kuliko ambavyo ilikusudiwa na matokeo yake tunapoteza fursa ya vijana kusoma na kupewa ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba Mfuko huu ulikusudia pia kufundisha wafanyakazi ambao wapo kazini wakapate ujuzi, lakini mapungufu haya yanaonekana wazi wazi kwamba waajiri bado wanachukua wafanyakazi kutoka nje ya

nchi kwa kisingizio kwamba waliopo hapa nchini hawana ujuzi ni muhimu Serikali ikaongeza hela kwenye Mfuko huu ili uweze kutimiza wajibu wake kama ambavyo imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninatoa pongezi kubwa sana kwa viongozi wa Wizara zangu zote mbili, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Dorothy Gwajima, Makatibu Wakuu wote na wasaidizi wao lakini hongera kubwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuweka nia ya kuendeleza ujuzi kwa vijana wote ili waweze kupata kazi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, naunga mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lulida Riziki jiandae Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipatia hii nafasi, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia kuwepo hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kishindo kwenda kugombea akiwa mwanamke peke yake, Mwenyezi Mungu azidi kumbariki, ampe afya njema na ninasema Mwenyezi Mungu ana kadari zake na ndiyo maana aliweka Adamu na Hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake ni zamu ya wanawake na Watanzania wote tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa vile kazi aliyopewa anaifanya kwa ufanisi na hakuna mjadala wa watu aliye na macho haambiwi tazama, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa Mwenyezi Mungu ambariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nitoe pole za dhati kwa familia ya Makamu Mwenyekiti wangu wa Malaria,

Mheshimiwa marehemu Faustine Ndugulile, kwa kweli Kamati au *caucus* yetu ya malaria tumeondokewa, Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu pema peponi na familia yake ipate faraja kwa kuwa kila nafsi *dhaaikatul maut,* hakuna nafsi itakayobakia duniani, wote tutaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitazungumzia kwanza mikopo. Kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais amehangaika amepambana mpaka sasa hivi zimepelekwa fedha Benki ya *NMB* kwa ajili ya kuwakopesha vijana, wanawake na walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilonalo ni mkanganyiko mkubwa hata pa kuanzia hawa watu hawapajui. Sheria iliyopo bado haijawafanya watu hawa kujua wanazipataje zile fedha, tukichukulia sasa hivi vijana wengi wanamaliza vyuoni hawana ajira, akisema aende maendeleo ya jamii bado hakujakaa vizuri, akisema aende *NMB* nako inakuwa ni vurugu kiasi ambacho vijana hawa hawajui waende wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuisimamie na tuangalie sheria hii kwa umakini, pale kwenye mapungufu tufanye marekebisho mara moja ili kuwawezesha vijana na wanawake hawa kuweza kupata mikopo kwa urahisi na kuweza kujishughulisha katika shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, riba ipo chini, hivyo kama kweli tungesimamia hawa vijana ambao wanahangaika sasa hivi bila kuwa na kazi, tumemsikia Mheshimiwa Mbunge anasema wengi wamemaliza vyuo hawana shughuli, wameamua kuingia katika shughuli za ulevi na wale wengine baada ya kuona maamuzi yao kwa vile vichwa vyao havijatulia wameamua kuingia katika ushoga kitu ambacho si afya ya Watanzania katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande huo huo wa mikopo vilevile kuna usajili. Nimefanya tathmini mara tatu sioni majibu. Kuna usemi usemao "likupigalo ndilo likufundishalo". Leo

tunafundishwa Waafrika na tunabezwa kwa vile hatujakuwa *serious* katika utendaji wa baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunayo *population* ya watu milioni 61, lakini vijana au wanawake wangesajiliwa milioni tatu kwa shilingi 20,000 tungekuwa na bilioni 60. Narudia tena hapo, tungesajili watu milioni tatu tungekuwa na bilioni 60, hivi kulikuwa na haja ya kukopa hapo? Ina maana fedha tunayo lakini hatutaki kuzichezesha *brain* zetu, tunangojea kukopa, lakini kukopa ndiyo kunatudhalilisha sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani Waziri wa Fedha angekuwa hapa maana yake linamuhusu. Ninaomba timu ya Wizara ya Fedha, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Wanawake na Watoto ikishirikiana na Kamati tukalifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utajiuliza Dar es Salaam, Temeke peke yake, kuanzia Temeke mpaka Mbagala na wafanyabiashara wale tungekuwa tunao watu wengi sana ambao wamesajiliwa, jambo la kusikitisha mpaka sasa hivi wamesajili watu 45 lakini waliolipa ni watu 15,000. Hivi ni kweli tupo *serious* katika kuhakikisha haya mambo yanafanikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu 15,000 Tanzania nzima ndiyo waliojisajili na leo kama wamejisajili watu 15,000 zile hela benki zimekaa tu, zitachezewa tu. Ninaomba, imefika mahali Mheshimiwa Rais kama anaweza kutoa fedha sisi tumeshindwa vipi kusajili watu milioni tatu, hiki si kitu cha kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kama Wizara zote tatu zitashirikiana hasa TAMISEMI, kila Halmashauri ikaonesha ilifanya kazi gani pale alipofeli Mkurugenzi kuonesha hawa watu tunaweza tukafanya hivi vitu, lakini tukitegemea leo mkopo tumeshazuiliwa kule, hela ya makusanyo ya ndani ya kawaida imetushinda, nani wa kumlaumu? Tujilaumu wenyewe kwa vile hatupo *serious*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui niseme nini, hii ni mara ya tatu ninazungumzia suala hili, hakuna ufanisi unaoingia au mtu akasema angalau tukae chini tuone tunafanya nini! Tupo tayari kujadiliana, kama mtu haelewi hata mkifanya *calculation* mara moja mtaona kuna hizi fedha zimekaa nje hazitumiki, zinachezewa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ukusanyaji ni Wizara ya TAMISEMI, hela inakwenda Hazina, kiasi gani kila mmoja ajue kinakwenda wapi. Sasa kwa nini tusibomolewe nchi kuwa hatujitambui katika makusanyo ya fedha wakati tuna fedha ma-*billions of billions* hazina mwelekeo, hazina mpangilio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wewe ni msikivu tuifanyie kazi. Imefika muda iwe mwisho! Tulikwenda Uganda na Kamati ya Bajeti kama miaka mitano nyuma, Uganda kila mfanyabiashara ana kitambulisho shingoni, huwezi kufanya biashara yoyote pale Uganda - Nakivubo bila kuwa na kitambulisho. Sisi tunavyo vitambulisho? Watu wanauza biashara hawana vitambulisho! Sasa kama hajajisajili unategemeaje kupata mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba, kwa kweli ninampongeza Donald Trump kwa hili atatufanya Waafrika tuamke. Tunaonekana nini, unajua kila siku ukidhalilishwa lazima utapata akili ya kuweza kujitegemea, hiyo tuifanyie kazi kama kweli tupo *serious*, tuna uwezo wa kukusanya mapato zaidi ya bilioni 100 katika mwaka huu na tukipata bilioni 100 Wizara hii haitakuwa tena na mikopo wala nini, vijana wanaweza wakajiendesha katika hela yao kwa *revolving fund. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira za nje, nimewasikia wenzangu wanaongea. Tanzania tuna vijana ambao wanasoma…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Eeh! Haya bwana. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis, Mheshimiwa George Mwenisongole, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi hii na nikupongeze wewe pia kwa namna ambavyo unaendesha Bunge letu. Nami niseme machache kuhusu suala hili na ninaunga mkono hoja za Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo hatujampa Mheshimiwa Rais wetu pongezi za kutosha ni kwenye kuendeleza na kuimarisha *social safeness* ambazo ndizo zinaenda sambamba na kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii yetu, ninaamini kwamba wote tunapoenda kwenye majimbo yetu kuomba mitano tena cha kusema zaidi ni hicho tu kwamba je, tumeimarisha ustawi wa jamii, je, jamii ina furaha zaidi mwaka huu kuliko mwaka 2020 au namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kusema kweli kwenye hilo ameonesha na nataka nijiunge na wenzangu kumpongeza sana kwa kupata hiyo tuzo ambayo anapokea siku ya leo ya kuweza kupunguza vifo vya watoto kutoka 556 hadi 104, ni haki yake kabisa apokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, njia moja ya kuhakikisha kwamba wananchi wengi au kila mwananchi anashiriki kwenye mafanikio nchi hii inayopata kwenye kukuza uchumi wetu ni hili la kwamba kuna vitu, kuna huduma za jamii, kuna vitu ambavyo vinafanyika kwenye jamii ambavyo mwananchi halipii kama ambavyo ingetakiwa kama ingekuwa tu ni soko huria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa njia moja ni hii ya kuongeza na kupanua upatikanaji wa huduma za jamii kama vile afya, elimu, maji, umeme pamoja na usafiri ambao ni rahisi unaweza kufikisha mazao kwenye masoko na kwa bei nafuu, pamoja na kuhakikisha kwamba vituo vya afya, kwa upande wa vituo vya afya vipo karibu na majumba yetu na pale tunapoishi ili kwamba

mwananchi asitumie gharama kubwa katika kupata hiyo huduma na mambo mengine mengi ambayo wote tunashuhudia kwamba yamefanyika kwa ufanisi sana wakati huu wa Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninasema kwamba *income distribution* ni somo humu sana kwenye uchumi kwa sababu watu hawajui wafanye nini, mara nyingi tunaambiwa kwamba pato limekua watu hawana fedha, fedha haionekani mifukoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa kwamba fedha iliyopo mfukoni siyo ya thamani kama ile ambayo unapata bure, mtu ameshakutengenezea kupata elimu bure, matibabu bure, kupata matibabu ambayo zamani ungeyafuata kwenye nchi nyingine, lakini sasa unayapata hapa kwa bei nafuu au mara nyingine hata bure na unaweza ukasamehewa kama hujiwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa maana ile tunasema kwamba kila mtu kwa namna moja anashiriki kwenye mafanikio ya nchi yetu na naamini kwamba siyo suala tu la miundombinu, lakini ni hili la huduma za jamii ambalo naamini kwamba wenzetu wa Kamati inahusika wamelizungumza kwa ufanisi na wametoa maazimio ambayo yanakubalika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba pale kwenye jimbo langu tulipokuwa tunaingia kwenye Bunge huku mwaka ule 2020 tulikuwa na sera inayosema kwamba kila kata itapata kituo cha afya. Sasa tatizo moja ni kwamba tulivyoingia tukaeleza vizuri na tukakubali siyo tu kwamba upewe kwa sababu ni Kata, tuangalie uhitaji na kweli hiyo sera ya usawa kwenye kugawa huduma za jamii na vitu vingine ikiwa ni pamoja na *ambulance,* vituo vya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tulikubali kwa sababu ni lazima kuwe na usawa, sasa usawa unaletwa kwa namna gani? Mojawapo ya kigezo cha usawa ni kugawa kulingana na idadi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale kwenye Jimbo langu nina watu elfu mbili karibu na sabini elfu, wapo wanatakiwa wahudumiwe na vituo vitatu tu vya afya. Sasa ukiniambia kwamba hiyo ni sawa nasema usawa upo wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna *data* na mimi nataka niombe sana Wizara inayohusika na Mtakwimu wetu Mkuu wa *NBS* atoe hizi *data* kwa ufasaha zaidi ili watu wajue kwamba ni wapi pa kupeleka kituo cha afya, kama kuna *ambulance* wanagawa, ni nani apewe ngapi na kwa sababu gani. Tunasema unatoa *item per seven unit or population.* Kwa maana ya kwamba kila watu 10,000 wapate angalau zahanati, lakini kama hiyo haipo inakuwa haijaleta tija sana kwa wale watu ambao walikuwa wanafikiri kila Kata inapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli ukiangalia ukubwa wa Kata zetu naamini kwamba kila Kata na *population* ya sasa hivi ambayo tumepata kutoka sensa ilivyofanyika kila Kata ingestahili kupata kituo cha afya, niseme hilo ni sawa sana, nirudi kwenye *issue* hii ya kusema kwanza *social safeness* watu wanafikiria tu ni hiyo tu ya huduma lakini hata hili suala zima la uwezeshaji ambalo linazungumzwa hapa, uwezeshaji wa vijana, wazee, wanawake na wengine wote ambao wanaweza, hata na wazee kama mimi… Aah, mimi siyo mzee samahani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba uwezeshaji wa watu ambao wana nguvu na uwezo wa kufanya biashara au kujiajiri. Kwa hiyo naomba kwamba hili liwekewe mkazo. Ninafikiri tumekuwa tunajaribu jaribu, watu wamekuwa wanatoa mapendekezo kwamba pengine ile mifuko ya uwezeshaji iwekwe mahali pamoja au kwenye taasisi mbili ili iweze kusimamiwa vizuri na iwekezwe, *issue* ya kwamba ile mifuko yenyewe inaweza ikadhamini watu, ikadhamini mabenki yakatoa fedha nyingi zaidi ili mifuko nayo ikue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukinipa dhamana ya shilingi elfu kumi inaweza ikatoa mikopo mara kumi ya ile, lakini najua

kwamba huyu mtu *possibility* ya ku-*default* haizidi 10%. Kama mtu ana *possibility* ya ku-*default* mikopo kwa asilimia zaidi ya kumi hapewi mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ni hivyo, kama *default rate* yangu ni *ten percent* naweza nikakopesha mara kumi ile hela ambayo umenipa, kwa hiyo ninasema pengine tuliundie mchakato ili tuweze kufikia sera hiyo, tutengeneze sera ambayo inaeleweka vizuri kuhusiana na *issue* nzima ya ustawi wa jamii katika kuwasaidia watu kujiajiri na kujitengenezea kipato na wakaishi kwa furaha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo, lakini niseme tena kwamba nawapongeza wote na kwa vile kesho sitopata nafasi ya kuhutubia basi ninawapongeze wana-CCM wote kwa kutimiza miaka 48 wanayoadhimisha kesho, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mushashu jiandae Mheshimiwa Mtaturu na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii jiandae.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, vilevile na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna walivyoboresha kwa kiwango kikubwa sekta ya afya. Ninampongeza Waziri wa Afya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri Dkt. Mollel, pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri mnayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Masuala ya UKIMWI na Wajumbe wote kwa taarifa nzuri pia ninampongeza sana Mwenyekiti kwa jinsi anavyoiongoza ile Kamati katika kuishauri Serikali na kwa usomaji mzuri wa taarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeimarisha huduma za afya kwa kiwango kikubwa sana ndani ya Tanzania kama tulivyosikia, katika kipindi kifupi imeweza kuongeza vituo vya kutolea afya zaidi ya 1,368, lakini hospitali ambazo sasa zinatoa huduma ya dharura zimepanda kutoka saba zilivyokuwa mwaka 2020 na sasa hivi mwaka 2024 ni 116.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwenye hospitali zetu za rufaa za mkoa tuna *ultrasound* zimewekwa, *digital x-ray* zipo na sasa hivi watu wanafanyiwa *dialysis* huko mkoani, hawatakiwi kwenda mpaka kwenye kanda. Ukienda kwenye hospitali za taifa kuna *cath lab* na kuna *angio suite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Afrika nzima kuna nchi tano tu ndizo zenye *PET scan*. *PET scan* ni mashine ambayo inaweza ikatambua magonjwa kama saratani hata kama ndiyo imeanza tu. Nchi hizo tano ni *Egypt, Ethiopia, South Africa*, Kenya na Tanzania tumo. Kwa hiyo, tuna sababu zote za kumpongeza mama yetu kwa jinsi anavyoendelea kuboresha sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa huduma za kibingwa na kibobezi na hivyo vifaa vingi vizuri vya kisasa sasa kumeleta ukuaji wa utalii tiba. Hadi mwaka 2024, tumepata wagonjwa zaidi ya 7,843 kutoka nchi za nje ambao wamevutiwa, sasa na badala ya kwenda India na mahali pengine wanakuja Tanzania kutafuta matibabu. Ahsante sana Wizara ya Afya kwa kazi nzuri na ahsante sana Mheshimiwa Rais kwa kuboresha Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera unakumbwa na magonjwa yanayoambukiza pamoja na ya mlipuko mara kwa mara. Kiasi ambacho hata nchi jirani wakisikia kwamba kuna kaugonjwa kama *Ebola* kametokea au *Marburg*, basi unakuta watu wanaanza kuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuomba kama ambavyo tunaendelea kuomba kila siku, kwamba, kwenye mpaka kati ya Burundi na Tanzania pale Kabanga, kwenye

mpaka wa Rwanda na Tanzania pale Rusumo, kwenye mpaka wa Kyerwa na Uganda pale Morongo, tujengewe *isolation centers* ili kusudi wale wasafiri wanaokuwa wametoka kwenye nchi za jirani wakiwa wanaingia Tanzania wakishukiwa, waweze kuwa *isolated* pale pale ili kusudi wasiingie Tanzania na kuweza kusambaza magonjwa kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali walituahidi kutujengea hospitali kubwa ya kisasa ambayo itawachukua wale waliokuwa *isolated* kwamba inawezekana wana haya magonjwa ili waweze kupimwa vizuri na kupata tiba inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba mchakato unaanza lakini tunauliza, ujenzi wa hospitali hiyo unaanza lini? Kwa sababu kwa kila mwaka ni lazima kuna kamlipuko fulani Mkoani Kagera. Kwa hiyo, tunaomba Serikali walione hili, watenge fedha za kutosha ili hii hospitali kubwa ya kisasa ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia imeandikwa na Watanzania tutamkumbuka Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha uanzishwaji wa bima ya afya kwa wote. Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria hii tarehe Mosi Novemba, 2023 na Mheshimiwa Rais akawa amesaini ikawa sheria tarehe Mosi Disemba, 2023. Sasa hivi kanuni ziko tayari na sheria hii imeanza kufanya kazi tangu tarehe 13 Septemba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima hii na kitita cha huduma muhimu. Ukishakichukua kitita hiki unatibiwa wewe, mwenzi wako na wategemezi wengine wanne, yaani watu sita. Sina uhakika kama Watanzania wanajua kwamba kwenye bima hii nzuri, bima ya afya kwa wote kuna kitita kizuri kama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitita hiki watu walifikiri kwa sababu ni kitita ambacho kila mtu ni lazima akipate, kwamba labda huduma zitaishia kwenye zahanati. Kitita hiki kufuatana na kanuni zilizopo kinakuruhusu kutibiwa tangu kwenye ngazi ya zahanati na kama ugonjwa wako unahitaji kwenda mpaka hata kwenye Hospitali ya Taifa kama Muhimbili, unaweza kupelekwa

kule kwa njia ya rufaa. Kwa hiyo, ni kitita kizuri sana. Tuwahamasishe watu waweze kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili bima hii iweze kufanikiwa ni lazima kuwe na utaratibu wa kuwatambua watu ambao hawana uwezo. Ndiyo, Serikali wanasema kwamba watatumia *TASAF*, Ofisi ya Takwimu na watatumia TAMISEMI, lakini ni lazima ule utaratibu utakaotumika kumtambua yule fulani kwenye kijiji kwamba huyu ndiye hana uwezo, uainishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu zaidi ya 26% ya Watanzania wanatambuliwa kwamba ni maskini. Hatuwezi kuwabeba wote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na vigezo vya kumtambua yule ambaye hana uwezo kabisa wa kuanza kumhudumia. La siyo hivyo, huu Mfuko utaelemewa na utashindwa kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Mfuko huu au Bima ya Afya iweze kufanya kazi, vilevile Serikali ni lazima itambue vyanzo ambavyo ni endelevu. Ninajua hapa Serikali ilikuja na vyanzo ambavyo nimevitaja, lakini kwa sababu masikini ni wengi Tanzania, tunaomba Serikali iendelee kutafuta vyanzo vingine vingi zaidi ambavyo ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kila mapato yanayotokana na chanzo fulani, waainishe kinagaubaga kwamba ni asilimia ngapi kutoka kwenye chanzo hicho inaenda kwenye bima ya afya, siyo kutaja tu. Vilevile, hizo hela zikishaingia mle ziweze kulindwa, ziwe *ringfenced* na ziweze kufanya kazi ya kuwahudumia wale watu ambao hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, ugonjwa haupigi hodi. Ugonjwa unaweza ukamshambulia mtu yeyote wakati ukiwa huna hata senti tano. Kwa hiyo, ndiyo maana ninaomba Wizara ya Afya, *NHIF* na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tukiwa kwenye mikutano yetu tuendelee kuwahamasisha watu wajue kwamba mkombozi wetu ni hii bima ya afya kwa wote. Tuingie ili

kusudi sisi na wapendwa wetu tuendelee kutibiwa kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI umewatesa Watanzania wengi kwa muda mrefu. Hadi leo tuna Watanzania zaidi ya 1,700,000 ambao wanaishi na UKIMWI na wengi kati yao wako kwenye matumizi ya dawa za kurefusha maisha *(ARVs)*. Kati ya hao, 63% ya hao wenye UKIMWI ni wanawake; na ukiangalia kwenye hayo maambukizi mapya 28% ya wenye maambukizi mapya ni vijana ambao wako kati ya miaka 15 mpaka 24…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante…

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaona kwamba bado tuna tatizo lakini takwimu zinaonesha…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wageni walioko Bungeni mchana huu, Wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni watano wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mbarouk Juma Khatib, mpiga kura na Mjumbe wa Kamati ya Siasa Bumbwini Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo; wanachama 84 na walimu 10 kutoka *Club* ya Wapinga Rushwa kutoka Shule ya Sekondari Ikungi, Nkuhi, Mtaturu na Puma za Wilaya ya Ikungi Mkoani Singida. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mtaturu, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja za Kamati mbili ambazo ziko mezani. Hoja ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI na Hoja ya Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ambazo zimewasilishwa vizuri sana na Wenyeviti; Ndugu yangu Mheshimiwa Elibariki Kingu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na pia Mama yangu Fatma Toufiq kwa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa sana kwenye Sekta ya Afya. Sisi wote tunashuhudia ambavyo watu wetu wameendelea kupunguziwa mwendo wa kupata huduma za afya, lakini dawa pamoja na vifaa tiba vimekuwa vikipatikana na huduma muhimu ambazo zilikuwa hazipatikanani katika maeneo yetu sasa zinapatikana, ikiwemo mashine za *MRI* pamoja na *ultrasound,* ambayo ilikuwa inapatikana mbali kutoka kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uweze kupata matibabu sahihi kwanza ni lazima upate vipimo. Eneo la vipimo lilikuwa ni changamoto lakini kwa sasa maeneo mengi yanakwenda vizuri, na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya na dhamira yake ya kuhudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi tunampongeza Mheshimiwa Rais, kwamba angalau taasisi mbalimbali zinazohusika na mambo ya afya duniani zinamtambua katika jitihada zake na Serikali yake. Leo tunaambiwa anapata tuzo hii kwa ajili ya kupunguza vifo vya mama na mtoto, ambalo lilikuwa ni tatizo kubwa sana. Tumetoka kwenye vifo 500 mpaka 100, maana yake ni kwamba, kazi kubwa imefanyika. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nichangie katika maeneo machache katika kuongeza ushauri wangu kwenye Kamati hizi mbili. Kwanza, ninataka kupongeza kazi kubwa inayofanywa na *MSD*. *MSD* inafanya kazi kubwa sana; inasambaza dawa katika maeneo yetu ya vituo vya kutolea huduma. Tunaona magari yanavyozunguka katika maeneo ya vituo vyetu kwenye vijiji vyetu, kata na wilaya zetu. Kazi kubwa inafanywa na *MSD* katika kusambaza vifaa tiba pamoja na huduma nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo wote tunajua, na tumempongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza kwamba changamoto kubwa ni mtaji. Wenzetu wa *MSD* hawana mtaji wa kutosha. Waliomba shilingi bilioni 561 lakini wamepatiwa shilingi bilioni 100 ambayo kimsingi kwenye uwekezaji ni fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu, ninaomba waangaliwe, waongezewe hizi fedha. Kwa sababu wamelenga pia kwenda kuhakikisha kwamba kwenye vile viwanda vya kuzalisha dawa; kilichoko pale Keko, Dar es Salaam pamoja na kile kule cha Arusha *Pharmaceutical,* kimsingi ambacho ni kiwanda kizuri, kikiwezeshwa kitazalisha dawa nyingi hapa nchini na hivyo tutaondokana na kuagiza dawa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, zile fedha za kigeni zitatumika kwa kazi nyingine. Kwa hiyo, nasi tutauza nje ya nchi na tutapata fedha za kigeni ambazo tutaweza kununulia bidhaa mbalimbali tunazohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali ambayo pia ina *shares* katika Kiwanda kile cha Keko kwa 70%, kwa hiyo ni kiwanda cha Serikali; ninaomba sana wawaangalie, waweze kuwapatia fedha kwa ajili ya kufanya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, tumeona wamepandisha mapato kutoka shilingi bilioni 378 hadi shilingi

bilioni 553. Hili siyo jambo dogo, ni jambo kubwa. Tunawapongeza sana taasisi hii kwa kuweza kuongeza mapato na tunampongeza Mkurugenzi, *Mr.* Mavere pamoja na menejimenti yake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia *MSD*. Hongera sana, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunao wenzetu wa *NHIF* ambao wanasimamia suala la bima ya afya kwa wananchi. Kwenye eneo hili tumeeleza kwamba tumekuja na mfumo huu wa bima ya afya kwa wote. Ni kazi nzuri, lakini hawa wenzetu wa bima ya afya wakiwezeshwa wataweza kufanya kazi sana kwa kutumia bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana kwamba mifumo ya kudhibiti mapato iimarishwe kwa kusomana kama ambavyo tumeona imeelezwa kwenye Kamati. Yale wanayoyahitaji yakifanyika vizuri, vituo vikasomana, tutaondokana na watu kufanya mambo ambayo hayako sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupoteza mapato nalo linaweza likadhibitiwa vizuri na kuufanya Mfuko kuwa na uwezo wa kuwahudumia wananchi wetu na kuweza kuongeza uwezo mkubwa wa kuweza kuhudumia wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili tunampongeza Mkurugenzi, dada yetu Ndugu Irene pamoja na wenzake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba wanaboresha Mfuko huu. Zaidi tumeona, kwamba wamepandisha mapato kutoka shilingi bilioni 696 mpaka shilingi bilioni 756. Mifumo ikisomana vizuri tutaona namna ambavyo watapandisha zaidi kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kwenye eneo la mikopo. Mikopo hii ilitolewa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kujiwezesha kiuchumi. Tuliangalia Mfuko kwenye maeneo mengi, ambapo huko nyuma Mfuko haukufanya vizuri sana; lakini kwa sasa tumekuja na mfumo mpya kwenye fedha hizi. Tunampongeza

Mheshimiwa Rais kwa kuruhusu wananchi kwenda kukopa tena katika fedha hizi. Kwa hiyo, makundi haya ni matatu, wanawake, vijana pamoja na wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema kwamba wamepeleka kwenye benki. Wananchi wengi hawajui vizuri mfumo wa kwenda kufuata fedha hizi. Ninaomba sana Serikali iweke mfumo rahisi ili wananchi wafikiwe na vikundi hivi viweze kuchukua zile fedha kwa ajili ya kujiwezesha kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili kumekuwa na kilio cha akinababa ambao nao wanatuambia kwamba, asilimia 10 mbona haziwagusi? Kwa hiyo, wazee wanalalamika kule kwenye maeneo mengi; wanasema na wao waguswe na fedha hizi kwa sababu wao pia wanatunza familia. Kwa hiyo, leo wakishazaa watoto vijana wakawaacha pale, maana yake wao wanaachwa wanakuwa kama *second hand.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wazee wanasema nao waangaliwe ili Mfuko wao uweze kupatikana. Kama hatuna Mfuko wa kuwapa fedha bure, basi wapewe za mkopo ili waweze kuimarika, na kwa hakika wawe na sauti kwenye nyumba kwa sababu akinababa nao wanaona wameachwa nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba Serikali nayo iende kuangalia upya. Mheshimiwa Rais anawapenda wazee, ambapo kama kweli wazee ni dawa basi wawe na uwezo wa kiuchumi ili waweze kuzisimamia familia zao, wasiwe wanyonge na waondoke kwenye unyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, ninaunga mkono hoja. Ninasema ahsante sana kwa mchango huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, ujiandae. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema. Ninakupongeza wewe kwa kuendesha Bunge hili Tukufu. Pia, ninapenda kuipongeza Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa hoja zao katika Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Kamati kwa ushirikiano ambao wanatupa katika Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Tumepokea ushauri wao na tunatekeleza vizuri kwa ushirikiano wanaotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru pia,Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa na upeo na kuona kuunda Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. Sasa wananchi wameweza kuona umuhimu wa wizara hii na wananchi wengi wanakuja kutatuliwa changamoto zao za kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja mbalimbali ambazo zinawahusu wananchi. Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum tunafanya nao kazi vizuri na tuko karibu nao; na sasa hivi tayari utaratibu kuhusu mikopo ya wafanyabiashara wadogo wadogo umeshakamilika, fedha zimeanza kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upendo kwa wananchi wa Tanzania tayari Mheshimiwa Rais ametoa fedha shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii walioko katika halmashauri zote nchini Tanzania kuhakikisha wananchi wanakwenda *NMB* na kuchukua vitambulisho vya

kielektroniki ili kuhakikisha wanapata mikopo hiyo na kuweza kujiwezesha wenyewe kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza bajeti ya vyuo vyote vya maendeleo ya jamii. Hadi sasa Mheshimiwa Rais ametuwekea fedha za ujenzi, fedha za *hostel* na fedha ambazo zitasaidia vibali vya ajira ili kuhakikisha kwamba vyuo vyetu vinaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 12.665 zimewekwa kwa ajili ya kuendesha vyuo hivi. Hii ni fursa nzuri kwa wananchi wetu kuhakikisha wanapata elimu hii ya maendeleo ya jamii ili waweze kujiwezesha wenyewe na pia kuleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa, kutorejeshwa fedha tulizozitoa za *WDF* ambazo tumewapa wananchi mikopo hiyo. Sasa hivi tumeshaunda Kamati ambayo itawawezesha kukusanya fedha hizi na kurejesha na kuwapatia wananchi wengine, ili kuhakikisha fedha hizi zinatoa msaada na wananchi wengine kupokea mikopo kama hii kutoka *WDF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuwezesha na kutuunganisha na mataifa mbalimbali. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais ametuunganisha na tumeingia mkataba na Benki ya Dunia kwa zaidi ya shilingi bilioni 248 tumefunga nazo mkataba. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuwakopesha wananchi wadogo wadogo hasa wanawake kwa riba nafuu ili kuhakikisha wanawake wetu wanaweza kujiendesha kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake kwa maono yake na upeo wake ambao analenga kwa wananchi wa Tanzania kuhakikisha wanapata fursa wanazozihitaji katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu ya mikopo kwa wananchi wote kupitia vyombo vya habari mbalimbali ambavyo vitawafikia wananchi hadi vijijini ili kuhakikisha kuwa wanapata fursa hizi nzuri za mikopo midogo midogo ili waweze kujiwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia na madhumuni ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wote wanapata fedha hizi na kuondokana na umaskini, matatizo na changamoto zote za maisha ambazo zinawakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mdogo sana. Kutokana na mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia na maelekezo ambayo wametupa, Serikali tutazifanyia kazi hoja zote na maazimio yote ya Kamati ambayo yametolewa hapa na kushirikiana vizuri kuhakikisha Serikali hii inakwenda vizuri kama Mheshimiwa Rais anavyotuelekeza sisi wasaidizi wake kuhakikisha wananchi wote wanakuwa salama na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa michango yote ya Kamati na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wanaotupa. Sisi tuko tayari, mlango yetu Wizara ya Maendeleo ya Jamii iko wazi kuhakikisha tunashirikiana pamoja na wananchi wote. Ahsanteni sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kutuongoza, lakini nilishukuru Bunge lako Tukufu kwa mambo makubwa ambayo amekuwa akitushauri. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa kweli na Kamati yetu imekuwa ikituongoza vizuri sana sisi Wizara ya Afya. Niwashukuru pia Viongozi wote wanaotuongoza ndani ya hili Bunge, lakini pia na *Chief Whip* wetu jinsi ambavyo anatupangilia vizuri katika kucheza mechi ndani ya hili Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliombe Bunge lako kwa sababu ya muda waniazime tafakuri ya kina kwa muda mfupi ili nitumie maneno machache, lakini ili wote kwa pamoja tuweze kumwelewa aina ya Mheshimiwa Rais ambaye tunaye sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaye Mheshimiwa Rais ambaye hafikirii tu kutatua matatizo madogo madogo yanayoibuka ndani ya nchi yetu na matatizo ambayo yanaonekana na watu katika ulimwengu wa damu na nyama, lakini Mheshimiwa Rais huyu anaifikiria Tanzania ya miaka 100 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais huyu anajua kwa nini siri ya tofauti ya Mataifa yenye nguvu na Mataifa maskini; siri ni nini? Mheshimiwa Rais huyu anajua kwamba siri siyo uwepo wa rasilimali na ukubwa wa nchi na mambo mengine, lakini siri ya Mataifa hayo ni uwepo wa watu wenye akili iliyopitiliza upeo wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Rais huyu amejua kwamba leo tupo kwenye dunia ambayo tunazungumzia *artificial intelligence* ambayo sasa inaanza kupitiliza hata ule uwezo wa akili ya kawaida wa binadamu na Mheshimiwa Rais huyu anajua leo *artificial intelligence* tunayoiona leo ni suluhu wa mambo mengi inaenda kuunganishwa na *quantum computing.*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakapounganisha hayo mambo mawili tutakuta tunahitaji binadamu wenye uwezo wa kufikiri kwa namna ya ajabu sana ili na sisi tuweze ku-*compete* na Mataifa mengine. Mheshimiwa Rais huyu ndiyo maana aliposimama hapa kwa mara ya kwanza alipofika eneo la mama na mtoto alirudia na kuongea kwa pozi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuishia hapo aliweka *resources.* Leo ndiyo maana unaona dunia ipo Tanzania siku hii ya leo ikimpa Mheshimiwa Rais wetu nishani kwenye kushusha vifo vya

akinamama kuliko ilivyotegemea kutoka 556 mpaka 104 yaani mwaka juzi na ilitegemewa ni mwaka huu. Leo dunia ipo na *Gate Foundation* na *Goalkeepers* wapo hapa Tanzania. Hawapo hivyo; matokeo haya yametokana na nini? Yametokana na *resources* aliyoingiza kwenye huduma ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuingiza *resources* lengo siyo kuokoa vifo vya akinamama na watoto, ndiyo maana unamwona amesaini mkataba na wakuu wa mikoa wa lishe. Mheshimiwa Rais wetu pamoja na kuhudumia huduma ya mama na mtoto anajua ili upate Taifa la watu wenye akili unaanza kumwangalia mtoto toka akiwa tumboni kwa mama yake akiwa ana miaka *zero*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake unaingiza *resources* kuanzia hapo, unaingiza lishe kwenye mama, unaingiza huduma zote ndiyo pale unapokwenda akazaliwa mtoto mwenye ubongo uliojengeka vizuri ambao una uwezo wa kuelewa mambo yaliyopitiliza upeo wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake chakula na mambo mengine huduma zote ndiyo zinatengeneza *wiring* ya ubongo. Usipotengeneza namna hiyo unakuwa na watu ambao wana ubongo lakini ubongo huo umeme *GB* chache tu zikiingizwa unaanza kupata moto, lakini ukiwa na ubongo uliojengwa vizuri wenye *wiring* ya kutosha hata upige *GB* kubwa kiasi gani una uwezo wa kupokea na kuchakata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana utaona kwamba kuna wakati mwingine watu wanajua kupokea mdude kitu chochote kizima kizima na kumeza kizima kizima, lakini ubongo uliochakatwa ukipokea chochote unachakata, unameng'enya na unafikiria *beyond* mwonekano wa macho ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndicho Mheshimiwa Rais anataka hizo akili tuzipate Tanzania. Ndiyo maana umemsikia akishazaliwa huyo mtoto sasa mwenye huo ubongo uliojengeka kwa afya nzuri na huduma nzuri za afya na lishe nzuri inahitaji elimu bora; ndiyo maana umemwona Mheshimiwa Rais huyu amewekeza sana

kwenye elimu na juzi hapa amezindua mtaala. Anazindua mtaala ambao unakuja ubongo mkubwa; huo mtaala je, una uwezo wa kusisimua huo ubongo mkubwa uweze kufikiria kwa namna ambayo unaweza kuona mambo yasiyoonekana? Ndiyo huyo Mheshimiwa Rais ambaye tunaye, anayetutayarishia Taifa la kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge tembeeni kifua mbele kwenye maeneo yote na kwenye eneo la afya na yote mliyoyasema, sisi kama afya tunayachukua. Tumeshamsikia Mheshimiwa Rais alichokisema na tunaenda kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa moja tu kwa kuwaambia kwamba mmesema eneo la afya kwa maana ya elimu kwenye afya na utoaji wa elimu. Naombeni Waheshimiwa Wabunge waturuhusu kuendelea kuhakikisha vichwa hivi vizuri ambavyo Mheshimiwa Rais wetu anaanza kuvitengeneza vya miaka 100 ijayo ndiyo vinaingia kwenye taaluma ya afya kwa sababu kwenye afya ukikosewa aidha umekuwa mlemavu au umekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria ukikosea una uwezo wa kukata rufaa, Mahakama nyingine ikakupa haki, lakini kwenye afya tunasababisha walemavu na mambo mengine. Ni eneo tunalohitaji tupate watu *smart* sana. Pia, Wabunge watakuwa wamesikia tunapokea watu sasa kutoka nje kuwatibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashindano hayo siyo ya teknolojia tu, mashindano hayo pia ni ya kupata *brain* nzuri zenye kuweza ku-*compete* na kufanya mambo kwa namna ambayo watu wengine hawawezi kufanya ndipo tunageuza Taifa letu linakuwa *pool* la kila mtu kuwa kimbilio lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba waendelee kutukubalia tuendelee kuhakikisha tunaweka *tight measurement* kuhakikisha watu wanaoingia huko kwenye kutibu watu wanakuja

watu ambao tuna uhakika kwamba wana uwezo wa kufanya hayo mambo yanayohusu maisha ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwaambia Mheshimiwa Rais huyu alichokifanya kwenye afya pamoja na ugumu wa bajeti na mambo mengine haijatatua tu matatizo ya Watanzania kwenye eneo la afya, imetatua na matatizo ya majirani zake. Maana yake leo walikuwa Zambia, Rwanda kwingine kote Msumbiji, Comoro mnaona wakisaini mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuwa watumie hela nyingi sana kwenda Ulaya na India leo wanakuja hapa karibu Tanzania kupata suluhu ya matatizo yao na fedha nyingine wanazibakiza nchini kwao kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais huyu ni Mheshimiwa Rais ambaye anatazama *beyond measure,* ni Mheshimiwa Rais ambaye ameleta suluhu za Tanzania na ameleta suluhu za nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waendelee kutukubalia, waendelee kutuunga mkono, waendelee kumuunga Mheshimiwa Rais wetu huyu mkono, tutembee kifua mbele kwa sababu tupo mikono salama ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na yote ambayo wametuelekeza waliyoyasema sisi kama afya tupo kifua mbele, tuna uhakika 100% yataenda kutekelezeka kwa sababu tuna jemedari wetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya

kuhitimisha hoja yetu. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia ni Waheshimiwa Wabunge sita, lakini pia Waheshimiwa Mawaziri ambao wamechangia ni Waheshimiwa Mawaziri wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchache labda niwabainishe hao Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia ni Mheshimiwa Msambatavangu, Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Kimei pamoja na Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizojitokeza zaidi ni kwamba fedha za machinga kutotolewa kwa muda mrefu na kasi ndogo na pia katika uandikishaji unaosuasua kwa hawa wamachinga. Kwa hiyo kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wanaendelea kulifanyia kazi na yale maoni ya Kamati tuliyoyatoa wataendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa ni kuhusiana na mikopo ya Mfuko wa Wanawake *(WDF)* kwamba fedha hizi zinatakiwa zirejeshwe kwa wakati kwani kuna baadhi ya halmashauri zilikopeshwa fedha hizi. Kwa hiyo inabidi zile halmashauri ambazo zimechukua hizi fedha zirudishe ili kusudi kwa sababu ule Mfuko ni *revolving* ili kusudi wanufaika wengine waweze kupata. Ni budi sasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii pamoja na TAMISEMI washirikiane kuhakikisha kwamba fedha hizi zinarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba kwenye suala zima la usimamizi kwenye ile *program* ya ufanisi wa kukuza ujuzi kwamba katika *program* ile ambapo inaonyesha kabisa kwamba inabidi Watanzania wengi zaidi waweze kupata fursa hii. Inaonekana napo bado kwenye kukuza ule ujuzi Watanzania wengi hawashiriki. Imeshauriwa kwamba walau ifikie hata 50% ili kusudi Watanzania au wale vijana wanaokuza ujuzi waweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni kwamba imeshauriwa hawa vijana wanaomaliza kupata yale mafunzo katika kukuza ujuzi waweze kupewa vitendea kazi. Hata hivyo, wameenda mbali zaidi kwamba kwenye hili suala la kukuza ujuzi kwa sababu *program* hii pia inataka wale wawekezaji wanaokuja hapa nchini waweze kutoa ujuzi kwa wale vijana wa hapa kwetu ili tuweze kupunguza kuleta ma-*expatriate* au kuleta wataalam kutoka nje. Hii nayo imezungumziwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Serikali ifanyie kazi kwa kuhakikisha kwamba Watanzania wengi na kwa wakati wanapata mafunzo haya ili mwisho wa siku sasa wale vijana waweze kuajirika hapa badala ya kutegemea wale wawekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limejitokeza ni kwamba waajiriwa na wastaafu kulipwa fdha za michango ya waajiri wao. Yaani kwamba wale wastaafu wanapokuwa wamefikia wakati wa kustaafu, kuna baadhi ya michango yao inakuwa haijaenda kule kwa hiyo kuna baadhi ya wastaafu ilibidi walipe zile fedha ili kusudi waweze kupata zile fedha zao za kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo tumelizungumza sana na bahati nzuri Sheria kabisa tumeshaipitisha. Kwa hiyo kuanzia sasa hivi ina maana kwamba mifuko yote hii haitafuatilia iwapo kama mwajiri hajapeleka michango basi wale wanufaika watatakiwa walipwe mafao yao na wakishalipwa mafao yao itabidi sasa mifuko ndiyo iendelee kufuatilia katika hizi halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limejitokeza ni kwamba inabidi kuwepo na *data* za kutosha kwa wale wote waliojengewa uwezo kwenye hili suala la kukuza ujuzi. Kwa upande wa *OSHA* kwamba sera ya usalama na afya mahali pa kazi inatakiwa irejewe upya kwa sababu inaonekana kwamba imepitwa na wakati. Kwa hiyo hii pia imezungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba kwenye suala la mifuko wamezungumzia ufanisi wa Mifuko. Ninapenda kusema kwamba, nadhani Serikali ilipofanya *revision* ya kuona kwamba Mifuko hii fedha zipelekwe benki ili kusudi ziwe salama zaidi baada ya kuonekana kwamba kulikuwa na mianya, niendelee tu kuwashauri Waheshimiwa Wabunge turidhiane na masuala ya Serikali kuona kwamba fedha hizi zipitie benki ili kusudi wanufaika wengi waweze kupata hasa wale wanaostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri ambao wamechangia hoja. Pia, kwa namna ya kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuhakikisha kwamba ustawi na maendeleo ya Watanzania yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa 2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa 2024 ilipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**NAIBU SPIKA:** Wote mmeafiki. Sasa hili ni Azimio rasmi la Bunge kwenda Serikalini.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kutupa muda sisi Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI kutoa taarifa yetu ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa mwaka 2024/2025 ambayo imeishia Januari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa na mengi sana ya kusema, lakini naomba niweke kumbukumbu vizuri. Mwanzo niliteleza kwa kusema kwamba Mheshimiwa Rais tuzo anayopokea leo siyo ya kupunguza vifo vya watoto ni vifo vya kina mama kutoka vifo 556 mpaka vifo 104.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi malengo yaliyokuwa yamewekwa na *WHO* yalikuwa ni kufikia vifo 225 kwa hiyo Tanzania Mheshimiwa Rais wetu na Serikali wamekwenda *beyond* kwa hiyo hatuna sababu ya kuacha kuwapongeza katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamechangia wachangiaji wengi. Wengi wameunga mkono mapendekezo na ushauri uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, wengi wameunga mapendekezo kwa mfano pendekezo la kuiomba Serikali ya kuitaka Serikali iweze kutoa mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni 460 kwa *Medical Stores Department* ili kuwawezesha kufanya uwekezaji, ununuzi, uhifadhi na usambazi wa madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, amechangia Mheshimiwa Sanga, ameshindilia kwenye hilo na Mheshimiwa Jacqueline ameshindilia kwenye hilo. Pia, amechangia Mheshimiwa Mwandabila amezungumzia masuala ya kuhakikisha kwamba tuwe na hospitali mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiona hapo kubwa ni kuiomba Serikali iendelee kufanya uwekezaji kwa hospitali zetu za

ndani kwa kufanya *public private partnership.* Kwa mfano tulizungumza hata kwenye Kamati yetu hivi karibuni tunayo hospitali ya *Arusha Lutheran Medical Centre* ambayo tuliishauri Serikali waingie nayo ubia badala ya kwenda kuwekeza kujenga majengo mapya, wanaweza kuingia ubia wakapeleka vifaatiba, mitaji na mambo mengine shughuli zikaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Mwandabila inaweza kuwa *solved* kwa kuhakikisha kwamba Serikali inaendelea kuwekeza katika hospitali zetu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Mushashu ninampongeza pia mama yangu na Mjumbe wa Kamati ametoa sifa na pongezi kwa Serikali, lakini pia ameomba Kagera wajengewe *centre* kwa ajili ya karantini kutokana na wingi wa milipuko ya magonjwa. Hilo jambo pia nafikiri ninaliafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, bima ya afya kwa wote watu wameendelea kusema elimu ya umma iendelee kutolewa na Mheshimiwa Mtaturu kaka yangu amempongeza Mheshimiwa Rais na pia ameomba mtaji kwa *MSD* wapewe. Amewapongeza watu wa *NHIF* kwa kuongeza mapato, lakini amesisitiza watu wa *NHIF* waimarishe mifumo yao ya huduma ili kuhakikisha kwamba ubadhirifu na upotevu wa fedha za Serikali zinazopotea uweze kudhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikiri kwa kifupi sana pamoja na changamoto nyingi ambazo kama Kamati tunaziona zipo nikiri Serikali wanafanya kazi kubwa sana katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata takwimu zinaonyesha; kwa mfano mpaka mwaka jana tumeweza kupata wageni kutoka nje ya nchi ambao jambo hili lilikuwa geni kwa nchi yetu, zaidi ya watu 11,332 wametoka nje ya nchi wamekuja kutibiwa Tanzania. Vifaatiba vya kisasa, tumekuwa na *digital x-ray,* tumekuwa na mashine za *MRI,* tumekuwa na mashine *digital*

za *ultra sound* vitu ambavyo mwanszo vilikuwa ni hadithi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna sababu ya kuendelea kuiunga mkono Serikali na pale ambapo Bunge tutapaswa kuishauri na kuona kwamba kuna mambo hayaendi vizuri hatutapepesa jicho kuiambia Serikali lakini pale itakapofanya vizuri tutaendelea kuipongeza ili kuwatia moyo waendelee kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana wewe binafsi, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru tena kwa mara ya pili, ahsante sana kwa kutupa nafasi. Baada ya kusema hayo ninatoa hoja ahsanteni sana.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu kupokea na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2024 na Maazimio ya Bunge kwa Serikali. Wote mmeafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2024 ilipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**NAIBU SPIKA:** Nawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti, mmefanya kazi nzuri sana na kwa kweli mnastahili pongezi ninyi na Wajumbe wenu na michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo imetolewa hapa. Pia, pongezi kwa majibu ya Serikali ya

Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote wawili kwa namna walivyokwenda mbele zaidi kueleza umuhimu na mambo yanayofanywa na Serikali.

Tanzania leo tuna mtambo wa *PEX* nafikiri Mheshimiwa Dkt. Mollel hujaismea hili vizuri hii *PEX* imefungwa pale *Ocean Road* ina uwezo wa kutambua vinyemela vya kansa *in advance*. Kwa maana ukishajiona unapata kitu kama hiki mtambo unaonyesha na unatibiwa na unapunguza madhara ya kansa kwa Watanzania. Mtambo huu katika nchi zetu za hapa jirani nafikiri upo Tanzania tu. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais Mama Samia apewe maua yake kwa kitu kama hicho alichokifanya. *(Makofi)*

Kwenye sherehe aliyoifanya Ndugu Haji Manara pale *Ocean Road* tulikwenda na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alikuwa ndiyo Mgeni Rasmi, tumeona taarifa za wagonjwa wa kansa kupungua kwa sababu Mheshimiwa Rais amepeleka mitambo ya *CT-Scan* wameweza Watanzania kugundua athari za ugonjwa huu na mapema na kuweza kuingia katika *program* na *protocol* za *treatment* na wanapata dawa na sasa hivi wanaendelea vizuri wanaondoka na athari za kuwa na kansa kwa siku za mbele. *(Makofi)*

Huyu ndiyo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunavyomsifia kuna watu hawapendi. Sasa sisi tunasema ugonjwa hauna chama, usifiche maradhi nyumbani njoo pale *Ocean Road* tutakutibu. Tunawajua wenye ugonjwa huo. *(Makofi/Vicheko)*

Baada ya maneno haya machache, ninawashukuru sana. Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.19 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 5 Februari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*